**24 APRILI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 24 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe*. Mussa Azzan Zungu*) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI.**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE.MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 145

### Mkakati wa kukuza ujuzi na stadi kwa vijana

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. LATIFA K. JUAKALI** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali wa kukuza ujuzi na stadi kwa vijana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifah Khamis Juakali Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza ujuzi na stadi za kazi kwa vijana, Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ujuzi wa miaka 10 (2016/2017 na 2025/2026) ambapo umelenga kuhakikisha nguvu kazi ya vijana inashiriki katika kujenga uchumi wa Taifa. Mkakati huu unatekelezwa kupitia program na mipango mbalimbali ya kukuza ujuzi na stadi kwa vijana inayotekelezwa na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baadhi ya programu na mipango hiyo ni pamoja Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambayo tangu kuanza kutekelezwa mwaka 2016/2017 imetoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa jumla ya vijana 118,415 na Mpango wa Mafunzo na Uwezeshaji wa Vijana kushiriki kilimo unaotekelezwa na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu lakini kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika,nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali; nina maswali mawili ya nyongeza.

i. Serikali inatumia mfumo gani kutathmini tija na matokeo ya programu hizo hasa ukizingatia kasi kubwa ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia iliyopo sasa?

ii. Serikali ina makakati gani wa kuhakikisha kwamba Vijana wengi wananufaika na programu hizo ukizingatia uhitaji ni mkubwa kuliko nafasi zinazopatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI, MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ameuliza maswali mawili ya nyongeza; la kwanza ni kuhusu mfumo wa namna gani tunafanya tathmini kwa vijana hawa. Chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ipo Idara ya Maendeleo ya Vijana. Chini ya mkurugenzi huyo kuna timu maalum ambayo inafanya tathmini ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo na utaratibu wa kuweka kanzidata katika vyuo husika ambavyo tunawapitisha vijana hao kupata mafunzo. Kwa hiyo tunabaki na takwimu kwa ajili ya kuwawezesha pia baada ya mafunzo waweze kupata fursa za ajira lakini zaidi tunawapa pia hadi vifaa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika,kuhusu swali la pili nalo ameuliza kuhusu vijana, sikuweza kulipata vizuri nikuombe kwa ridhaa yako, niweze kulisikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili halikusikika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Husikia, swali la pili.

**MHE.NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili lilikuwa ni kwamba; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vijana wengi zaidi wananufaika na *programme* hizo ukizingatia uhitaji ni mkubwa kuliko nafasi zinazopatikana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati ambayo Wizara imeweka ni pamoja na huo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya kuhakikisha vijana wengi wanaingia kwenye *blue economy,* kwa maana ya ufugaji wa samaki. Mkakati mwingine ni huu wa ukuzaji ujuzi ambapo tayari tumefundisha vijana zaidi ya 74,598, lakini pili upo mkakati mwingine huu ambao uko chini ya Wizara ya Kilimo unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu wa *BBT* ambapo tayari vijana 821, na Mheshimiwa Rais alizindua *programme* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mkakati mwingine kupitia *NACTVET* pamoja na mafunzo ya *TEHAMA* ambayo tunaendelea nayo. Vilevile tuna Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa ambao unatutaka tuweze kuwafikia vijana zaidi ya 681,000 kwa kipindi hiki katika mpango huo wa miaka mitano. Tayari Serikali imeanza *engagement* na wadau wa maendeleo wakiwemo *GIZ*, *International Labour Organisation* pamoja na wadau wengine ni pamoja na Serikali yenyewe katika kuweka fedha kuhakikisha mafunzo haya tunayatoa kwa vijana walio wengi zaidi na kuwatafutia ajira ndani na nje ya nchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais Mheshimiwa Mtaturu.

Na. 146

**Kujenga Soko la Kisasa – Ikungi**

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kujenga soko la kisasa Ikungi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imeweka mpango wa kujenga soko la kisasa katika Kijiji cha Ikungi lenye ukubwa wa ekari mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa halmashauri inaendelea kufanya mazungumuzo na wananchi ambao wamejenga vibanda vya biashara katika eneo hilo lililoainishwa na mipango miji kwa ujenzi wa soko la kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwa kushirikiana na *UN WOMEN* imekamilisha ujenzi wa jengo la mabucha na mbogamboga lenye thamani ya shilingi milioni 82 katika eneo hilo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa soko la kisasa Ikungi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; lakini pia naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, changamoto iliyopo hapo Ikungi ni sawa sawa na iliyopo katika Jimbo la Singida Kaskazini katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambapo tulisha wasilisha maandiko kwa ajili ya kupatiwa soko la kisasa katika mji wa Melya njia panda ya Melya lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

Je, Serikali inatoa *commitment* gani kwa ajili ya kujenga soko hilo la kisasa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi?

Swali la pili, Mji wa Ikungi pamoja na Singida Kaskazini hazina stendi zinazoeleweka za kisasa kwa ajili ya magari kuingia na kutoka. Je,Serikali sasa itajenga lini stendi hizo kwa ajili ya kupendezesha miji yetu lakini pia hata kuingizia mapato halmashauri zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Igondo Ramadhani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii ambayo pia iko katika Jimbo la Singida Kaskazini Halmashauri ya Singida la kukosa soko, na niwapongeze Halmashauri ya Singida kwa sababu tayari kweli walishawasilisha andiko mkakati kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Ikungi pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Singida Kaskazini kwamba Serikali inaendelea na uchambuzi wa maandiko yale kuona kama yanakidhi vigezo vya kuwa

miradi ya kimkakati ili fedha ziweze kutafutwa kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na changamoto ya stendi ya mabasi, Serikali imeshaweka mpango kazi kwenye halmashauri zetu zote kuanza kuainisha maeneo ambayo yanatakiwa kujenga stendi lakini pili kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani pamoja na Serikali kuu kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga maeneo hayo. Kwa hiyo Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Stendi hizo zinajengwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; kwa kuwa uko mradi wa *TACTIC* wa kujenga soko la kisasa pale Ipembe lakini na soko la vitunguu. Nataka kujua ni lini mradi huu utatekelezwa ili wananchi waweze kupata huduma stahiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *TATCTIC* una awamu tatu. Awamu ya kwanza tayari iko hatua ya kutafuta wakandarasi, awamu ya pili iko hatua ya usanifu wa mwisho na awamu ya tatu itafanyiwa usanifu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla ya mwaka 2025 Serikali imeweka *commitment* kuhakikisha kwamba miradi yote ya *TACTIC* itakuwa imekamilika kwa sehemu na mingi iko kwenye utekelezaji hatua za mwisho, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mji wa chemba unakuwa kwa kasi lakini hauna soko kabisa. Naomba kujua mkakati wa Serikali wa kujenga soko pale kwenye mji wa Chemba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze Mkurugenzi wa halmashauri ya Chemba kuainisha na kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa soko na kuleta andiko la kuona uwezo wa halmashauri kwa mapato ya ndani yanafikia eneo gani ili Serikali Kuu iweze kuona sehemu gani inahitaji kuchangia ili kujenga soko katika mji huu wa Chemba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Maganga.

Na. 147

**Kuwasaidia watu wenye ulemavu kupata mitaji Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Watu Wenye Ulemavu mitaji katika Jimbo la Mbogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ilitenga shilingi milioni 56 kwa ajili ya mikopo ya watu wenye ulemavu. Hadi kufikia mwezi marchi, 2023 jumla ya vikundi 6 vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa kiasi cha shilingi milioni 34. Fedha hizi zimewezesha vikundi vya watu wenye ulemavu kuanzisha biashara na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe imetenga shilingi milioni 56.19 kwa ajili ya mikopo isio na riba kwa vikundi vya watu wenye ulemavu. Fedha hizi zitatolewa kupitia mfumo ulioboreshwa wa asilimia 10, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE.NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Swali la kwanza, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia walemavu ambao hawajiwezi kujiunga na vikundi, kuwasaidia angalau baiskeli ya kutembelea?

Swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri uko tayari baada ya Bunge hili tuongazane mimi na wewe kwenda kuwatambua walemavu walioko Mbogwe na kuwasikiliza shida zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali wawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa au utaratibu wa mikopo ya asilimia kumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kundi la watu wenye ulemavu hawalazimiki kujiunga kwenye vikundi, hata mmoja anaweza akakopeshwa mkopo kama yeye na akafanya shughuli zake za ujasiriamali. Tayari wengi wameendelea kupata huduma hiyo kwa kupata mkopo kwa mtu moja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na viti mwendo kwa watu wenye ulemavu utaratibu wa Serikali upo na maafisa maendeleo ya jamii katika maeneo hayo wanaainisha. Tunahusiana na wadau mbalimbali wanaendelea kuwasaidia. Kwa hiyo nitoe wito kwa halmashauri ya Mbogwe kuwatambua watu wenye ulemavu wanaohitaji viti mwendo ili Serikali iweze kuona namna ya kushirikiana na wadau katika kuwawezesha kupata viti mwendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili la bajeti ili twende Mbogwe tuweze kupitia baadhi ya vikundi ambavyo vimenufaika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa kuwa Serikali imesimamisha kwa

muda utoaji wa mikopo ya asilimia kumi kwa mfumo uliopo mwanzo, na sasa hivi halmashuri hazitoi tena, ni lini serikali inakusudia kuleta hapa mwongozo wa utoaji mikopo hiyo ambao tutaupitia kwa pamoja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Constantine Kanyasu Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesitisha kwa muda utaoji wa mikopo wa asilimia kumi ili kupitia mwongozo vizuri ili kuhakikisha kwamba fedha ambazo zinakopeshwa zinarejeshwa lakini zinakuwa na tija zaidi kwa vikundi ambavyo vinakopeswa. Serikali iko kwenye hatua ya kuupitia mwongozo huo na mara utakapo kuwa tayari Waheshimiwa Wabunge wataufahamu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa David Mwakipose Kihenzile.

Na. 148

**Uhitaji wa magari ya kubebea wagonjwa – Vituo vya Afya Mufindi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka magari ya kubebea wagonjwa katika Vituo vya Afya vya Mtwango na Mgololo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu na uhitaji wa magari ya kubebea wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kwa kutambua mahitaji yaliyopo, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga shilingi bilioni 35.1 kwa ajili ya ununuzi wa magari 316 ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za manunuzi zinaendelea na magari hayo yatagawiwa kwenye halmashauri zote 184 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ambayo itapewa magari 2 ya kubebea wagonjwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuahidi kuleta magari mawili kwenye hivi vituo viwili cha Mtwango pamoja na cha Mgololo. Swali langu la nyongeza ni moja.

Je, kwa kuwa wananchi katika maeneo haya wameonesha jitihada kubwa za kuanza kujenga vituo hivyo vya afya, Serikali iko tayari kuleta fedha ili vikamilike mara moja kutokana na uhitaji mkubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge amewasilisha hoja hizi za Vituo vya Afya vya Mtwango na Mgololo. Niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwa kuanza kujitolea nguvu zao. Nawahakikishia kwamba Serikali imeshaweka kwenye mpango wa kupeleka fedha ili kukamilisha vituo hivi vianze kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge, jiandae Ndulane.

**MHE ALLY M. KASINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Nanjilinji ambayo ina umbali wa zaidi ya kilomita 100 kutoka sehemu ya kutolea huduma ya afya kwa maana ya Hospitali ya Wilaya pale Kinyonga haina gari la wagonjwa.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Nanjirinji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kupeleka gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Nanjirinji na nimhakikishie kwamba kwenye magari ambayo tayari yameanza

kununuliwa, tayari magari 117 yameingia kati ya 316 na kituo hiki kitapewa kipaumbele kupewa gari la wagonjwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, jiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kilwa ina majimbo mawili; je, Serikali ina mpango gani wa kuleta *ambulance* zaidi ya moja ili kukidhi uhitaji katika Wilaya yetu ya Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapeleka magari ya wagonjwa kwenye kila halmashauri, lakini ndani ya halmashauri kuna vipaumbele vya maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa zaidi wa magari ya wagonjwa. Kwa hiyo, tunapeleka magari mawili katika Halmashauri ya Kilwa, lakini pia kukiwa na uhitaji na vigezo vya kutosha, basi tutaona namna ya kuepeleka gari nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Jimbo la Buchosa lina idadi ya watu wasiopungua 400,000 na vituo vya afya vinane, lakini lina gari la wagonjwa moja na watu wengi wanaishi visiwani. Je, Serikali iko tayari sasa kutamka kwamba

Jimbo la Buchosa litapata magari ya wagonjwa katika miongoni mwa magari haya ya wagonjwa yanayotolewa na moja lipelekwe visiwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba katika magari 316 ya wagonjwa, Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa pia itapelekewa magari mawili ya wagonjwa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Na. 149

**Mpango wa kukarabati miundombinu ya Hospitali ya Arumeru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Arumeru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali Kongwe Nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali 19. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2023, kiasi cha shilingi bilioni 12.95 zimekwishatolewa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya hospitali kongwe kumi na nne 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali itatenga shilingi bilioni 27.9 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe 31 ikiwepo Hospitali ya Halmashauri ya Meru ambayo imetengewa shilingi milioni 900. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; hospitali hii ni ya siku nyingi sana na majengo yake yamechakaa sana kiasi kwamba mengine yatalazimika kuvunjwa na kujengwa upya, lakini pia kuna changamoto ya eneo. Kwa Hiyo tunaona kwamba ni busara kuanza sasa kuwaza kwenda kujenga majengo ya ghorofa.

Je, Serikali pamoja na kwamba imetupatia shilingi milioni 900 ambazo tunashukuru sana, je, Serikali haioni kuwa ni muhimu kujipanga kwa ajili ya kujenga maghorofa kwa maana ya kwamba fedha ziongezwe? Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hospitali hii haina *mortuary* siku zote tangu imejengwa. Tumejitahidi tumejenga

*mortuary* pale na mpaka sasa haijapata majokofu. Je, ni lini Serikali itatupatia majokofu ili ile *mortuary* ianze kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hospitali hii ni kongwe, ni ya siku nyingi na mwezi mmoja uliopita nilifanya ziara pale nikishirikiana na Mheshimiwa Mbunge, lakini tulikubaliana kwamba kwa sababu imekwishaingizwa kwenye Mpango wa Hospitali Kongwe 31 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi ndio maana mwaka wa fedha 2023/2024 imetengewa Milioni 900. Sasa dhamira ya kujenga hospitali mpya ndani ya halmashauri wanaweza wakakaa na kuleta mapendekezo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili na sisi tuweze kuyatathimini na kuona kama yanaweza kutekelezeka ama vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwapongeze kwa kujenga jengo la kuhifadhia miili ya marehemu *(mortuary)* lakini jokofu liko ndani ya uwezo wa halmashauri kupitia Bohari ya Dawa *(MSD)*. Kwa hiyo, nielekeze Mkurugenzi wa Halmashauri hii kuhakikisha kwamba wanaomba jokofu Kupitia akaunti ya *MSD* ili waweze kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali iliahidi kwamba imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga ambayo miundombinu yake imechakaa sana na ni hospitali ya siku

nyingi. Je, ni lini ukarabati huo utaanza ili wananchi wa Wilaya ya Mbinga wapate huduma za afya bora na stahiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Serikali ya 2023/2024 iliyopitishwa hapa Bungeni wiki iliyopita, Serikali imetenga Shilingi Milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali Kongwe ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, ni lini sasa Serikali itajenga *mortuary* katika Kituo cha Malawi kilichopo Yombo Vituka Jimboni Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatvyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwezo wa mapato ya ndani ya Manispaa ya Temeke, naelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuweka kipaumbele cha kujenga jengo la kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya cha Yombo Vituka, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina.

**MHE: YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kituo cha Afya cha Eshkesh kilipewa Shilingi Milioni 400 na imekamilisha jengo la *OPD* na nyumba ya Daktari, lakini bado jengo la Mama na Mtoto na kituo hicho hakijaanza kufanya kazi. Je, sasa ni lini Serikali itakamilisha jengo la Mama na Mtoto ili kituo hicho kianze kufanya kazi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Eshkesh kilipata shilingi milioni 400 na hatua za ujenzi zimefikia umaliziaji wa baadhi ya majengo na ni kweli kwamba jengo la Mama na Mtoto halijakamilika. Nimhakikishie tu kwamba Serikali iliweka mpango wa ujenzi wa vituo vya afya hivi kwa awamu. Tumekwenda awamu ya kwanza tumekamilisha majengo hayo, tunakwenda awamu ya pili kutafuta fedha kwa ajili kukamilisha pia jengo la Mama na Mtoto ili ianze kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dkt. Mathayo.

Na. 150

**Kutatua kero za Muungano**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, ni kero zipi za Muungano zimetatuliwa na zipi zimebaki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali za pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimejadili na kuzipatia ufumbuzi jumla ya changamoto 22. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

(i) Gharama za Kushusha Mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibari;

(ii) Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na

(iii) Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, changamoto zote zilizopatiwa ufumbuzi zimefafanuliwa kwa kina na zinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizobakia kutatuliwa ni nne ambazo ni:-

(i) Mapendekezo ya Tume ya pamoja ya Fedha;

(ii) Usajili wa Vyombo vya Moto;

(iii) Uingizaji wa Sukari katika Soko la Tanzania Bara; na

(iv) Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zitakazokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kero za Muungano zimechukua muda mrefu sana na sasa hivi tuko Awamu ya Sita lakini bado kuna kero na zingine mpya zinajitokeza. Ningependa kuuliza ni mambo gani ambayo yanakwamisha kukamilika kwa kero zote za Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Sheria Mama ni Katiba na katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi vimeorodheshwa kama masuala ya Muungano na jibu la Serikali linaonesha kwamba changamoto hii imemalizika. Je, suala hili kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano limefutwa kwa sheria gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri au arudie tena swali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili.

**NAIBU SPIKA:** Rudia tena swali lako.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID**: Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili linasema kwamba, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi ni suala ambalo limewezeshwa katika mambo ya Jamhuri ya Muungano kwenye Katiba ya mwaka 1977. Sasa katika jibu lake amesema kwamba changamoto hii imekwishatatuliwa.

Nataka kujua imetatuliwa vipi ama kwa sheria gani imetatua suala hili la mafuta kwamba sio la Jamhuri ya Muungano tena?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mbunge na Watanzania kwa ujumla kwamba suala la utatuzi wa changamoto za Muungano halijakwama wala halijasuasua, ni suala ambalo linakwenda kwa sababu mpaka hivi tunavyozungumza asilimia ya changamoto zilizotatuliwa ni nyingi tofauti na zilivyokuwa. Vile vile, katika orodha ya mambo yaliyotatuliwa yapo mengi, tulikuwa tuna changamoto nyingi, lakini sasa hivi kama atarejea kwenye jibu langu la msingi jumla ya changamoto 22 zimekwishatatuliwa. Zilizobakia ni changamoto ambazo Kamati zinazohusika ziko mbioni na zinakaa kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hizi na Muungano huu uendelee kudumu kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili, ni kweli kwamba suala la utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia lilikuwa ni changamoto, ilifika wakati lilikuwa lina mvutano

kidogo, lakini kwa sababu ya busara ya viongozi wetu wanaosimamia Muungano huu na Kamati zilizoundwa zikiwemo Kamati za Makatibu Wakuu, Kamati za Wataalam na Kamati zile za Mawaziri, zimefikia mahali pazuri katika kulitatua jambo hili, tena limetatuliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zote na sasa hivi tayari Zanzibar iko vizuri na Muungano unakwenda vizuri katika suala hili la mafuta na gesi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kamonga.

Na. 151

**Miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba – Ziwa Nyasa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha Ludewa kwa ajili ya Miradi ya Ufugaji Samaki kwenye vizimba ndani ya Ziwa Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa samaki kwa vizimba ziwani unafanyika katika maeneo yaliyokidhi vigezo vya kisheria na kitaalam. Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* hufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira

(*Strategic Environmental Assessment*) ili kuhakikisha maeneo husika yanakidhi vigezo kabla ya kuanza uwekezaji. Tathmini hii imepangwa kufanyika kwa awamu katika Maziwa yetu yote na kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023 ilianza katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali imepanga kuendelea kufanya tathmini katika Ziwa Nyasa ikiwemo Ludewa ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki katika vizimba. Pia, Serikali itawezesha *TAFIRI* kufanya majaribio ya ufugaji samaki kwa kushirikiana na wananchi utakaojumuisha uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina ya magege (*Oreochromis karongae*) na ufugaji wake kwa vizimba. Hatua hii inalenga kuwajengea uwezo wananchi wa ufugaji wa samaki pindi tathmini itakapokamilika. Vile vile, hatua hii itawawazesha wananchi wa Ludewa na Ziwa Nyasa kwa ujumla kunufaika na fursa za mikopo zilizopo kwa ajili ya kuwezesha ufugaji samaki kwa vizimba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na pia atupelekee shukrani nyingi Serikalini kwa kutuletea milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Samaki pale Manda. Pamoja na Shukrani hizo naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kule Ludewa wananchi wana ng'ombe kama 33,871 wa kienyeji na 687 wa kisasa ambao sio bora sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea madume bora kwa ajili ya kuboresha uzao wa ng'ombe kule Ludewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha, Sheria Sera na Kanuni ili ziweze kusimamia Sekta ya Uvuvi ipasavyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili nyongeza ya Mheshimiwa Kamonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunapokea shukrani na pili *Program* ya Uboreshaji wa Mifugo inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni *program* endelevu inayotumia njia ya madume bora na njia ya uhimilishaji. Yeye ameomba madume bora na katika mwaka huu wa fedha tunaoelekea 2023/2024, mkakati huu utaendelea na Ludewa tutaiweka kwenye eneo mojawapo la kunufaika na program hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya Sera, Sheria na Kanuni zetu tumekuwa tukifanya hivi na kila mara panapotokea hitaji, tutaendelea kuboresha Sheria na Kanuni zetu. Kwa hiyo kama Mheshimiwa Mbunge analo jambo mahususi tunamkaribisha kwa ajili ya kufanya maboresho hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Serikali imewahi kwenda kutoa elimu ya ufugaji wa vizimba vya samaki kwa wananchi wanaozunguka Ziwa Basutu. Je, kwa kuwa imekwishakuwa ni muda mrefu ni lini Serikali itapeleka fedha ili wananchi hao waweze kunufaika na mafunzo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari wananchi wa Basutu wamekwishapata elimu naomba nimuahidi kuwa Serikali inalichukua jambo hili na kwenyewe tutakwenda kufanya tathimini ya kimazingira ili waweze kunufaika na *program* hii na kujiongezea kipato na kutengeneza ajira. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kuna nguvu kubwa sana imepelekwa katika ukanda wa Maziwa katika suala zima la ufugaji wa samaki kwa vizimba. Je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba na Ukanda wa Pwani ikiwa ni pamoja na Kigamboni zinanufaika na uvuvi wa samaki kwa njia ya vizimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa 2022/2023 upande wa Mikoa ya Pwani kwenye programu hii ya ufugaji wa samaki tulipeleka pesa zaidi upande wa ukulima wa mwani Takribani Bilioni 2.1zimenufaisha wakulima wa mwani kutoka Tanga kule Moha mpaka Mtwara kule Msimbati, sasa katika mwaka wa 2023/2024 kupitia programu maalum ya

*blue economy* tunatarajia kupeleka tena nguvu kwa maana ya uwezeshaji, kwa lengo la mwani vilevile unenepeshaji wa Kaa na ufugaji wa Majongoo Bahari. Kwa hivyo, wakulima na wavuvi wa ukanda wa Pwani wakiwemo wa Kigamboni na wenyewe makundi ya vijana na akina mama yatapata kunufaika na programu hii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Madini Mheshimiwa Matiko.

Na. 152

**Fidia kwa wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele watalipwa fidia kutokana na madhila waliyoyapata kutoka Mgodi wa Barrick?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa *Barrick North* Mara kwa sasa hauhitaji eneo la Kitongoji cha Nyamichele kama wananchi walivyokuwa wametarajia hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mgodi wa *North* Mara kutohitaji eneo hilo, kuna utaratibu ambao unaandaliwa na mgodi huo wa kutoa kifuta jasho kwa wananchi waliopata madhila kutoka kwa mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na nasikitishwa kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa *North* Mara walifanya tathmini pamoja na kubomoa nyumba na mazao ya wananchi mwaka 2013, ambapo walifanya tathmini kwa *phase* sita, baadae baada ya miaka kadhaa wakaja wakasema wanahitaji *phase* nne tu ambazo wamelipa zikabaki *phase* mbili zenye wananchi 1,586 na wakasema kama walivyosema kwamba wangelipa kifuta jasho ambapo mpaka sasa hivi wananchi hawa hawajaweza kulipwa kifuta jasho takribani miaka kumi, ningependa kujua ni lini Serikali itahakikisha inasimamia sheria zile za madini na za ardhi kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanalipwa fidia yao stahiki ya kubomolewa nyumba, mazao na muda uliopotea kutofanya shughuli za maendeleo kwa muda wa miaka kumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, mwaka 2018 baada ya wananchi hao kuona kwamba inachukua muda hawalipwi hicho kifuta jasho kinachosemwa waliifungua kesi Mahakama Kuu, ambapo Waziri wa Madini Mheshimiwa Biteko alienda kule Nyamongo akawasihi wananchi waondoe hii kesi mahakamani mwaka 2018 lakini mpaka sasa hivi wananchi hao bado hawajaweza kulipwa. Mwaka huu mapema walifuatilia kwa Mthamini Mkuu wa Serikali na akakiri kwamba hajapokea *document* yoyote ile au taarifa yoyote ile ya kutoka mgodini kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua ni kwa nini pale ambapo mgodi au ardhi ya wananchi inatwaliwa Serikali

inashindwa kufuata sheria zilizopo kuhakikisha kwamba wananchi wanalipwa stahiki zao mara moja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatanyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali lake la kwanza kwamba ni lini hawa wananchi wanaokaa katika *Phase* Mbili zilizobaki ambazo hazijafidiwa watalipwa. Napende tu kumhakikishia kwamba baada ya kampeni kumwajiri Mkandarasi aliyefanya tathmini kufahamu watu wanostahili kulipwa na kufahamu kiwango ambacho kinastahili kutolewa kama kifutajasho kwa sasa hivi ndani ya miezi miwili ijayo utaratibu wa malipo hayo utaenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali lake la pili, kwamba ni kwa nini Serikali isisimamie sheria yake na kuhakikisha kwamba wananchi ambao waliondoa kesi Mahakamani mwaka 2018 wanalipwa, napenda tu kumhakikishia kwamba Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ni Serikali inayopenda kutenda haki, nasi kama Wizara kwa niaba yake tunasimama kidete kuhakikisha kwamba wananchi hawa baada ya hizi tathmini kuwa zimeshafanyika na sasa tumeshafikia mwisho wake na wanakwenda kupata malipo yao, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuongezea katika majibu mazuri ambayo ameyatoa Naibu Waziri wa Madini. Nilitaka kuzungumzia suala la fidia kwa nini

fidia zinachelewa kulipwa na kwa nini pengine hali inatokea namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la fidia ucheleweshaji wa fidia wakati mwingine unatokana na udanganyifu unaokuwepo kwenye maeneo husika. Kwa mfano, katika masuala mazima ya kuwa na tuna lugha rahisi inaitwa tegesha, unakuta mazao yanaota kwa haraka kwa siku mbili mazao yapo ambayo yanakuwa ni pandikizi kwa hiyo katika suala zima la kufanya uthamini kadri unavyokwenda unakuta kuna mabadiliko kwenye lile eneo, lakini wanasahau kwamba Serikali huwa inachukua picha za anga kabla ya kufanya zoezi na inaangalia picha za nyuma na kuweza kujua kabla ya uthamini kuanza kulikuwa na nini pale na unapoanza uthamini unakuta kuna mali nyingi zinaongezeka, upandaji wa mazao ambayo mengine yanapandwa usiku na mchana. Kwa hiyo, wakati mwingine niwaombe tu wananchi ya kwamba Serikali ina nia na dhamira njema ya kuweza kulipa fidia, kwa hiyo tuache ule udanganyifu ambao unachelewesha haki za Watanzania katika kulipwa fidia zao.

**NAIBU SPIKA:** ahsante Mheshimiwa Agnes Marwa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhalisia huohuo kwamba Serikali ilikwishafanya uthamini na ikaelewa kwamba ni watu wangapi wanahaki ya kulipwa maeneo yao katika maeneo yambayo wamechukua Wawekezaji.

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hili kutokana na kwamba wao Wawekezaji wameshapata faida ya kutosha na sasa mashimo ndiyo yatakayobaki na wananchi wamesubiri kwa muda mrefu na ni tatizo la muda mrefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kwamba tathmini zote zimeshafanyika na kiwango cha malipo kinachostahili kulipwa kimeshajulikana, mchakato unaoendelea kwa sasa ni huo wa kuhakikisha kwamba wanaostahili kulipwa, kiwango wananchostahili kulipwa na maelewano ya wao kukubali malipo hayo ndiyo yanayoendelea na Wizara tutaendelea kusimamia hilo liweze kutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, kwa niaba yake Mheshimiwa Ndugulile kwa niaba ya Turky, yupo, Mheshimiwa Massare?

Na. 153

**Kutoa elimu ya saratani nchini**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y MHE. TOUFIQ S. TURKY** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa Saratani nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitumia njia mbalimbali za kutoa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na ugonjwa wa saratani kupitia vipindi vya redio na televisheni, machapisho na magazeti, mitandao ya jamii kama *Facebook*, *Instagram* na pia televisheni sehemu za kusubiria wagonjwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kutoa elimu ya ugonjwa wa saratani kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa kampeni mbalimbali za uelimishaji wa jamii na uchunguzi wa awali wa saratani nchini ikiwemo huduma Mkoba.

(ii) Kuandaa mtaala wa mafunzo wa magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo saratani kwa watoa huduma wa ngazi za msingi ili kuwajengea uwezo wa kutoa elimu kwa jamii.

(iii) Kuandaa vipindi mbalimbali na machapisho ya utoaji wa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasisyo ya kuambukiza ikiwemo saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Je, sasa Serikali ni lini itasaidia hospitali za Mikoa nazo kutoa huduma hii ya saratani, kwa sababu sasa hivi inatolewa katika Hospitali za Kanda tu na hospitali kubwa kama ile *KCMC*, Bugando na *Ocean Road* tu?

Swali la pili, kwa kuwa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukizwa ukiwemo ugonjwa wa kisukari, *pressure* pamoja na magonjwa mengine; Je Serikali sasa ina mkakati gani wa kutoa elimu ya kutosha hasa Wilayani ambako wagonjwa hawa ndiyo wanakotokea ili kuondoa rufaa nyingi kwa ajili ya hospitali kubwa kama Muhimbili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ndiyo maana Serikali sasa hivi, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha na amehakikisha hospital zote za Mikoa zina *CT scan,* maana yake sasa kwenye hospitali zetu za Mikoa wanaweza kucheki na kugundua mapema saratani kabla haijakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mkakati mahsusi wa kuwasomesha Wataalam kwa ajili ya kuwapeleka ngazi za Mikoa na kuweza kutoa huduma hiyo. Kwa sasa tunapima lakini tunashirikiana kwa kutumia *telemedicine* ili kuwasiliana na hospitali zetu za Kanda na Mikoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tumekuelewa ahsante kwa jibu zuri. Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, saratani ya kizazi pamoja na saratani ya matiti imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wanawake. Je, nini mkakati wa Serikali wa kufanya utafiti wa kina ili kujua chanzo cha saratani hii ili iweze kuzuiwa badala ya kutibu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ndiyo maana umesikia kuna kampeni zinazoendelea kule shuleni na kwingine kuhakikisha kwamba watoto wanapata chanjo hasa watoto wadogo na wasichana, vilevile tunahamasisha sana kupima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachukua ushauri wako na tutaendelea kufanya utafiti na kuona changamoto zinazosababisha mambo haya yaongezeke kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwijage.

Na. 154

**Hitaji la meli ya abiria Muleba**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Meli ndogo ya abiria Muleba pamoja na kutumia meli ya MV Victoria kujaribu masoko ya nchi za Uganda na Kenya ?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa ujenzi na uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua hitaji kubwa la usafiri wa wananchi Wilayani Muleba hususani waishio katika Visiwa. Kwa kutambua hitaji hilo, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imetenga meli moja iitwayo MV Clarias kutoa huduma katika Visiwa vya Godziba Wilayani Muleba na Visiwa vya Gana Wilayani Ukerewe. Meli hiyo iliyokuwa imeanza kutoa huduma katika visiwa hivyo tarehe 3 Machi, 2023 ilisimama tarehe 22 Machi, 2023 baada ya kupata hitilafu za kiufundi. Huduma hizo zitaendelea kuanza tena mwanzoni mwa mwezi Mei, 2023 baada ya matengenezo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za safari za kwenda Uganda na Kenya, *MSCL* inatarajia kuanza safari hizo kwa kutumia meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu mara baada ya ujenzi wake kukamilika. Meli ya MV Victoria haitaweza kutumika kwani ndiyo meli pekee inayotegemewa katika utoaji wa huduma za usafiri kati ya Mwanza na Bukoba kupitia Kemondo na ni msaada mkubwa kwa wakazi wa ukanda huo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE :** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, gati la kuegesha meli katika Kisiwa cha Godzba baada ya maji kushuka ya Ziwa Victoria, kuegesha meli za *Songoro Marine* na hiyo Clarias imekuwa ni shida. Serikali mnaonaje haraka mtujengee gati lile liweze kuhimili kupokea meli zetu maji yanapopanda na kupwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza; visiwa vya Ikuza bandari ya Magarini, Mazinga, Bumbile Kerebe havijahusishwa kwenye mpango wa Serikali ulioutaja. Je, ni lini

Serikali itaangalia gati za visiwa hivyo na kuweza kuzitekeleza kusudi Muleba nzima iweze kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika gati hili la Godzba kuna changamoto ya maji kushuka na hivyo kusababisha gati hilo kutotumika ipasavyo na meli hizi. Kwa maana hiyo, Serikali inatoa maelekezo kwanza kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari nchini kutuma timu ya wataalam ili kulirekebisha gati hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa hatua za awali kwa kuwa wenzetu wa *MSCL* wana-*floating dock* tatu (tishari), nataka moja ije eneo hili la Godzba ili lianze kufanyakazi wakati meli hii inafanya kazi eneo hili na tishari nyingine itaenda katika kisiwa cha Gana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anataka kujua ni lini tutapeleka huduma katika visiwa vya Kerebe Bumbile, Kyamkwikwi, Godzba na maeneo mengine. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa meli hii ya MV Clarias tayari tumeshakamilisha matengenezo yake jana na tunategemea ndani ya wiki hii, namuelekeza mkurugenzi wa *TASAC* atume timu yake ya wataalamu ili wakajiridhishe na hatimaye meli hii ianze kufanya kazi. Kwa maeneo ya visiwa ambavyo umevitamka Mheshimiwa Mbunge nako tutaanza kupeleka huduma kama ambayo inafanya sasa maeneo mengine. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ukianzia Kigoma mpaka Kalambo tulikuwa tukitegemea meli ya *MV* Liemba pamoja na MV Mwongozo, ni muda mrefu sana hatuna usafiri wa meli.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuhakikisha kwamba inapatikana meli kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Ziwa Tanganyika tuna changamoto za meli, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuelekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya Uchukuzi kwamba mwaka huu wa fedha tunakwenda kusaini mikataba minne ya ujenzi wa meli tatu pamoja na chelezo kubwa katika Ziwa hili la Tanganyika kwa maana ya meli tatu, meli mbili zitakuwa Ziwa Tanganyika na chelezo na meli moja itakuwa Ziwa Victoria. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa ukanda wa Kigoma kwamba kwa meli hii ya MV Liemba ambayo tayari tupo hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi pia itakarabatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mamabo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa niaba yake Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Na. 156

**Kumalizia changamoto zinazokabili Kituo cha Polisi Mlandizi**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, nini mkakati gani wa kumaliza changamoto za ukosefu wa nyumba za askari, magari na ufinyu wa ofisi katika Kituo cha Polisi Mlandizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Aaah! Samahani endelea kuna swali moja tumeliruka hapo, endelea tu na jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Mlandizi kilichopo Mkoa wa Pwani, kina gari moja *PT 4336 Ashok Leyland* ambalo linafanya kazi. Kituo hicho kinatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba mbili za kuishi familia Sita za Askari. Ujenzi wa nyumba hizo ambao umegharimu Shilingi Milioni 106.92 umechangiwa na nguvu za wananchi na wadau. Jengo moja lipo kwenye hatua ya kumalizia na lingine liko kwenye hatua ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumalizia ujenzi wa nyumba zote mbili kiasi cha shilingi milioni 147.054 kinahitajika. Kuhusu mahitaji ya ofisi, tathmini kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Upelelezi, uchunguzi wa kisayansi na intelijensia ya jinai

umefanyika na kubaini kuwa kiasi cha fedha shilingi 82,000,000 kinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa nyumba za nyumba za askari, pamoja na ofisi zitaombwa kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mwakamo Mwakamo Michael

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa gari analolizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni gari aina ya lori na kituo kile kina shughuli nyingi za kipolisi kwa sababu eneo la Mji wa Mlandizi limejengeka. Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuwapelekea gari dogo litakaloendana sawa na kasi ya kukabiliana na uhalifu katika Mji ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili jengo la Kituo cha Polisi Mlandizi linatumika kwa ajili ya *OCS* pamoja na *OCD,* sasa kwa kuwa jengo hili ni dogo hawaoni sasa ni muda muafaka wa kutafuta eneo lingine kuzitofautisha ofisi hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakambo Michael, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, tunatambua kwamba lori kwa kweli lina changamoto kwenye ufuatiliaji wa doria hasa

kwenye vichochoro na njia kama hizo, lakini kwa shughuli nyingi za kiuchumi zinazoendelea pale Mlandizi wanayo kweli haki ya kupata gari ndogo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwakambo pamoja na Wabunge wote kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi, karibuni itapata magari kwa ajili ya kuwezesha ofisi zote za ma *OCD* kupata gari ndogo kuwezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jengo hili, tumeeleza ofisi zitakazoongezeka kama kwenye jibu langu la msingi tulivyosema lakini kutokana na hoja kwamba eneo ni dogo, namwomba Mkurugenzi, kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, kutafuta eneo, na pale litakapokuwa limepatikana, sisi *always* tutakuwa tayari kushirikiana na Halmashauri hiyo kuimarisha majengo yanayotakiwa kwenye kituo kile, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunarudi swali namba155 la Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga.

Na. 155

**Ujenzi wa barabara ya Mabokweni – Maramba – Daluni – Bombomtoni – Magoma - Korogwe**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mabokweni – Maramba – Daluni – Bombomtoni – Magoma – Korogwe utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania imeanza na inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Mabokweni – Bombomtoni – Mashewa – Magoma – Kwamndolwa hadi *Old* Korogwe urefu wa kilometa 127.69. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ilianza mwezi Agosti, 2022 na inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka za kiofisi tulizonazo kutoka Serikalini zilionesha kwamba katika barabara hii, usananifu na upembuzi yakinifu ungekamilika mwezi wa Sita lakini sasa tunaambiwa ni mwezi wa Tisa: Je, Waziri anaweza kuniambia mpaka sasa kazi iliyofanyika, imefanyika kwa kiwango cha asilimia ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kutokana na umuhimu wa barabara hii kiusalama na kiuchumi, Wizara ipo tayari kutenga fedha ili ujenzi uweze kufanyika kwenye *lots* ambazo kazi imeshakamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asilimia ambayo imefikiwa, naomba baada ya kikao hiki niweze kupata taarifa kamili kwa sasa tuko asilimia ngapi? Hata hivyo nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pengine kitu muhimu hapa ni lini tutakamilisha hii kazi ambayo kwenye jibu langu la msingi nimesema kazi hii ya usanifu itakamilika mwezi Septemba. Kwa maana ya takwimu, asilimu naomba nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kutoka hapa kupata taarifa kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba barabara hii ni muhimu sana kiusalama na kiuchumi na ndiyo maana tumeamua kuifanyia usanifu wa kina ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mwakamo.

Na. 157

**Kuwawekea mazingira mazuri wakulima wadogo – Mto Ruvu**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawekea mazingira mazuri Wakulima wadogo wa kilimo cha Umwagiliaji katika Mto Ruvu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kilimo kwa wakulima wadogo ndani ya Bonde la Mto Ruvu kwa kubaini maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa Skimu ya Kisere (Nyani), usanifu huu ukikamilika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji utaanza katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri eneo ambalo tayari limeshafanyiwa upembuzi yakinifu liko Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Morogoro Vijijini.

Je, Serikali haiko tayari sasa kuja kufanya upembuzi yakinifu kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini kwenye Kata za Ruvu, Dutumi, Kwala, Gwata, Kikongo ili tuweze kuona namna bora ya kuwahudumia wakulima wadogo katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tunaposema wakulima kwenye Bonde la Ruvu ni wakulima wadogo, ni wadogo kweli kwa sababu wanatumia umwagiliaji kwa kutimia mashine ndogo na keni za mkono; na kuna katazo la watu kufanya umwagiliaji kwa kutumia Mto Ruvu. Je, Serikali inatoa tamko gani kuwasaidia watu wa Jimbo la Kibaha Vijijini kuendelea na umwagiliaji wa kutumia keni kwa kuwa hawajawa na mabwawa ya kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Machi, 2023 tuliingia mikataba na washauri waelekezi kwa ajili ya kwenda kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde 22 hapa nchini Tanzania likiwemo Bonde la Mto Ruvu. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika skimu alizizozitaja zitaingia ndani ya mpango huo wa Serikali ambapo kazi inaanza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na katazo; kwa mujibu wa sheria inayoongoza matumizi ya maji na sheria za mabonde, imeweka utaratibu wa matumizi ya maji kupitia kibali maalum. Sisi kama Wizara tutakaa na wenzetu wa bonde kuweka utaratibu mzuri ili mwisho wa siku wakulima wetu wale wadogo walime kupitia taratibu zote za kisheria na kutunza mazingira pia. Kubwa zaidi ni kwamba tutaweka miundombinu mikubwa zaidi ili wananchi waachane na changamoto hiyo ya kubeba makopo kwenda kumwagilia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Fakharia Shomari.

Na. 158

**Vijana waliopata nafasi za ufadhili nje ya nchi**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, ni vijana wangapi wa Tanzania wamepata nafasi za masomo nje ya Nchi kwa mwaka 2015-2020 na wangapi wanatoka Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi za ufadhili wa masomo unaotolewa na mashirika au nchi rafiki zinazopitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, huratibiwa kwa ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano. Idara za elimu ya juu zina jukumu la kubaini sifa za waombaji na kupendekeza wanufaika wa ufadhili kwa kuzingatia vigezo bila kujali mwombaji anatoka upande upi wa Muungano. Aidha, zipo baadhi ya nafasi za ufadhili wa masomo ambazo huratibiwa moja kwa moja na nchi au shirika linalotoa ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2015 - 2020, Wizara ya Elimu, Sayani na Teknolojia kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar iliratibu ufadhili wa masomo katika nchi za Uingereza, Hangaria, China,

Morocco, Misri, Algeria, Urusi, Ujerumani, Msumbiji, Thailand, Mauritius, Iran na Indonesia. Watanzania walionufaika na ufadhili huo ni 873 ambapo kati yao wanaume ni 587 na wanawake 286.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; kwanza sina budi kuishukuru Serikali kwa jibu lake zuri lenye mafanikio kwa wananchi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inafanya juhudi kubwa kusomesha vijana wake ili kufaidika nao; je, baada ya kuhitimu masomo hayo, Serikali inafaidika kitu gani wakati vijana hao wanabakia vijiweni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa Serikali haina ajira kwa watu wote, na vijana hawa tayari wamesoma; je, Serikali inawatengenezea mazingira gani vijana hawa ili nao waweze kuishi maisha bora? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba, Serikali inapata manufaa makubwa sana kwa kupeleka vijana kusoma nje ya nchi, kwa sababu licha ya ujuzi na maarifa ambayo wanapata, lakini vijana hao pia wanapata uzoefu kutoka nchi nyingine; kutoka nchi ambayo wanafunzi wanasoma lakini pia na nchi ambazo zinakuwa zimepeleka wanafunzi katika chuo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kwamba Serikali haina ajira na je, inatengeneza mazingira yapi kwa vijana hawa wanaotoka nje ya nchi: Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kuwa inatoa ajira kupitia ajira zinazotangazwa na Sekretarieti ya Ajira na pia kupitia sekta binafsi ambayo inakua kwa kasi kubwa. Vile vile, Serikali imeendelea kutengeneza mazingira kwa kuwapa nafasi za kupata mafunzo ya uzoefu kazini wakati wakiwa wanasubiri kupata ajira.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Paresso.

Na. 159

**Kuunganisha Mfumo wa Utoaji Leseni katika Sekta ya Utalii**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha mifumo ya utoaji leseni katika Sekta ya Utalii ili kurahisisha upatikanaji wa leseni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshaunganisha mfumo wa utoaji wa leseni katika sekta ya utalii kupitia mfumo wa kieletroniki wa *MNRT – Portal.* Hatua hiyo imeongeza tija katika utoaji huduma ikiwemo kurahisisha mchakato wa utoaji

wa leseni za biashara za utalii na hivyo kupunguza gharama, muda na kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi na wawekezaji mbalimbali katika biashara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Je, ni lini mifumo ya malipo ya *TANAPA, TAWA,* Ngorongoro pamoja na ile ya Wizara itaunganishwa na kuwa mfumo mmoja wa malipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itaruhusu uhai wa leseni za *TALA* uwe kwa mwaka ambao leseni imekatwa tofauti na sasa hivi ambavyo leseni inakuwa ni kalenda ya mwaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo ya malipo katika taasisi zetu tayari imeshaanza kutumika. Baadhi ya taasisi kama Ngorongoro na *TANAPA* utekelezaji wake unaendelea, lakini baadi ya taasisi tayari tulishaunganisha. Kwenye upande wa leseni; sasa hivi leseni inatoka kwa mfumo mmoja tu ambapo imeunganishwa mifumo yote. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye suala la leseni wadau wote wanafaidika na mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili lingine la *TALA,* tumeshaanza kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali hususan wadau wa masuala ya utalii na

tunaangalia tupitie kanuni upya tuone kama zitaleta tija katika marekebisho ya utoaji wa leseni. Nawakumbusha tu wadau hawa kwamba Serikali ina *calenda year* ambapo ndiyo huwa inakusanya mapato yake na imejiwekea mipango yake. Kwa hiyo, kama tutaona kuna haja ya kurekebisha kanuni hizi, basi tutawashirikisha kwa kuchukua maoni yao, lakini kwa kuangalia pia Serikali katika ukusanyaji wa mapato, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika; wageni wanane ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kutoka Bunge la Uganda, wakiambatana na Maafisa kutoka Bunge hilo; Mheshimiwa Okiror Boasco, Kiongozi wa Ujumbe; Mheshimiwa Achaya Juliet Lodou, Mjumbe; Mheshimiwa Otimgwi Issac, Mjumbe; Mheshimiwa Opio Samuel Acuti, Mjumbe; Mheshimiwa Nambooze Teddy, Mjumbe; Ndugu Sitnach Cherotich, Afisa wa Bunge; Ndugu Agatha Akankunda, Katibu wa Ujumbe. Wameambatana na mwenyeji wao Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Thea Ntara. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni viongozi wa Wizara hiyo; Ndugu Mary Maganga, Katibu Mkuu; Dkt. Switbert Mkama, Naibu Katibu Mkuu Mazingira; Ndugu Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Muungano; Ndugu Ignas Chuwa, Mkurugenzi wa Sera na Mipango; Dkt. Andrew Komba, Mkurugenzi wa Mazingira; Ndugu Edwin Makamba, Katibu wa Makamu wa Rais; Ndugu Osman Haji, Katibu wa Makamu wa Rais Msaidizi, Zanzibar; Ndugu Emma Liwenga, Msaidizi wa Makamu wa Rais Mazingira; Ndugu Baraka Baraka, Msaidizi wa Makamu wa Rais

Muungano; Dkt. Eng. Samuel Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu – *NEMC*. Wameambatana na Watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambao ni familia yake; Ndugu Asha Shame Vuai, Mke wa Waziri Dkt. Jafo; Ndugu Asha Shame Kombo, mwanafamilia; Ndugu Haurati Amiri Jafo, mwanafamilia; Ndugu Amina Mndolwa, mwanafamilia; Ndugu Ismail Jafo, mtoto wa Mheshimiwa Jafo; Ndugu Displine Manoza, Katibu wa Mheshimiwa Mbunge; na wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Jafo ambao ni Mabolozi wa Mazingira. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunaye mgeni wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye ni ndugu yake kutoka Wilaya Mufindi, Ndugu Mahenda Leonard, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Simon Songe, kutoka Busega, Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Busega, Ndugu Kauli Idaso, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni wakili msomi kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe, Ndugu Jenipher Mishack Mpanda, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Zacharia Issaay, ambao ni Waheshimiwa Madiwani na Watumishi kutoka Halmashauri ya Mbulu Mjini, Mkoa wa Manyara, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni waimbaji wa Kwaya ya Mamajusi kutoka Jimboni kwake Arumeru Mashariki, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunaye mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoa wa Tabora, Ndugu Aloyce Mishiri, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 145 ambao ni Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha *SUA* cha Mkoa wa Morogoro. Wanafunzi 33 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba hotuba yangu iingie katika *Hansard* za Bunge kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili

taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa taifa na leo amenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Hakika katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika uongozi wake katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni heshima na faraja kubwa kwangu kufanya kazi chini yake na ahadi yangu kwake na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwamba kwa ujumla nitaendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa maendeleo ya taifa na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia masuala ya Muungano hususan ufumbuzi wa hoja za Muungano na hifadhi ya mazingira ikiwa pamoja uongozi wa vitendo unaoonyesha katika shughuli za upandaji wa miti na usafi wa mazingira. Uongozi wake thabiti umedhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri zinazotekelewa na Ofisi hii niliyopewa dhamana ya kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha ninampongeza kwa uongozi wake imara katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa ya kutekeleza majukumu yao na hakika nashukuru kwa ushirikiano wao walionipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mbunge), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. Hakika katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kusimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri unayofanya ya kumsaidia Spika katika kuliendesha Bunge letu hili Tukufu. Vile vile nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusaidia kuliongoza Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti wa

Kamati na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hizo. Ninawaahidi kwamba ushirikiano wangu katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar. Tuendelee kumwombea kwa Mungu ampumzishe kwa amani. Aidha ninampongeza Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuliongoza Jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga (Mbunge) pamoja na Naibu Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote wa kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Dkt. Moses Mpogole Kusiluka kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti hii. Kipekee, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis almaarufu Chiro (Mbunge), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo na maelezo hayo ya awali, sasa ninaomba kutoa taarifa ya

utekelezaji wa kazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na malengo ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, jumla ya shilingi 12,974,292,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya fungu 26. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,000,000,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 974,292,000.00 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fungu namba 31, kiasi cha shilingi 40,142,025,000.00 kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi 18,180,328,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 21,961,697,000.00 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, jumla ya shilingi 9,176,806,096.7 zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya fungu 26 sawa na asilimia 70.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,662,500,000.0 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na asilimia 72.2 na shilingi 514,306,096.7 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 52.9 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya shilingi 9,058,921,949.3 zilitumika sawa na asilimia 98.7 ya fedha zilizopokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, fungu 31 lilipokea jumla ya shilingi 13,072,365,731.05 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 71.9 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, shilingi 2,210,195,938.75 ni mishahara ya

Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi 3,532,999,727.84 ni Mishahara ya Watumishi wa *NEMC* na shilingi 7,729,170,064.46 ni Matumizi Mengineyo. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, shilingi 12,250,067,332.7 zilitumika sawa na asilimia 91.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi 17,493,042,990.17 zilipokelewa sawa na asilimia 80 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni shilingi 1,174,486,893.00 na fedha za nje ni shilingi 15,618,555,997.17 sawa na asilimia 85.1. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 11,014,914,034.16 zilitumika ambapo shilingi 1,874,486,893.00 ni fedha za ndani sawa na asilimia 100 na shilingi 9,140,427,141.16 ni fedha za nje sawa na asilimia 58.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi inatambua kuwa Muungano wetu ni Tunu ya Taifa letu na ndiyo utambulisho wetu duniani, hivyo ni jukumu letu sote kuulinda, kuudumisha na kuuenzi. Mwaka huu Muungano unatimiza miaka 59 tangu kuasisiwa kwake, hivyo ni dhahiri kuwa umeendelea kuwa imara na kuimarika na hakika ni jambo la kujivunia kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi iliratibu vikao vitatu vya Kamati ya pamoja ya SJMT na SMZ kwa lengo la kujadili Masuala ya Muungano. Vikao hivyo vilifanyika katika ngazi ya kamati ya pamoja ya SJMT na SMZ, Mawaziri wa SJMT na SMZ na Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo hoja nane zilijadiliwa ambapo hoja nne zilipatiwa ufumbuzi na

kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni pamoja na: Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; Kodi ya Mapato *(Pay-As-You Earn - PAYE)* na Kodi ya Zuio *(Withholding Tax);* Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume *(Terminal III);* na Ongezeko la gharama za Umeme kutoka Shirika la Umeme *(TANESCO)* kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nne zilizobaki za Muungano zinazoendelea kutafutiwa ufumbuzi ni mgawanyo wa mapato yaliyokuwa yatokanayo na hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu, mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, usajili wa vyombo vya moto na uingizaji wa sukari inayozlishwa Zanzibar katika Soko la Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa hoja za Muungano zilizopo na zinazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuulinda na kuudumisha Muungano wetu adhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi imeendelea kuratibu gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila mwaka ambapo hadi Machi, 2023 shilingi bilioni 51.7 ambazo ni fedha za misaada ya kibajeti kutoka nje zilipelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi Machi, 2023 jumla ya shilingi bilioni 1.4

zilipelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo. Miradi na programu hizo zimefanikiwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Miradi na programu zilizotekelezwa ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF III)* Mzunguko wa Pili; Miradi ya Elimu chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania; Mpango wa ufadhili na Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi kwa Vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kuwa tarehe 26 Aprili, 2022 Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango alizindua Kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo. Katika uzinduzi huo, Makamu wa Rais alielekeza kuhakikikisha kitabu hicho kinatumika mashuleni. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi imekamilisha taratibu zote za kupata ithibati ya kitabu hicho kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule za Sekondari hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje katika eneo la usimamizi endelevu wa mazingira. Uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea matumizi endelevu ya rasilimali ikiwemo misitu, bahari, maziwa, mito, ardhi-oevu, wanyamapori, ardhi, gesi asilia na madini ambazo zina mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi na kupunguza umasikini nchini. Ili kuboresha matumizi ya rasilimali hizo na kuongeza uzalishaji wa huduma

na sekta mbalimbali za kiuchumi zimetekeleza miradi yenye kuchangia upunguzaji wa uharibifu wa mazingira na kukuza uchumi wa nchi. Sekta hizo ni pamoja na Nishati, Uchukuzi, Kilimo na Umwagiliaji, Mifugo na Uvuvi, Maji na Maliasili na Utalii. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kupunguza uharibifu wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho Serikali imetekeleza miradi ya kitaifa inayochangia kupunguza uharibifu wa mazingira. Miradi hiyo ni pamoja na: miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa itakayotumia umeme badala ya dizeli na hivyo kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa; mradi wa uzalishaji umeme wa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere utakaochangia umeme kiasi cha megawati 2,115 kwenye gridi ya Taifa; mradi wa usafiri wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam; Mradi wa usambazaji wa nishati gesi majumbani na kuweka vituo vya ujazaji gesi kwenye magari katika Jiji la Dar es Salaam; na programu ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi husika Ofisi imefanya uchambuzi wa kuangalia namna Sera za kisekta zilivyoakisi matamko ya Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021. Lengo la uchambuzi huo ni kuhakikisha kuwa Sera za kisekta zinahusisha masuala ya Hifadhi ya Mazingira katika Mipango mikakati ya kisekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi inaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sura namba 191 ili kuakisi matakwa ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na masuala mengine ya usimamizi ya Mazingira. Mapitio haya yanahusisha wadau mbalimbali na yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha huu 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Mazingira, sura namba191 kwa kuandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia *GN* Na. 636 kwa Kiingereza na *GN* Na. 637 kwa Kiswahili; na Mwongozo wa Taifa wa Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022 kwa ajili ya kutoa maelekezo mahususi kuhusu biashara ya kaboni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi imeandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2022 mpaka 2032. Mpango huo unasababisha hatua za kimkakati zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto za mazingira kwa kuzingatia jiografia na mifumo ikolojia ya maeneo husika. Aidha, mpango kabambe unaweka misingi wa mpango wa kibajeti shirikishi ya wasimamizi wa mazingira katika ngazi zote za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhifadhi wa Bonde la Ruaha Mkuu, Ofisi imeshiriki katika utatuzi wa mgogoro wa ardhi katika Bonde la Mto Ruaha katika eneo la Ihefu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa bwawa la Mwalimu Nyerere. Utatuzi wa mgogoro huu ulihusisha Mawaziri kutoka Wizara nane za Kisekta, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Jumuiya za Wafugaji, Wawekezaji katika mashamba ya mpunga, wakulima wadogo wa mpunga na Wananchi wa Wilaya ya Mbarali na Chunya. Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi ili kuhifadhi mazingira ya Bonde hilo na ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi inaendelea na kuratibu na kutoa mwongozo wa usimamizi, utekelezaji wa Katazo la Mifuko ya Plastiki ikiwa ni pamoja na utekelezaji maelekezo

mahsusi yaliyotolewa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Agosti, 2022 kuhusu kuongeza kasi ya utekelezaji wa Marufuku ya Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji, Usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya Mifuko ya Plastiki hapa nchini ikiwa ni pamoja na vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tarehe 26 Agosti, 2022, nikiwa kama Waziri mwenye dhamana ya mazingira nilitoa taarifa kwa umma kuendelea kusisitiza marufuku ya matumizi ya vifungashio kutumika kama vibebeo hususan bidhaa za masokoni. Kadhalika, tarehe 6 Aprili, 2023 nilirejea tena Tamko la Serikali kuhusu utekelezaji wa Katazo la Matumizi ya Mifuko ya Plastiki na kuelekeza *NEMC* kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa kuendelea na Kampeni ya kuondosha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo natoa agizo na msisitizo tena kwa jamii yote kuacha kabisa kutumia vifungashio hivyo vya plastiki visivyoruhusiwa vinavyotumika kama vibebeo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu na kushiriki mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Tabianchi uliofanyika Novemba, 2022 mjini *Sharm El Sheikh*, Misri. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la mkutano huo pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kujadili namna ya kupunguza uzalishaji wa gesi joto Duniani pamoja na kuweka jitihada za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na uharibifu wa fukwe katika bahari, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi yenye lengo la kukabiliana na mmomonyoko wa fukwe

katika maeneo ya Mtwara Mikindani na Sipwese kule Pemba. Miradi hii inahusu ujenzi wa kuta za bahari katika maeneo hayo. Katika kutekeleza miradi hii kiasi cha shilingi 1.04 kimetumika kutekeleza kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti ikijumuisha kampeni ya Soma na Mti inayohusisha shule za msingi, sekondari na vyuo. Kampeni ya upandaji wa miti inatekelezwa nchini kwa kila halmashauri kwa kupanda miti milioni 1.5 kila halmashauri. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, idadi ya miti iliyopandwa ni miti milioni 185.6 na iliyostawi ni miti milioni 154.93 sawa na asilimia 83.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nizipongeze halmashauri 23 zilizofanya vizuri katika kipindi hicho. Halmashauri hizo ni halmashauri ya *Iringa DC, Kilolo DC, Mufindi DC, Bukoba DC, Muleba DC, Ngara DC, Korogwe DC, Kibondo DC, Butiama DC, Chunya DC, Rungwe DC, Mlimba DC, Njombe DC, Makambako TC, Njombe TC, Kibiti DC, Mbinga DC, Nyasa DC, Madaba DC, Tunduru DC, Ushetu DC, Kaliua DC* na *Lushoto DC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi zimefanya vizuri sana kati ya halmashauri 184 hapa nchini zilizovuka lengo kwa kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka. Hivyo, ninazihimiza halmashauri zote ambazo hazikufikia lengo kuchukua hatua za makusudi za kupanda miti ili kunusuru nchi na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira kwa ukataji wa misitu na ukataji miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani hufanyika kila tarehe 5 Juni kila mwaka. Kwa mwaka 2023 maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Kimataifa yatafanyika Abidjan, Ivory Coast na Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo ni "*Beat Plastic Pollution*" kwa Kiswahili ni

"Tokomeza uchafuzi wa Mazingira utokanao na Matumizi ya Mifuko ya Plastiki".

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Ofisi inaendelea na Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambapo kaulimbiu ya kitaifa ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni "Pinga Uchafuzi wa Mazingira Utokanao na Mifuko ya Plastiki". Aidha, maadhimisho ya mwaka huu yanaenda sambamba na Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2023 ambazo ujumbe wake mkuu ni Mabadiliko ya Tabianchi, Hifadhi ya Mazingira na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji chini ya kaulimbiu isemayo kwamba "Tunza mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa Ustawi wa Viumbe Hai na Uchumi wa Taifa Letu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Tanzania ilishiriki Mkutano wa kumi wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe 8 Desemba, 2022 Bujumbura, Burundi. Katika mkutano huo, Tanzania ilikabidhi Uenyekiti kwa Jamhuri ya Burundi na ilikubalika kwamba lugha ya Kiswahili iwe lugha mojawapo ya mawasiliano katika mikutano ya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hicho baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia unaotekelezwa katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini A -Unguja. Katika kutekeleza kazi za mradi, kiasi cha shilingi bilioni 3.8 kilitumika. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Uchimbaji wa visima virefu 12,

ujenzi wa malambo saba, ujenzi wa majosho sita, ujenzi wa viwanda vidogo viwili vya bidhaa za ngozi na kimoja cha kuchakata mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame nchini katika Wilaya za Magu, Nzega, Mkalama, Kondoa na Micheweni - Pemba. Katika kutekeleza shughuli za mradi kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kilitumika. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uandaaji na utoaji wa hati miliki 2,284 za kimila za ardhi, uchimbaji wa visima 22 na ujenzi wa maghala matatu kwa ajili ya kuhifadhi mazao hususani mpunga na ujenzi wa vituo vitatu vya kukusanya mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza La Taifa La Hifadhi na Usimamizi Wa Mazingira; katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 baadhi ya masuala yaliyotekelezwa ni kama yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu Baraza lilifanya jumla ya kaguzi 480 katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, viwanda, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, miundombinu ya upakiaji wa makaa ya mawe, upakuaji wa mafuta kutoka melini na Maeneo yanayotumika kuhifadhi taka hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kipindi hicho, Baraza limesajili jumla ya miradi 1,316 ambapo miradi 933 ni miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(TAM)* na miradi 383 imefanyiwa ukaguzi wa mazingira. Aidha, katika

kipindi hicho jumla ya miradi 691 imeidhinishwa na kupata vyeti vya Athari ya Tathmini ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Maombi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024. Katika upande wa muungano masuala yaliyowekwa kipaumbele ni kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano; pili kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii, kuratibu masuala yasiyo ya muungano, kutoa elimu kwa umma kuhusu mauala ya muungano kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho, majarida na mitandao ya kijamii. Sita kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; kuandaa machapisho na kushiriki katika maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na nane kuandaa mfumo wa taarifa wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira katika kipindi cha mwaka 2023/2024 katika kuhakikisha uhifadhi endelevu ya mazingira Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vifuatavyo: -

i. Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa Mazingira;

ii. Kuimarisha usimamizi wa biashara ya Kaboni nchini;

iii. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Fursa ya Biashara ya Kaboni;

iv. Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikijumuisha utoaji elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira; na

v. Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira na miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika wilaya mbalimbali hapa nchini. Kwa upande wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka 2023/2024 ofisi imepanga kuendelea kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 kwa kufanya kaguzi na ufuatiliaji katika migodi, viwanda na miradi inayotekelezwa nchini ili kulinda na kutunza mazingira;

ii. Kuratibu Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kusajili na kufanya mapitio ya miradi pamoja na kusajili wataalam elekezi wa mazingira. kufanya tafiti ya kubaini malighafi zinazoweza kuoza katika mazingira ambazo zitatumika kutengeneza mifuko mbadala;

iii. Kuendesha Kongamano la Sita la Sayansi Kuhusu Uhifadhi wa Maeneo Oevu;

iv. Kuratibu na kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

v. Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, dira na maelekezo aliyotupatia kuhusu majukumu yetu. Kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana. Vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake katika kutoa maelekezo ili kutimiza majukumu yetu. Kadhalika, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa burasa zake na weledi wake wa kusimamia shughuli za Bunge ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Khamis H. Khamis, Mbunge, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wasaidizi wangu katika utendaji kazi wa Ofisi. Kwa kuanza napenda kumshukuru Bi. Mary Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; akisaidiwa na Bw. Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; na Dkt. Switbert Mkama, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Hali kadhalika, ninawashukuru pia Prof. Mhandisi Esnath Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *NEMC*, Dkt. Mhandisi Samwel G. Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC*, Wakuu wa Idara na Vitengo na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na *NEMC* kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Ninawashukuru wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo mkubwa napenda kuishukuru sana familia yangu kwa ujumla kwa upendo, msaada na hamasa kubwa wakati nikitimiza majukumu yangu. Mafanikio tuliyopata mwaka huu yametokana na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Washirika wa Maendeleo tuliofanya nao kazi kwa karibu ni pamoja na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali ya Norway, Serikali ya Sweden, Serikali ya Uingereza, Mabalozi wa nchi mbalimbali, *UNDP, UNEP*, Mfuko wa Mazingira wa Dunia, Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola, *UNIDO, UNCDF, WWF, IFAD, GCF, FAO, GIZ,* asasi zisizo za kiserikali, sekta binafsi zikiwemo benki mbalimbali za hapa nchini na mabalozi wa mazingira, ambao kwa leo wamewakilishwa na mabalozi wa mazingira kutoka Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Bi. Oliva Nyiega kutoka Dodoma na Balozi Alex Chagi kutoka Morogoro. Kwa kweli mabalozi wetu wamefanya kazi kubwa sana tunawashukuru sana mabalozi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuimarisha Muungano wetu na kuhifadhi Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuomba fedha. Ili Ofisi iweze kufikia malengo tarajiwa kama nilivyobainisha kwenye hotuba yangu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 26, Makamu wa Rais, ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi

ya shilingi 14,731,640,000.00 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, shilingi 1,251,640,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 13,480,000,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya matumizi ya shilingi 39,370,444,000.00 kwa ajili ya Fungu 31. Kati ya kiasi hicho, shilingi 20,712,399,000.00 ni kwa ajili matumizi ya kawaida na shilingi 18,658,045,000.00 ni matumizi ya miradi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi 3,349,788,000.00 mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi 5,264,448,000.00 mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na shilingi 12,098,163,000.00 matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya miradi ya maendeleo yanajumuisha shilingi 3,602,000,000.00 fedha za ndani na shilingi 15,056,045,000.00 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote, na kwa kuwa nimeomba taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge, sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**

**UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekitiwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Mapitio ya

Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2022/23 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24 kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

***3. Mheshimiwa Spika***, kwa dhati naomba kutoapongezi kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Hakika, katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni heshima na faraja kwangu kufanya kazi chini yake na ahadi yangu kwake na kwa Watanzania wote kwa ujumla ni kuendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa maendeleo ya nchi yetu.

***4.*** **Mheshimiwa Spika**, aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia masuala ya Muungano hususan ufumbuzi wa hoja za Muungano na Hifadhi ya Mazingira ikiwa pamoja na uongozi wa vitendo anaouonesha katika shughuli za upandaji miti na usafi wa Mazingira. Uongozi wake thabiti

unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri zinazotekelezwa na Ofisi hii niliyopewa dhamana ya kuisimamia.

***5. Mheshimiwa Spika***, vilevile, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

***6. Mheshimiwa Spika***, nitumie pia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2023/24. Aidha, ninampongeza kwa uongozi wake imara katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira.

***7. Mheshimiwa Spika***, ninapenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson (Mb.)**, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu, hakika katika kipindi cha uongozi wako tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuisimamia Serikali. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa **Mussa Azzan Zungu (Mb.)**, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu. Kadhalika, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hizo. Ninawaahidi ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

***8. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuchukua fursa hii kutoa pole kufuatia kifo cha **Mhe. Mussa Hassan Mussa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar. Tunaendelea kumuombea kwa Mungu ampumzishe kwa amani. Aidha, ninampongeza **Mhe. Abdul Yussuf Maalim** kwa kuchaguliwa kuongoza Jimbo hilo.

***9. Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa **Dkt**. **Joseph Kizito Mhagama (Mb.)** na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mheshimiwa **Jackson Gedion Kiswaga (Mb.)** pamoja na Naibu Wenyeviti na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2023/24.

***10. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza **Dkt. Moses Mpogole Kusiluka** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti hii. Kipekee, namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Khamis H. Khamis (Mb.)**, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

***11. Mheshimiwa Spika,*** baada ya pongezi hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2022/23 na malengo ya mwaka 2023/24.

## B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

**Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2022/23**

***12. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Fungu 26**

***13. Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka 2022/23, jumla ya **Shilingi 12,974,292,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 974,292,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fungu 31**

***14. Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa Fungu 31, kiasi cha **Shilingi 40,142,025,000.00** kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 18,180,328,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 21,961,697,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha **Shilingi 3,297,558,270.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 4,362,627,730.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na **Shilingi 10,520,142,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha **Shilingi 3,602,000,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 18,359,697,000.00** fedha za nje**.**

**Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi,2023**

**Fungu 26**

***15. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **Shilingi 9,176,806,096.7** zilipokelewa kwa ajili ya kutekelezamajukumu ya **Fungu 26** sawa na asilimia **70.7** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

**8,662,500,000.0** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia **72.2** na **Shilingi 514,306,096.7** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **52.9** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi 9,058,921,949.3** zilitumika sawa na asilimia **98.7** ya fedha zilizopokelewa.

**Fungu 31**

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **Fungu 31** lilipokea jumla ya **Shilingi 13,072,365,731.05** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **71.9** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichopokelewa, Shilingi **2,210,195,938.75** ni mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 3,532,999,727.84** ni Mishahara ya Watumishi wa NEMC na **Shilingi 7,329,170,064.46** ni Matumizi Mengineyo. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **Shilingi 12,250,067,332.7** zilitumika sawa na asilimia **91**.

***17. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo jumla ya **Shilingi 17,493,042,890.17** zilipokelewa sawa na asilimia 80 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni **Shilingi 1,874,486,893.00** na fedha za nje ni **Shilingi 15,618,555,997.17** sawa na asilimia 85.1. Aidha, katika kipindi hicho, **Shilingi 11,014,914,034.16** zilitumika ambapo **Shilingi 1,874,486,893.00** ni fedha za ndani sawa na asilimia 100 na Shilingi **9,140,427,141.16** ni fedha za nje sawa na asilimia **58.5**.

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191; Ajenda ya

Maendeleo ya Afrika (2063), Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030); Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira (2022-2032); Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

## KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023

## MASUALA YA MUUNGANO

***19. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ni Tunu ya Taifa letu na ndio utambulisho wetu duniani, hivyo ni jukumu letu sote kuulinda, kuudumisha na kuuenzi. Mwaka huu Muungano unatimiza miaka 59 tangu kuasisiwa kwake, hivyo ni dhahiri kuwa umeendelea kuwa imara na hakika ni jambo la kujivunia.

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

***(i) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano***

***21. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi iliratibu vikao vitatu (3) vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kwa lengo la kujadili masuala ya Muungano. Vikao hivyo vilifanyika katika ngazi ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ; Mawaziri wa SJMT na SMZ; na Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ. Aidha, Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ilifanya kikao kwa ajili ya maandalizi ya kikao cha kamati ya pamoja cha kushughulikia masuala ya Muungano. Vikao hivyo viliratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

***22. Mheshimiwa Spika***, katika vikao hivyo hoja nane (8)

zilijadiliwa ambapo hoja nne (4) zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni pamoja na: Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi Mara mbili; Kodi ya Mapato (Pay-As-You Earn - PAYE) na Kodi ya Zuio (Withholding Tax); Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III); na Ongezeko la gharama za Umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO).

***23. Mheshimiwa Spika***, maelezo ya hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo: Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi Mara mbili. Hoja ilitokana na kuwepo kwa utofauti wa ukadiriaji wa viwango vya thamani za bidhaa na kodi ya forodha baina ya Tanzania Bara na Zanzibar inayosababisha wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa kodi ya ziada kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara. Hali hii iliibua malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kwamba wanatozwa kodi mara mbili.

***24. Mheshimiwa Spika***, ufumbuzi wa hoja hii ulipatikana baada ya kubainika kwamba, wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa Zanzibar kutoka nje ya nchi na kupeleka Tanzania Bara hulazimika kulipia tofauti ya kodi iliyoachwa kukusanywa Zanzibar kutokana na tofauti ya uthaminishaji wa bidhaa. Hivyo, suala hilo haliwafanyi wafanyabiashara kulipa Kodi mara mbili badala yake hulipa kodi inayostahili kulipwa kwa uthaminishaji uliofanyika Tanzania Bara. Kwa sasa suala hilo linaeleweka vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

***25. Mheshimiwa Spika***, Hoja nyingine ilikuwa ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutonufaika ipasavyo na *PAYE* ya wafanyakazi wa Taasisi za Muungano waliopo Zanzibar pamoja na kodi ya zuio (*Withholding Tax*) itokanayo na

kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya majadiliano, ufumbuzi wa hoja hii ulipatikana kama ifuatavyo: Hoja ya kodi ya zuio kwa makampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar, Wizara zinazohusika na masuala ya Fedha za SJMT na SMZ zilikubaliana kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (*Tax Administration Act*) Sura ya 438 na Sheria ya Kodi ya Mapato (*Income Tax Act)* Sura ya 332 kupitia Sheria ya Fedha Namba 5 ya Mwaka 2022 ili Kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar kuweza kulipa Kodi ya Zuio Zanzibar. Kuhusu Kodi ya Mapato yatokanayo na mishahara ya watumishi wa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar ufumbuzi uliopatikana ni kwamba kiasi cha shilingi bilioni 1.75 ambacho kimekuwa kikitolewa kwa SMZ kila mwezi kama malipo ya *PAYE* kiendelee kutolewa kwa SMZ.



*Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Jamhuri wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum wakionesha Hati ya Makubaliano ya kuondoa Hoja ya Wafanyabiashara kutozwa Kodi mara mbili iliyopatiwa ufumbuzi wakati wa Kikao cha Kamati ya Pamoja kilichoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano*

*wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 06 Desemba, 2022 jijini Dodoma.*

***26. Mheshimiwa Spika***, kuhusu mkataba wa Mkopo wa Fedha kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (*Terminal III*), hoja ilikuwa ni kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Exim ya China kutokana na Mkataba kuhusisha vipengele vya kuweka mali za Serikali kama dhamana ya mkopo. Ufumbuzi ulipatikana baada ya SJMT na Benki ya Exim ya China kukubaliana kuondoa sharti hilo na hivyo kuwezesha Mkataba wa Mkopo huo kusainiwa tarehe 03 Novemba, 2022.

***27. Mheshimiwa Spika***, kuhusu ongezeko la gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO, hoja ilikuwa ni kuongezeka kwa bei ya umeme kwa wateja wa TANESCO ikiwemo Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kulikotokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme. Ongezeko hilo liliibua malalamiko kwa watumiaji wa umeme kwa upande wa Zanzibar. Baada ya majadiliano, hoja hii ilipatiwa ufumbuzi ambapo mapendekezo ya ZECO kununua umeme kwa shilingi 130 kwa uniti yalikubaliwa.

***28. Mheshimiwa Spika***, hoja nne (4) zilizobaki za Muungano zinazoendelea kutafutiwa ufumbuzi ni: - Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu; Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha; Usajili wa Vyombo vya moto; na Uingizaji wa sukari inayozalishwa Zanzibar katika soko la Tanzania Bara.

***29. Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa

lengo la kuulinda na kuudumisha Muungano wetu adhimu.

## *(ii) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii*

**Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

***30. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila mwaka ambapo hadi kufikia Machi, 2023 Shilingi bilioni 51.7 ambazo ni fedha za misaada ya kibajeti kutoka nje zilipelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**a) Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Zanzibar**

***31. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi Machi, 2023 Shilingi bilioni 1.4 zilipelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo. Aidha, Hesabu za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Halmashauri na Manispaa zote za Zanzibar kwa mwaka 2021/22 ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**b) Miradi na programu za Maendeleo**

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Miradi na programu hizo zimefanikiwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii.

***33. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi hiki Miradi na programu zilizotekelezwa ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) Mzunguko wa Pili; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); Miradi ya Elimu chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania; Mpango wa ufadhili

wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi kwa Vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu.

***(iii) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya SJMT na SMZ***

***34. Mheshimiwa Spika,*** ushirikiano baina ya SJMT na SMZ katika masuala yasiyo ya Muungano umeendelea kuimarika. Ofisi imeendelea kuhimiza umuhimu wa Wizara/Idara na Taasisi zisizo za Muungano kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu, sera, sheria, utaalamu na wataalamu. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 vikao kumi na mbili (12) vya ushirikiano vimefanyika baina ya Wizara/Taasisi na Idara za SJMT na SMZ.

***(iv) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano***

***35. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho/vipeperushi, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na Mitandao ya Kijamii. Aidha, Ofisi ilishiriki katika Maonesho ya Siku ya Wakulima Kitaifa (Nane Nane) yaliyofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 10 Agosti, 2022 Jijini Mbeya. Katika maonesho hayo, Elimu ya Muungano ilitolewa kwa wananchi kwa njia ya maswali na majibu na machapisho mbalimbali ikiwemo: Kitabu cha "Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo", Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais; na Magazeti ya zamani yenye habari kuhusu Muungano.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizindua Kitabu cha Historia ya Muungano wakati wa Maadhimisho ya Miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyofanyika jijini Dodoma tarehe 26 Aprili, 2022.*

***36. Mheshimiwa Spika***, Utakumbuka kuwa tarehe 26 Aprili, 2022 Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango alizindua Kitabu cha 'Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo'. Katika uzinduzi huo, Makamu wa Rais alielekeza kuhakikikisha kitabu hicho kinatumika mashuleni. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi imekamilisha taratibu zote za kupata Ithibati ya kitabu hicho kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule za Sekondari nchini.

### *(v) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano*

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kuratibu masuala ya Muungano yanayosimamiwa na Wizara, Taasisi na Idara za Muungano kwa faida ya pande zote mbili za Muungano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kati

ya Taasisi 33 za Muungano, Taasisi 27 zina Ofisi Zanzibar na hivyo kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, mafanikio yaliyopatikana kupitia Taasisi za Muungano ni pamoja na:

i. Utambuzi na usajili wa wananchi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar uliofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);

ii. Kutoa ithibati ya Mitaala kwa Vyuo Vikuu vya Tanzania Bara - Zanzibar iliyofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania;

iii. Udahili wa wanafunzi wa Shahada ya kwanza katika Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania Bara na Zanzibar kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); na

iv. Mafunzo kwa vyuo na shule za sekondari kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar yaliyotolewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

**HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WAMAZINGIRA**

***38. Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea matumizi endelevu ya maliasili ikiwemo misitu, bahari, maziwa, mito, ardhi-oevu, wanyamapori, ardhi, gesi asilia na madini ambazo zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini nchini. Ili kuboresha matumizi ya rasilimali hizo na kuongeza uzalishaji na huduma, sekta mbalimbali za kiuchumi zimetekeleza miradi yenye kuchangia kupunguza uharibifu wa mazingira na kukuza uchumi wa nchi. Sekta hizo ni pamoja na Nishati, Uchukuzi, Kilimo na Umwagiliaji, Mifugo na Uvuvi, Maji na Maliasili na Utalii. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kupunguza uharibifu wa mazingira.

***39. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho Serikali imetekeleza miradi ya kitaifa inayochangia kupunguza uharibifu wa mazingira. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa itakayotumia umeme badala ya mafuta ya dizeli na hivyo kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa; mradi wa kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere utakaochangia umeme kiasi cha megawati 2,115 kwenye gridi ya taifa na hivyo kupunguza uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta mazito yanayoharibu mazingira; mradi wa usafiri wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam unaochangia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kwa kupunguza idadi ya magari yanayotumia mafuta ya dizeli na petroli; Mradi wa usambazaji wa nishati ya gesi majumbani na kuweka vituo vya kujazia gesi kwenye magari katika Jiji la Dar es Salaam; na programu ya nishati safi ya kupikia.

***40. Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine inayochangia kupunguza uharibifu wa mazingira ni pamoja na miradi ya upandaji miti inayoendelea katika Halmashauri zote nchini na miradi inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, miradi ya kilimo cha umwagiliaji inayotekelezwa nchini inatoa mchango mkubwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uzalishaji wa chakula. Maeneo mengine yanahusisha uvuvi endelevu katika maziwa na bahari; ufugaji wa kisasa na wa kibiashara; kilimo endelevu cha kibiashara; na biashara ya kaboni.

***41. Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na kazi kubwa inayoendelea kufanyika katika Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, bado nchi yetu imendelea kukabiliwa na changamoto za mazingira katika maeneo mbalimbali. Ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira, Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutunga Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo, Mikakati, kutekeleza Programu na Miradi ya

hifadhi ya Mazingira pamoja na kuridhia Mikataba ya mazingira ya Kikanda na Kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 Ofisi imetekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:

***(i)* Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021**

***42. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi husika Ofisi imefanya uchambuzi wa kuangalia namna Sera za kisekta zilivyoakisi matamko ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021. Lengo la uchambuzi huo ni kuhakikisha kuwa Sera za kisekta zinahuisha masuala ya Hifadhi ya Mazingira katika Mipango na Mkakati ya kisekta. Matokeo ya uchambuzi huo yameonesha kuwa Sera tatu (3) za kisekta zilizotungwa hivi karibuni zimeakisi Hifadhi ya Mazingira. Naomba nitoe rai kwa Wizara zinazofanya mapitio ya Sera zao zihakikishe zinaakisi masuala ya Hifadhi ya Mazingira.

***(ii)* Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

***43. Mheshimiwa Spika***, Ofisi inaendelea kufanya mapitio ya sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ili kuakisi matakwa ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na masuala mengine ya usimamizi ya Mazingira. Mapitio haya yanahusisha wadau mbalimbali na yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/24.

***(iii)* Kanuni na Miongozo ya Hifadhi ya Mazingira**

***44. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kuandaa na kufanya mapitio ya Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia GN 636 (Kiingereza) na GN 637 (Kiswahili); na Mwongozo wa Taifa wa Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022 kwa ajili ya kutoa maelekezo mahususi kuhusu biashara ya kaboni nchini. Vilevile, katika kipindi hicho,

Ofisi imefanya marekebisho ya Kanuni za Wataalamu wa Mazingira za Mwaka 2022 na kukamilisha maandalizi ya Kanuni na Mwongozo wa Dhamana ya Mazingira katika shughuli za uchimbaji Madini (Environmental Perfomance Bond).




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko hundi ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya vijiji nane (8) vinavyotekeleza mradi wa Biashara ya Kaboni vilivyopo katika Tarafa ya Mwese wakati wa halfa iliyofanyika tarehe 23 Julai, 2022 katika Kijiji cha Katuma Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.*

### *(iv)* Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira

***45. Mheshimiwa Spika***, Ofisi imeandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka

2022 hadi 2032. Mpango huu unabainisha hatua za kimkakati zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto za mazingira kwa kuzingatia jiografia na mifumo ikolojia ya maeneo husika. Katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango huu, shughuli zifuatazo zitatekelezwa katika ngazi mbalimbali. Shughuli hizo ni pamoja na: kukuza uelewa kwa jamii kuhusu hifadhi ya mazingira; kuimarisha na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira; kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi; Kuandaa na kutekeleza programu za kurejesha mifumo ikolojia iliyoharibiwa; kuandaa na kutekeleza mipango ya usimamizi na udhibiti wa taka; kuimarisha usimamizi na uzingatiaji wa sheria; kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala; kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora za uzalishaji viwandani na kuhamasisha kufanyika kwa tafiti za mazingira na matumizi ya matokeo ya tafiti hizo. Aidha, Mpango Kabambe unaweka msingi wa mipango na bajeti shirikishi ya usimamizi wa mazingira katika ngazi zote.

***46. Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji wa mpango huu ni jukumu la kila Sekta katika kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanaendelea kulindwa na kurejeshwa katika hali yake kwa maeneo yaliyoathirika. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwasihi wadau wote ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi za Serikali wanapoandaa Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya utekelezaji kuhakikisha wanazingatia Mpango Kabambe pamoja na kufanya Tathmini ya Mazingira Kimkakati kabla ya kuanza utekelezaji wa sera, mikakati na mipango hiyo. Aidha, miradi yote nchini ifanyiwe Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kulinda mazingira na kuongeza uzalishaji.



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Semina ya kutambulisha Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT), Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ), Wizara ya Fedha na Mipango na Washirika wa Maendeleo iliyofanyika tarehe 13 Oktoba, 2022 jijini Dar es Salaam.*

***(v)*** **Hifadhi ya Mazingira na Mifumo Ikolojia katika Vyanzo vya Maji**

***47. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhifadhi wa Bonde la Ruaha Mkuu, Ofisi imeshiriki katika utatuzi wa mgogoro wa ardhi katika Bonde la Mto Ruaha katika eneo la Ihefu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa bwawa la Mwalimu Nyerere. Utatuzi wa mgogoro huo ulihusisha Mawaziri kutoka Wizara nane (8) za Kisekta, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Jumuiya za Wafugaji, Wawekezaji katika mashamba ya mpunga, wakulima wadogo wa mpunga na Wananchi wa Wilaya za Mbarali na Chunya. Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi huo ili kuhifadhi mazingira ya Bonde hilo na ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt.Philip Isdor Mpango akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Kituo cha Wanahabari Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA) mara baada ya kufungua Kongamano la Wahariri na Wadau wa Uhifadhi Mazingira na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji lililofanyika Mkoani Iringa tarehe 19 Desemba, 2022.*

**(vi) Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira**

***48. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inaendelea na kuratibu na kutoa miongozo na kusimamia utekelezaji wa Katazo la Mifuko ya Plastiki ikiwa ni pamoja na kutekeleza maelekezo mahsusi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ya tarehe 22 Agosti, 2022 kuhusu kuongeza kasi ya utekelezaji wa Marufuku ya Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji, Usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya Mifuko ya Plastiki nchini ikiwa ni pamoja na vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango. Aidha, tarehe 26 Agosti, 2022, nikiwa kama Waziri mwenye dhamana ya mazingira nilitoa taarifa kwa umma kuendelea kusisitiza marufuku ya matumizi ya vifungashio kutumika kama vibebeo hususan kwa bidhaa za msokoni. Kadhalika, tarehe 6 Aprili, 2023 nilirejea tena Tamko la Serikali kuhusu utekelezaji wa Katazo la Matumizi ya Mifuko ya Plastiki na kuelekeza NEMC kwa kushirikiana na Sekretarieti za

Mikoa kuendesha Kampeni za kuondosha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

***49. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia Bunge lako tukufu kusisitiza na kuutahadharisha Umma kuwa ni makosa kisheria kubadili matumizi ya vifungashio kuwa mifuko ya kubebea bidhaa, na kwa mujibu wa sheria, adhabu stahiki zitatolewa kwa watakaokiuka sheria wakiwemo watengenezaji, waingizaji, wasambazaji na watumiaji wa vifungashio vya plastiki vilivyozalishwa ama kuingizwa nchini na kutumika kama vibebeo vya bidhaa. Hivyo, natoa agizo na msisitizo kwa jamii yote kuacha kabisa kutumia vifungashio hivi vya plastiki visivyoruhusiwa vinavyotumika kama vibebeo.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa kwenye ziara ya kutembelea na kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika kiwanda cha Iron and Steel Ltd kilichopo Mikocheni mkoani Dar es Salaam tarehe 22 Julai, 2022.*

***(vii)* Usimamizi wa Taka Hatarishi na matumizi ya taka kama rasilimali viwandani**

***50. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23,

Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021 na Kanuni za Udhibiti wa Taka za Kieletroniki za mwaka 2021. Katika kipindi hicho, Ofisi imetoa vibali 272 vya taka hatarishi, na vibali 12 vya taka za kielektroniki kwa makampuni 67 na watu binafsi 23. Aidha, katika kurahisisha utekelezaji na kuongeza wigo wa wadau wanaojihusisha na shughuli za urejelezaji wa taka hatarishi, Ofisi imetafsiri Kanuni hizo kwa lugha ya Kiswahili.

***(viii)*** **Kuratibu utekelezaji wa Mpango - Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu nchini**

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2022/23, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imehamasisha wafanyabiashara wa Zebaki kusajili kemikali hiyo. Lengo la hatua hii ni kubaini kiasi cha Zebaki kinachoingizwa nchini ili kuweza kuchukua hatua mahususi za kudhibiti uingizaji na matumizi ya Zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya kampuni tisa (9) zimesajiliwa na jumla ya tani 5.8 za Zebaki kimeingizwa nchini.



*Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis akikagua sehemu ya kuchenjulia dhahabu wakati alipofanya ziara ya kukagua shughuli za uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Kijiji cha Nayu wilayani Chamwino mkoani Dodoma tarehe 10 Agosti, 2022.*

### *(ix)* Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu na kushiriki mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Novemba, 2022 mjini Sharm El Sheikh, Misri. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo kuu la mkutano huo pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kujadili namna ya kupunguza uzalishaji wa gesi joto Duniani pamoja na kuweka jitihada za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

***53. Mheshimiwa Spika,*** mambo muhimu yaliyojitokeza katika mkutano huo ni pamoja na: Serikali kujadiliana na Benki ya Dunia ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya

kupunguza uzalishaji wa gesi joto; Majadiliano na Taasisi ya *2050 Pathway* yanayolenga kuandaa mkakati wa muda mrefu wa kupata fedha za kusaidia kupunguza uzalishaji wa gesi joto; Majadiliano ya kuimarisha mashirikiano kati ya Tanzania na Norway katika eneo la kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; na Majadiliano na wawakilishi wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi yaliyolenga kutatua changamoto zilizopo katika kuziwezesha Taasisi za Tanzania kupata ithibati ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ili kupata fedha zinazotolewa na mfuko huo. Aidha, hadi kufikia Machi, 2023 Serikali imeendelea kufanyia kazi maeneo yaliyobainishwa ikiwemo kufanya vikao vya majadiliano na Serikali ya Norway, Benki ya Dunia na Taasisi ya *2050 Pathway* katika kutekeleza makubaliano ya Mkutano huo.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye Mkutano wa 27 Umoja wa Mataifa wa nchi wanachama wa Mkataba wa mabadiliko ya Tabianchi (COP27) uliofanyika katika Mji wa Sharm El Sheikh nchini Misri tarehe 07 Novemba, 2022.*

**(x) Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za**

**mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha Bahari**

***54. Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na uharibifu wa fukwe katika bahari, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi yenye lengo la kukabiliana na mmomonyoko wa fukwe katika maeneo ya Mikindani (Mtwara) na Sipwese (Pemba). Miradi hii inahusu ujenzi wa kuta za bahari katika maeneo hayo. Katika kutekeleza miradi hii kiasi cha **Shilingi 1,040,579,966** kimetumika kutekeleza kazi zilizopangwa.

### *(xi)* Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi

***55. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ulio chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Katika kipindi hicho, Benki ya CRDB imekamilisha mchakato wa kupokea fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 500 ikiwa ni pamoja na kusaini mkataba wa usimamizi wa fedha hizo ambazo zitatumika kwa ajili ya utoaji mikopo na mafunzo kwa wanufaika tarajiwa. Vile vile, Ofisi inaendelea kuzisaidia taasisi nyingine katika kupata ithibati ya mfuko wa mabadiliko ya tabianchi. Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Benki ya NMB, NBC na TADB.

***56. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia ambapo katika awamu ya nane (8) ya utoaji fedha, Tanzania imetengewa kiasi cha dola za marekani milioni 33.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mazingira. Aidha, katika hatua za awali za kuwezesha upatikanaji wa fedha hizo, Ofisi iliratibu mkutano wa wadau wa masuala ya hifadhi ya mazingira mwezi Februari, 2023 Jijini Dodoma. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kukubaliana miradi ya kipaumbele kupitia Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira nchini. Mkutano huo ulihusisha wadau ambao ni Wizara na Taasisi za Serikali, Taasisi za Utafiti na Elimu, Azaki, Sekta binafsi pamoja na Washirika wa Maendeleo. Miradi ya

kipaumbele iliyopendekezwa ilihusu masuala ya: Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; Hifadhi ya bioanuai na vyanzo vya maji; Kukabiliana na changamoto za uharibifu wa ardhi; na Udhibiti wa taka. Maandiko dhana manne (4) ya miradi yamewasilishwa Sekretarieti ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa hatua za awali za mapitio.




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wawakilishi wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) na wadau wengine wakati wa Warsha ya siku mbili ya Wadau na Wataalamu wa Mazingira iliyolenga kuainisha vipaumbele vya miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi inayosimamiwa na GEF jijini Dodoma tarehe 13 hadi 15 Februari, 2023.*

***(xii)* Kampeni ya Upandaji Miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri kwa Mwaka**

***57. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti ikijumuisha kampeni ya Soma na Mti inayohusisha shule za msingi, sekondari na vyuo. Kampeni ya upandaji miti inatekelezwa nchini kwa kila Halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, idadi ya miti iliyopandwa ni 185,636,155

na iliyostawi ni 154,934,563 sawa na asilimia 83.5. Aidha, nizipongeze Halmashauri 23 (Iringa DC, Kilolo DC, Mufindi DC, Bukoba DC, Muleba DC, Ngara DC, Korogwe DC, Kibondo DC, Butiama DC, Chunya DC, Rungwe DC, Mlimba DC, Njombe DC, Makambako TC, Njombe TC, Kibiti DC, Mbinga DC, Nyasa DC, Madaba DC, Tunduru DC, Ushetu DC, Kaliua DC na Lushoto DC) kati ya 184 zilizovuka lengo la kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka. Hivyo, ninazihimiza Halmashauri zote ambazo hazikufikia lengo kuchukua hatua za makusudi za kupanda miti ili kunusuru nchi na athari zitokanazo na uharibifu wa misitu na ukataji miti.

***58. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa jamii yote ya Watanzania kwa lengo la kunusuru mazingira yasiharibike. Katika kutekeleza azma hiyo, nimetoa Katazo kwa Taasisi zinazolisha kati ya watu 100 hadi 300 kutokutumia kuni na Mkaa kwa kupikia ifikapo tarehe 31 Januari, 2024. Na kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 300 kutotumia kuni na mkaa kwa kupikia ifikapo tarehe 31 Januari, 2025. Katazo hilo limetolewa kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na. 12 la tarehe 24 Machi, 2023. Napenda kutumia fursa hii kutoa rai kwa taasisi hizo kuzingatia muda uliotolewa katika kukoma kwa matumizi ya kuni na mkaa.

***(xiii)* Kampeni ya kukijanisha Dodoma**

***59. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kukijanisha Dodoma ambapo Jumla ya miti 908,480 ilipandwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo: Jiji la Dodoma - miti 600,040; Wilaya ya Mpwapwa - miti 12,400; Wilaya ya Bahi - miti 25,300; Wilaya ya Chemba - miti 7,300; Wilaya ya Kongwa - miti 39,940; Wilaya ya Kondoa - miti 17,500; na Wilaya ya Chamwino - miti 152,000. Aidha, ili kutimiza azma ya Serikali ya kulifanya jiji la Dodoma kuwa la kijani natoa msisitizo kwa wadau wote wa mazingira waliopo Dodoma kuongeza kasi katika utekelezaji wa Kampeni

ya Kukijanisha Dodoma.

***(xiv)* Elimu kwa Umma Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira**

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Elimu ilitolewa kupitia runinga, redio, mitandao ya kijamii, warsha za wadau, semina, hotuba za viongozi zinazotolewa wakati wa maadhimisho ya kitaifa na kimataifa kuhusu mazingira.

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu na kutoa elimu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira, Makatibu Wakuu, Washirika wa Maendeleo, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na Sekta Binafsi. Elimu hiyo ilihusu masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi, kanuni na mwongozo wa biashara ya Kaboni. Aidha, Ofisi ilitoa mafunzo ya kujenga uwezo wa Wizara za Kisekta na Taasisi 30 kuhusu kusimamia na kuratibu shughuli za kupunguza hewa ukaa inayotokana na ukataji na uharibifu wa misitu na kuandaa maandiko ya miradi ya kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi.

***62. Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo wadau mbalimbali ikiwemo Wizara za Kisekta na Taasisi za Serikali ili kuzingatia utekelezaji wa Mpango kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo. Elimu ilitolewa kwa wanahabari 50, wachimbaji wadogo 39 na Maafisa Mazingira wa Mikoa 12 yenye uchimbaji wa dhahabu. Aidha, Ofisi imetoa mafunzo kwa Maafisa mazingira na Wakaguzi wa mazingira 50 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu udhibiti na uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa kemikali na taka hatarishi.

***(xv)* Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani**

***63. Mheshimiwa Spika,*** maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani hufanyika tarehe 5 Juni kila mwaka. Kwa mwaka 2023 maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Kimataifa

yatafanyika Abidjan, Ivory Coast na Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo ni: "*Beat Plastic Pollution*" kwa kiswahili ni "Tokomeza uchafuzi wa Mazingira utokanao na Matumizi ya Mifuko ya Plastiki".

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi inaendelea na Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambapo kaulimbiu ya kitaifa ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni "Pinga Uchafuzi wa Mazingira Utokanao na Mifuko ya Plastiki". Kaulimbiu hii inahamasisha jamii kusitisha uzalishaji na matumizi ya bidhaa za plastiki ikiwemo mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na matumizi ya vifungashio vya plastiki kama vibebeo kwa lengo la kuhifadhi mazingira yetu. Aidha, maadhimisho ya mwaka huu yataenda sambamba na Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2023 ambazo ujumbe wake mkuu ni **Mabadiliko ya Tabianchi, Hifadhi ya Mazingira na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji** – chini ya kaulimbiu isemayo –"*Tunza mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa Ustawi wa Viumbe Hai na Uchumi wa Taifa*".

### *(xvi)* Maadhimisho ya Siku ya Kuhifadhi Tabaka la Ozoni Duniani

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 Ofisi iliratibu maadhimisho ya Siku ya Ozoni Duniani yaliyokuwa na Kauli Mbiu ya "Miaka 35 ya Itifaki ya Montreal: Ushirikiano wa Kimataifa katika kulinda afya ya binadamu na mazingira". Maadhimisho hayo hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka. Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika Jijini Arusha. Katika maadhimisho hayo shughuli zilizofanyika ni pamoja na: mafunzo kwa maafisa 35 kutoka kwenye Wizara na Taasisi za Serikali zilizopo katika mpaka wa Namanga, Arusha kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; mafunzo kwa mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu 40 wa mkoa wa Arusha kuhusu njia bora za kukarabati vifaa hivyo pasipo kuachia

angani kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulinda Tabaka la Ozoni kupitia vipindi vitatu(3) vya redio na kipindi kimoja (1) cha runinga. Aidha, katika kudhibiti uingizwaji wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni, Ofisi ilitoa mafunzo kwa maafisa forodha, wakala wa forodha na wasimamizi wengine wa sheria wapatao 160. Mafunzo hayo yalitolewa katika Vituo vya forodha vya Dar es salaam na Vituo vya Mipaka ya Horohoro - Tanga na Tunduma – Songwe.

**(xvii) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazoikabili dunia ambapo Ofisi ilishiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kimataifa inayohusu Mazingira. Aidha, Ofisi ilishiriki Mkutano wa kwanza wa majadiliano ya kuanzisha Mkataba wa Kimataifa wa Kukabiliana na Uchafuzi wa Plastiki uliofanyika Desemba, 2022 katika Jiji la *Punta del Este, Uruguay*. Lengo la mkataba huo ni kudhibiti matumizi ya plastiki katika mazingira na bahari kwa kudhibiti uzalishaji, matumizi na uteketezwaji wake.

***(xviii)*** **Mkutano wa Mawaziri Kumi wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Tanzania ilishiriki Mkutano wa kumi wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe 08 Desemba, 2022 Bujumbura, Burundi. Mkutano huo ulihusisha nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Tanzania. Masuala muhimu yaliyojadiliwa na kupitishwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa programu za usimamizi wa mazingira katika ngazi ya kanda zinazosimamiwa na Sekretarieti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika; na Kuendelea na mikakati ya

utafutaji fedha katika ngazi ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza kasi ya kuhifadhi mazingira ya Ziwa Tanganyika na bonde lake. Katika mkutano huo, Tanzania ilikabidhi Uenyekiti kwa Jamhuri ya Burundi na ilikubalika kwamba lugha ya Kiswahili iwe lugha mojawapo ya mawasiliano katika mikutano ya mkataba huu.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akimkabidhi nyundo Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo wa Burundi Prof. Sanctus Niragira, kama ishara ya makabidhiano ya Uenyekiti wa Mkutano wa 10 wa Mawaziri waliopo katika Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe ya 8 Desemba, 2022 jijini Bujumbura nchini Burundi.*

### *(xix)* Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

***68. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hicho jumla ya miradi nane (8) ilitekelezwa kama ifuatavyo: -

**a) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia**

**69. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia unaotekelezwa katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini A -Unguja. Lengo la mradi ni kuongeza uwezo wa jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kujiongezea kipato kwa kutumia mifumo ikolojia. Katika kutekeleza kazi za mradi, kiasi cha **Shilingi bilioni 3.8** kilitumika. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Uchimbaji wa visima virefu 12 vyenye urefu wa mita 100-150; ujenzi wa malambo saba (7); ujenzi wa majosho sita (6); ujenzi wa viwanda vidogo viwili (2) vya bidhaa za ngozi na kimoja (1) cha kuchakata mafuta ya alizeti.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Dkt. Switbert Mkama akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa visima vya maji safi vilivyochimbwa kupitia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia (EBARR) katika Halmashauri ya Mpwapwa Mkoani Dodoma.*

**b) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa**

***70.*** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa unaotekelezwa katika Halmashauri za Ludewa, Makete, Nyasa, Mbinga na Kyela. Lengo la mradi ni kuhifadhi mazingira katika Bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya jamii inayozunguka bonde hilo. Katika kutekeleza shughuli za mradi, kiasi cha **Shilingi milioni 435** kilitumika kutekeleza kazi za mradi.

**c) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania**

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini katika Wilayaza Magu, Nzega, Mkalama, Kondoa na Micheweni - Pemba. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo - ikolojia ili kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula katika maeneo husika. Katika kutekeleza shughuli za mradi kiasi cha **Shilingi bilioni 1.6** kilitumika. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Uandaaji na utoaji wa hati miliki 2,284 za kimila za ardhi; uchimbaji wa visima 22; ujenzi wa maghala matatu (3) kwa ajili ya kuhifadhi mazao hususani mpunga; na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kukusanya mazao ya nyuki.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis akitazama kondoo wanaofugwa na wananchi wa kijiji cha Lumeji kilichopo Kata ya Sukuma Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza ambao ni wanufaika wa Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame Tanzania (LDFS) wakati wa ziara yake ya kukagua miradi hiyo tarehe 23 Februari, 2023.*

**d) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto wa Asili na Hifadhi ya Bionuai katika mifumo ikolojia ya Bonde la Ruaha Mkuu na Ziwa Rukwa**

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai katika mifumo ikolojia ya Bonde la Ruaha Mkuu na Ziwa Rukwa. Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo ikolojia na jamii kwa ujumla. Mradi huu

unatekelezwa katika Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga vijijini na Mpimbwe katika bonde la Ziwa Rukwa na katika Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika bonde la Ruaha Mkuu. Katika kipindi hicho, jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** zilitumika katika kutekeleza shughuli za mradi.

**e) Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

***73. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kuratibu Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm unaohusu Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu. Lengo la mradi ni kulinda afya ya binadamu na mazingira kutokana na athari za kemikali hizo. Kiasi cha **Shilingi milioni 171.8** kimetumika kutekeleza kazi za mradi.

**f) Mradi wa Kupunguza uzalishaji wa Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji miti na Uharibifu wa Misitu nchini.**

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu nchini. Lengo la mradi ni kuiwezesha Tanzania kuwa tayari katika utekelezaji wa makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na kunufaika na biashara ya kaboni. Katika kipindi hicho, kiasi cha **Shilingi milioni 180** kimetumika kutekeleza kazi za mradi.

**g) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa kutekeleza Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi unaolenga kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

ambapo katika kipindi hicho jumla ya kiasi cha **Shilingi milioni 94.7** kilitumika kutekeleza shughuli za mradi.

**h) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

***76. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Lengo la mradi ni Kujenga uwezo wa Kitaifa kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 320.6** kimetumika katika utekelezaji wa shughuli za mradi.

**MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA**

***77. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2022/23 ni pamoja na: Ukarabati wa makazi ya Makamu wa Rais Kilimani – Dodoma; Luthuli II Dar es Salaam; na kuendelea kusimamia ujenzi wa Ofisi ya kudumu katika Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma; Kuandaa Andiko la Uchumi wa Buluu kwa ajili ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu; Utoaji wa mafunzo kwa watumishi 192; Upandishwaji vyeo kwa watumishi 27; Ajira mpya watumishi watano (5); Semina kuhusu masuala ya udhibiti wa maadili kwa watumishi 80; Upatikanaji wa vitendea kazi; na Stahili mbalimbali za watumishi; Kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja; na Kuratibu kikao cha Baraza la Wafanyakazi.

***78. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa ni: Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kuandaa taarifa za hesabu za fungu 26 na 31 ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Miradi ya Maendeleo; na Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; na kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

**CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO**

***79. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: Kuendelea kuwepo kwa hoja nne (4) za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi; Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Muungano; Uzingatiaji hafifu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake; na Uelewa Mdogo wa jamii kuhusu masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

***80. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi, hatua zifuatazo zimechukuliwa:- Kitabu cha Historia ya Muungano kupata ithibati ya kutumika kama kitabu cha ziada katika shule za Sekondari; Kuendelea kutafuta ufumbuzi wa hoja nne (4) za Muungano ambazo hazijatatuliwa; Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; na Kujenga uwezo kwa wataalam katika Mamlaka za Serikali za Mtaa ili kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya hifadhi ya mazingira katika ngazi mbalimbali hususani ngazi ya jamii, wamiliki wa viwanda, migodi, wadau wa urejelezaji wa taka na wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu na vyanzo vya maji.

## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 masuala yaliyotekelezwa yanajumuisha:

***(i)*** **Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria yaMazingira, Sura 191**

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Baraza limefanya jumla ya kaguzi 480 katika maeneo mbalimbali

ikiwemo: Maeneo ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini; viwanda; Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa; Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere; Miundombinu ya upakiaji wa Makaa ya Mawe; Upakuaji wa mafuta kutoka melini; na Maeneo yanayotumika kuhifadhi taka hatarishi.

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Baraza lilifuatilia utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa mazingira katika miradi iliyopata Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Maeneo mahususi yaliyofanyiwa ukaguzi ni pamoja na Mgodi wa Dhahabu wa North Mara, Ufuatiliaji wa Bwawa la kuhifadhi Tope katika Mgodi wa Williamson Diamond Limited, Mgodi wa Sunshine, Ufuatiliaji wa katazo la mifuko ya plastiki isiyokidhi viwango vya ubora na kufuatilia utekelezaji wa mwongozo wa Usafishaji Mito katika Mkoa wa Dar es Salaam.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Mhandisi Samuel Gwamaka Mafwenga akiwa katika moja ya Operesheni za uteketezaji wa Vifungashio vya Plastiki visivyokidhi viwango ambapo tani 44.4 ziliteketezwa tarehe 15 Septemba, 2022 Jijini Dar es Salaam.*

***(ii)* Kushughulikia Malalamiko ya Umma Kuhusu Uchafuzi na**

**Uharibifu wa Mazingira**

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Baraza limeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake ambapo Baraza lilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 317. Malalamiko hayo yalihusu uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo, uchafuzi wa hewa, utiririshaji wa maji taka katika mazingira, umwagikaji wa mafuta kwenye miundombinu ya ushushaji wa mafuta kwenye meli kwenda kwenye matenki ya kuhifadhi mafuta, uchimbaji holela wa mchanga na utupaji holela wa taka ngumu. Katika kushughulikia malalamiko hayo, Baraza lilichukua hatua za kisheria ikiwemo kutoa onyo na adhabu. Aidha, elimu iliendelea kutolewa ili kuhamasisha jamii kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake.

***(iii)*** **Udhibiti wa Taka Hatarishi**

***85. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23, Baraza limepokea maombi **60** ya usimamizi wa uteketezaji wa taka hatarishi ambapo kiasi cha tani **3,422** za taka hatarishi zimeteketezwa zikiwemo dawa, bidhaa za viwandani zilizokwisha muda wake pamoja na kemikali zisizofaa kwa matumizi. Vilevile, Baraza limeshughulikia maombi ya vibali vya taka hatarishi aina ya chuma chakavu, betri chakavu, mafuta machafu, taka za kielektroniki, tairi chakavu, taka za kemikali na taka za plastiki ambapo jumla ya vibali **272** vimetolewa.

***(iv)*** **Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)**

***86. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2022/23, Baraza limesajili jumla ya miradi 1,316 ambapo miradi 933 ni miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Miradi 383 imefanyiwa Ukaguzi wa Mazingira. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya miradi 691 imeidhinishwa na kupata vyeti vya TAM.

### *(v)* Usajili wa Washauri Elekezi wa Mazingira

***87. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 Baraza limesajili washauri elekezi binafsi 27 wa TAM na 19 wa Ukaguzi wa Mazingira ambao walitangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 11 Novemba, 2022. Vilevile, maombi 26 ya washauri elekezi binafsi wa TAM na 10 wa Ukaguzi wa Mazingira pamoja na kampuni tatu (3) za ushauri za TAM ziliidhinishwa na Bodi ya NEMC.

### *(vi)* Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi ya Mazingira

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 Baraza limeendelea kutoa elimu kwa umma na mafunzo kwa wadau kuhusu masuala ya usimamizi wa utunzaji wa mazingira kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo: Mkutano wa 21 wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki wa Afrika Mashariki; Maonesho ya kilimo yaliyofanyika Morogoro; Maonesho ya Biashara na viwanda yaliyofanyika Kibaha; Maonesho ya sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam; na maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Mbeya. Aidha, katika kipindi hicho Baraza liliandaa makala 30 na Habari 98 kuhusu masuala mbalimbali ya utunzaji wa mazingira yaliyorushwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Pia Baraza limeratibu mikutano 13 ya waandishi wa habari kuhusu masuala ya usimamizi wa mazingira.

## C: MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/24

### MASUALA YA MUUNGANO

### *(i)* Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano

***89. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu utatuzi wa hoja nne (4) zilizobakia na zitakazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kupitia Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya

Muungano. Vikao hivi vitafanyika katika ngazi tatu (3) ambazo ni: - Kamati ya Pamoja; Mawaziri; na Makatibu Wakuu. Aidha, kutakuwa na Vikao vya Kamati Ndogo za Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala vitakavyofanyika kulingana na mahitaji. Vikao hivyo vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ. Ofisi itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na Kamati ya Pamoja kwa sekta zenye hoja.

***(ii)*** **Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano**

***90. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itafanya maandalizi ya kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuwa na mfumo endelevu wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka za Muungano ili kuongeza uelewa wa masuala ya Muungano kwa kizazi cha sasa na kijacho.

***(iii)*** **Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii**

***91. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar. Aidha, Ofisi itatoa mafunzo ya usimamizi wa miradi inayogharamiwa na fedha za Mfuko wa Jimbo kwa Waheshimiwa Wabunge, Wakurugenzi wa Halmashauri na wataalamu katika Halmashauri za Zanzibar.

***(iv)*** **Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano**

***92. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Taasisi za SJMT na SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana ili kuimarisha ushirikiano kati ya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**(*v*) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Masuala ya Muungano**

***93. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho, majarida na mitandao ya kijamii. Aidha, Ofisi itatumia maonesho, makongamano na matukio mbalimbali ya kitaifa kutoa elimu ya Muungano.

**(*vi*) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

***94. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano yaliyo orodheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**(*vii*) Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

***95. Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2024 Muungano wa Tanganyika na Zanzibar utatimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Kutokana na umuhimu wa maadhimisho hayo, Ofisi itaandaa machapisho mbalimbali kuhusu Muungano kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

**(*viii*). Kuandaa Mfumo wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano**

***96. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaandaa Mfumo wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano wenye lengo la kurahisisha upatikanaji, uandaaji, uchambuzi na uunganishaji wa taarifa za utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Aidha, Ofisi itatoa mafunzo kwa Maafisa Viungo wa Wizara na Taasisi kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano na mfumo husika.

## HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WAMAZINGIRA

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha hifadhi endelevu ya mazingira, kwa mwaka 2023/24, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele vitano (5) vifuatavyo: Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa Mazingira; Kuimarisha usimamizi wa biashara ya Kaboni nchini; Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Fursa ya Biashara ya Kaboni; Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikijumuisha utoaji elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira; na Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

### (i) Kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza kazi zifuatazo: Kuandaa na kutekeleza miongozo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ikiwemo Mpango wa Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2023 – 2030); Kufuatilia utekelezaji wa Miongozo ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ikiwemo Mwongozo wa Dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza, na Mwongozo wa Kelele na Mitetemo; Kufanya uchambuzi na kutoa vibali vya taka hatarishi, Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Ukaguzi wa Mazingira, Tathmini ya Mazingira Kimkakati; Kutoa mafunzo kwa wakaguzi na wataalamu wa mazingira kuhusu Sheria ya usimamizi wa mazingira; na Kutoa elimu kuhusu Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

### (ii) Kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi

**wa mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa**

***99. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika ngazi za Serikali za Mitaa, Ofisi itaendelea kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na mkakati wa utekelezaji na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.

**(iii) Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032)**

***100. Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Miji na Majiji ikiwemo udhibiti wa taka na upandaji miti; Kuendelea kuratibu utekelezaji wa program ya Kukijanisha Jiji la Dodoma; Kuratibu shughuli za hifadhi ya vyanzo vya maji na kufanya tathmini ya hali ya ardhi oevu nchini; Kuratibu usimamizi wa utekelezaji wa jitihada mbalimbali za kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi; Kufanya tathmini ya fursa za uwekezaji katika biashara ya Kaboni; na Kufuatilia utekelezaji wa mipango na mikakati ya kisekta ya hifadhi ya misitu na matumizi ya nishati mbadala.

**(iv) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpangokazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu Nchini (2020 – 2025)**

***101. Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu Nchini (2020 – 2025). Vilevile, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na mafunzo kwa maafisa mazingira, maafisa forodha, wakaguzi kutoka katika mamlaka za udhibiti kuhusu kudhibiti uingizaji, matumizi salama ya zebaki, utupaji wa taka zitokanazo na zebaki na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki.

**(v) Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya usimamizi wa mazingira**

***102. Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; Kuratibu Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa; Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya kikanda na Kimataifa ya Hifadhi ya Bioanuai; Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya udhibiti wa kemikali na taka hatarishi; na Kuratibu uandishi wa miradi ya kipaumbele kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi.

**Kazi nyingine zitakazotekelezwa na Ofisi**

***103. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2023/24 ni pamoja na: Kusimamia Menejimenti ya Rasilimaliwatu na Utawala; Kuandaa Sera ya Uchumi wa Buluu na Mkakati wa Utekelezaji; Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Kuelimisha umma kuhusu majukumu, Sera, mikakati na programu zinazotekelezwa na Ofisi; Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa; Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31 ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Miradi ya Maendeleo; na Kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

**Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

***104. Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka 2023/24, Ofisi itaratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ifuatayo:

**a) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bondela Ziwa Nyasa**

***105. Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za Ludewa na Makete, Kyela, Nyasa na Mbinga. Lengo la Mradi ni kuhifadhi mazingira ya bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya jamii inayozunguka eneo hilo. Katika mwaka 2023/24, **Shilingi milioni 344.8** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii ili kukabiliana na uharibifu wa ardhi katika bonde la Ziwa Nyasa.

**b) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bioanuai**

***106. Mheshimiwa Spika,*** Mradi huuunatekelezwa katika Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga vijijini na Mpimbwe katika bonde la Ziwa Rukwa na wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika bonde la Ruaha Mkuu. Lengo la mradi ni kurejesha uoto wa asili na hifadhi ya bioanuai kupitia usimamizi jumuishi wa mifumo ikolojia**.** Kwa mwaka 2023/24 kiasi cha **Shilingi bilioni 4.0** zimetengwa kwa kazi ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, majosho 14, visima virefu sita (6) malambo matatu (3) na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 38 na urejeshaji wa misitu na mazingira.

**c) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

***107. Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/24**, Shilingi milioni 342** zimetengwa kazi zitakazotekelezwa zinajumuisha kutoa mafunzo kwa maafisa forodha, maafisa Ununuzi na Ugavi na wasimamizi wa sheria kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozone pamoja na Kutoa vifaa kwa vyuo vya VETA vinavyofundisha fani ya kukarabati viyoyozi na majokofu na Mamkala ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

**d) Mradi wa kutekeleza Mkataba wa Stockholm unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

***108. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, **Shilingi milioni 609.2** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo: Kujenga vituo vitatu vya kuchambua taka zinazorejelezeka katika Manispaa za Kigamboni na Ubungo; Kuratibu na kusimamia uondoshaji wa mafuta ya transfoma na vifaa vilivyothibitika kuwa na kemikali ya PCBs kwa njia salama; na Kurejesha eneo la Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Morogoro lililochafuliwa na Viuatilifu vyenye kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.

**e) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania**

***109. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Kondoa, Mkalama, Nzega, Magu na Micheweni - Pemba. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo ya kiikolojia ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika na unategemea kuongoa hekta 9,000 za ardhi zilizoharibika. Kwa mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi milioni 324.1** zimetengwa kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi, kufanya tathmini ya mwisho na kufanya ukaguzi wa mradi.

**f) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia**

***110. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Simanjiro, Mpwapwa, Kishapu, Mvomero na Kaskazini A - Zanzibar. Lengo la mradi ni kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini Tanzania kwa kuimarisha mifumo ikolojia. Katika mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi bilioni 3.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo kuendelea na uchimbaji visima virefu viwili (2); uchimbaji wa malambo matatu (3); ujenzi wa kiwanda kidogo cha bidhaa za ngozi; kukamilisha

ujenzi wa mabirika manne ya kunyweshea mifugo; na utengenezaji wa majiko banifu na uzalishaji wa biogas.

**g) Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu waMisitu**

***111. Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kujenga uwezo wa kitaasisi katika kupunguza Hewa Ukaa ifikapo Mwaka 2023. Katika mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi milioni 407.2** kimetengwa kwa ajili ya Kujenga uwezo wa Kitaasisi kupitia utoaji wa vifaa na kutoa elimu kwa umma kuhusu upunguzaji uzalishaji wa gesi joto utokanao na ukataji na uharibifu wa misitu.

**h) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

***112. Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu ni wa kitaifa wenye lengo la kuimarisha uwezo wa Taasisi na Mamlaka husika ikiwemo mifumo na nyenzo za kisasa katika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Katika mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi bilioni 2.6** kimetengwa kwa ajili ya kujenga uwezo wa taasisi kusimamia Sheria ya mazingira ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni tano (5), miongozo mitano ya usimamizi wa mazingira, kanzi data ya tathmini ya mazingira pamoja na kuanzisha Jukwaa la kitaifa la usimamizi wa mazingira.

**i) Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Kingo za fukwe katika maeneo ya mwambao Mikindani - Mtwara na Sipwese - Pemba**

***113. Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu una lengo la kurejesha uasili wa mazingira katika maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa Bahari nchini. Katika mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi bilioni 1.0** kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kingo katika fukwe za Mikindani na Sipwese.

**j) Mradi wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi katika jamii zinazozunguka misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar**

***114. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa katika misitu ya Miombo iliyopo katika mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la Mradi huu ni Kupunguza athari na kujenga/kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii pamoja na ikolojia katika Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Maeneo Kame ya Zanzibar. Katika mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi milioni 850.8** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WAMAZINGIRA**

***115. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24 Baraza limepanga kuendelea kutekeleza kazi zifuatazo: Kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 kwa kufanya kaguzi na ufuatiliaji katika migodi, viwanda na miradi inayotekelezwa nchini ili kulinda na kutunza mazingira; Kuratibu Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kusajili na kufanya mapitio ya miradi pamoja na kusajili Wataalam Elekezi wa Mazingira; Kufanya tafiti ya kubaini malighafi zinazoweza kuoza katika mazingira ambazo zitatumika kutengeneza mifuko mbadala; kuendesha kongamano la sita la Sayansi kuhusu uhifadhi wa maeneo oevu; Kuratibu na kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Uchafuzi wa mazingira unaotokana na matumizi ya zebaki; Tathmini ya vyanzo vya maji; Kujenga uwezo wa kitaasisi katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; na Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira.

**HITIMISHO NA SHUKRANI**

***116. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Aidha, shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake, dira na maelekezo aliyotupatia kuhusu majukumu yetu. Vilevile, ninamshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake katika kutoa maelekezo ili kutimiza majukumu yetu. Kadhalika, ninamshukuru **Mheshimiwa Khamis H. Khamis (Mb.),** Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

***117. Mheshimiwa Spika,*** Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wasaidizi wangu katika utendaji kazi wa Ofisi, napenda kumshukuru Bi. Mary N. Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; akisaidiwa na Bw. Abdallah H. Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano); na Dkt. Switbert Z. Mkama, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Hali kadhalika, ninawashukuru pia Prof. Mhandisi Esnath O. Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NEMC, Dkt. Mhandisi Samwel G. Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na NEMC kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Ninawashukuru wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/24.

***118. Mheshimiwa Spika***, Mafanikio tuliyopata mwaka huu yametokana na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Wadau mbalimbali. Baadhi ya Washirika wa Maendeleo tuliofanya nao kazi kwa karibu ni pamoja na: Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Serikali ya Norway; Serikali ya Sweden; Serikali ya Uingereza; Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Mfuko wa Kuhimili

Mabadiliko ya Tabianchi (AF); Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (FCDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo (UNCDF); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - IFAD; Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ); Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); Sekta Binafsi; na Mabalozi wa Mazingira. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi katika kuimarisha Muungano wetu na kuhifadhi Mazingira yetu.

**MAOMBI YA FEDHA**

***119. Mheshimiwa Spika,*** ili Ofisi iweze kufikia malengo tarajiwa kama nilivyobainisha kwenye hotuba yangu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2023/24 kama ifuatavyo: -

**FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS**

***120. Mheshimiwa Spika***, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 14,731,640,000.00** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 1,251,640,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na **Shilingi 13,480,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

***121. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 39,370,444,000.00** kwa ajili ya Fungu 31. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 20,712,399,000.00** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Shilingi **18,658,045,000.00** ni Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **Shilingi 3,349,788,000.00** Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi5,264,448,000.00** Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na **Shilingi 12,098,163,000.00** Matumizi Mengineyo. Aidha,Matumizi ya Miradi ya Maendeleo yanajumuisha **Shilingi 3,602,000,000.00** fedha za Ndani na **Shilingi 15,056,045,000.00** fedha za Nje.

***122. Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdullah wakiwa katika picha ya pamoja na Mawaziri wa SJMT na Mawaziri wa SMZ mara baada ya kumalizika kwa kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kilichofanyika katika Ukumbi wa Kambarage,Treasury Square jijini Dodoma tarehe 06 Desemba, 2022.*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema aliyotujalia na ametupa afya kubwa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile taarifa ya kamati hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa. Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, sehemu ya tatu inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati na sehemu ya nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu mawili ambayo ni Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya hii. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 24 Machi, 2023. Uchambuzi huo umejikita katika kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu hili lilidhinishiwa jumla ya Sh. 12.9 kwa matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo shilingi milioni 974.2 sawa na asilimia 7.5 ilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 12 sawa na asilimia 92.5 ilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 8.5 kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 65.9. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 446.9 sawa na asilimia 45.9 ilipokelewa kwa ajili ya mishahara na shilingi 8.1 sawa na asilimia 67.5 ilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea Fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida hususan bajeti ya Mishahara ni matarajio ya ofisi hii kuwa na ajira mpya ambao hadi

Februari, 2023 hawakupokea watumishi wapya wala watumishi waliopandishiwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13.4. kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23 sawa na asilimia 17.6 ilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 8.2 sawa na asilimia 61.4 ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 2.8 sawa na asilimia 21 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 7.6 sawa na asilimia 57. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.3 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 5.3 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 1.07 sawa na asilimia 38.27 zilipokelewa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya miradi ya maendeleo hadi kufikia Februari, 2023 ni ucheleweshaji wa kuandaa hati za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba, kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 29.2 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hii ilipokea Jumla ya Shilingi bilioni 17.2 sawa na asilimia 60 ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na

Mazingira ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja na mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha kuwa mwenendo wa matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023 kiasi cha shilingi biioni 1.0 kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Kilimani Dodoma na Oysterbay Dar es salaam pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II – Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo hadi kufikia Februari, 2023 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ukarabati wa Makazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Kilimani – Dodoma na Oysterbay Dar es Salaam, hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya

shilingi milioni 991.4 zilikwishalipwa kwa mkandarasi *M/s Corporation Sole Works Superintendent* kwa ajili ya kazi zilizofanyika ambazo zinajumuisha ujenzi wa ukuta, ujenzi wa nyumba ya mapumziko kwa ajili ya madereva na ujenzi wa miundombinu mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II - Dar es Salaam, hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya shilingi milioni 87.9 zimekwishalipwa kwa mkandarasi *ARU Built Environment Consulting Company Ltd.* Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uzibaji wa nyufa katika kuta, ukarabati wa dari, kupaka rangi ndani na nje ya jengo, kuweka mfumo wa zimamoto, kukarabati mfumo wa maji safi na maji taka, kukamilisha uzio, kukarabati milango, ngazi na geti la kuingilia. Kazi zinazoendelea ambazo zipo katika hatua za awali ni pamoja na matengenezo ya sehemu ya kuegeshea magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo Matano. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu ofisi kuondoa kipengele cha makusanyo katika makadirio na mapato iwapo ofisi hii haina vyanzo vyake vya makusanyo ya maduhuli. Kwenye randama za ofisi zilizowasilishwa Machi, 2023, kipengele cha makusanyo na maduhuli kiliondolewa kama ilivyo shauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya Kudumu za Bunge zinatambua umuhimu na uzoefu unaopatana katika mwaka

wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo wa masharti ya Kanuni ya Bunge kwa kuchambua Makadirio na Matumizi ya mwaka wa fedha 2023/2024, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Taasisi zilizoko chini yake imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 26.8 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.7 ni kwa ajili ya Mishahara na Bilioni 23.0 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika mwaka wa fedha 2023/2024, imeongezeka kwa asilimia 1.58 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha ambapo Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa ni Bilioni 26.3. Kamati imebaini kwamba moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange Bajeti kulingana na mahitaji halisi. Hali ya ongezeko hili linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwepo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizoombwa zinatumika vizuri ili kuhakikisha kwamba bajeti inatekelezwa ipasavyo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria kwa mchanganuo kama ilivyoelezwa kwenye kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 2.0 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kiasi hiki cha fedha kinatokana na fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imepungua kwa zaidi ya Shilingi Milioni 818, sawa na asilimia 40.9 ya upungufu ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwa sababu ya upungufu wa Bajeti kwa Maendeleo ni kutokana na kutokuwepo kwa miradi mipya inayotekelezwa na ofisi hii na kwamba Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi hii inaomba fedha za ukamilishaji wa Miradi ya Ukarabati, Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, Dar es Salaam, Pemba iliyoanza kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati. Baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi wa kubaini maoni ya Kamati yaliyojenga mtazamo ambao ndiyo msingi wa ushauri wa Kamati na maoni haya ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa mipango na majukumu ya bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarijio ya wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi chochote cha fedha ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(c) Upo umuhimu wa Wizara kuendelea kutoa elimu ya mara kwa mara kuhusu umuhimu na faida za Muungano;

(d) Selikali ifanye tathimini ya uwiano wa watumishi wa umma kwenye Taasisi za Muungano ili kubaini kama mgawanyo wa watumishi umezingatia pande zote mbili za Muungano; na

(e) Uwepo umuhimu wa Serikali kufanya marekebisho ya sheria ili kutoa fursa ya ugawaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo kwa Wabunge wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushauri wa Kamati; kwa maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi huu naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kutoa elimu ya kutosha kuhusu historia, faida na umuhimu wa Muungano wetu katika ngazi mbalimbali za kwenye jamii;

(b) Serikali ihakikishe kuna uwiano wa Watumishi wa Taasisi za Muungano ili kuzingatia pande mbili zote za Muungano;

(c) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge ni kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake zinapatikana kwa ukamilifu ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu uliyopangwa; na

(d) Serikali ihakikishe kuna usawa kwenye ugawaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo kwa Wabunge wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Naomba majina yao yote yaingizwe kwenye kumbukumbu na Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa

Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati. Naomba pia niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Mary Maganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati za Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, niwashukuru Makaimu Wakurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati Ndugu Frank Nkya, Ndugu Praisegod Lukio, Ndugu Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### *1.1. Maelezo ya Awali*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

c) Sehemu ya tatu inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

d) Sehemu ya nne ni Hitimisho.

### 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a)

cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu mawili (2) ambayo ni:-

a) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais,

b) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### *2.1 Ufafanuzi wa Jumla*

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023*

Mheshimiwa Spika, **napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya hii. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 24 Machi, 2023. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -**

**2.2.1 Fungu Na. 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu hili lilidhinishiwa jumla ya **Sh. 12,974,292,000** kwa matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 974,292,000** sawa na **asilimia 7.5** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 12,000,000,000** sawa na **asilimia 92.5** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 8,547,743,696.7** kwa matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 65.9**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 446,963,096.7** sawa na **asilimia 45.9** ilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 8,100,780,600** sawa na **asilimia 67.5** ilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea Fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida hususan bajeti ya Mishahara ni matarajio

ya ofisi hii kuwa na ajira mpya ambao hadi Februari, 2023 hawakupokea Watumishi wapya wala Watumishi waliopandishiwa vyeo.

**2.2.2 Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Raisi Muungano**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 13,409,672,470**. kati ya fedha hizo **Sh. 2,361,333,270** sawa na **asilimia 17.6** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 8,228,339,200** sawa na **asilimia 61.4** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 2,820,000,000** sawa na **asilimia 21** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 7,630,238,323.84** sawa na **asilimia 57**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,321,278,127.9** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 5,329,546,196.2** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 1,079,413,999.72** sawa na **asilimia 38.27** zilipokelewa kwa ajili ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya mradi wa maendeleo hadi kufikia Februari, 2023 ni ucheleweshaji wa kuandaa hati za malipo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba, kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 29,203,964,470** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 17,257,396,020.26** sawa na **asilimia 60** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya

taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na**. **1** na **Na. 2.**

**KIELELEZO NA. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26**– Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais | 12,974,292,000 | 8,547,743,696.7 | 65.9 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 10,589,672,470 | 6,650,824,324.12 | 63 |
| **JUMLA KUU** | **23,563,964,470** | **15,198,568,020.8** | **64.5** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira, 2023.*

**KIELELEZO NA. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 31**– Ofisi ya | 2,820,000,000 | 1,079,413,999.72 | 38.27 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | | | |
| **JUMLA KUU** | **2,820,000,000** | **1,079,413,999.72** | **38.27** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira, 2023.*

### *2.3 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano*

**Mheshimiwa Spika,** bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati **Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora.

### *2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii ilitengewa jumla ya **Sh. 2,820,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hadi kufikia Februari, 2023 kiasi cha **Sh. 1,079,413,999.72** kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Mhe. Makamu wa Rais Kilimani Dodoma na Oysterbay Dar es

salaam pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II – Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo hadi kufikia Februari, 2023 ni kama ifuatavyo:-

**2.4.1 Ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais Kilimani – Dodoma na Oysterbay Dar es Salaam**

Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya shilingi **991,477,872.87** zimekwishalipwa kwa mkandarasi *M/s Corporation Sole Works Superintendent* kwa ajili ya kazi zilizofanyika ambazo zinajumuisha: Ujenzi wa ukuta; ujenzi wa nyumba ya mapumziko kwa ajili ya madereva; na ujenzi wa miundombinu mingine.

**2.4.2 Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II - Dar es Salaam**

Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya shilingi **87,936,086.85/=** zimekwishalipwa kwa mkandarasi *ARU Built Environment Consulting Company Ltd*. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Uzibaji wa nyufa katika kuta; ukarabati wa dari; kupaka rangi ndani na nje ya jengo; kuweka mfumo wa zimamoto; kukarabati mfumo wa maji safi na maji taka; kukamilisha uzio; na kukarabati milango, ngazi na geti la kuingilia. Kazi zinazoendelea ambazo zipo katika hatua za awali ni pamoja na matengenezo ya sehemu ya kuegesha magari.

***2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023,

Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Matano (5). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri uliozingatiwa, unahusu Ofisi hii kuondoa kipengele cha makusanyo katika Makadirio ya Mapato iwapo Ofisi hii haina vyanzo vyake vya makusanyo ya maduhuli, kwenye Randama za Ofisi hii zilizowasilishwa Machi, 2023 kipengele cha Makusanyo ya Maduhuli kimeondolewa kama ilivyoshauriwa na Kamati.

### *2.6 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo:-

#### 2.6.1 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,801,422,100** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 3,740,760,000** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Sh. 23,060,662,100** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 1.58** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh. 26,383,964,470** Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na

mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3**

**KIELELEZO NA. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2022/2023 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | ASILIMIA YA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26** – Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais | 12,974,292,000 | 14,731,640,000 | 13.54 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais | 10,589,672,470 | 12,069,782,100 | 14 |
| **JUMLA KUU** | **26,383,964,470** | **26,801,422,100** | **1.58** |

*Chanzo:* ***Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira, 2023.***

### 2.6.2 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 2,002,000,000** kwa ajili ya Utekelezaji

wa Miradi ya Maendeleo, Kiasi hichi cha fedha kinatokana na fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepunguwa kwa Sh. 818,000,000 sawa na asilimia 40.9 ya upungufu ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa sababu ya upungufu wa bajeti ya maendeleo nikutokana na kutokuwepo kwa mradi mpya unaotekelezwa na Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi hii inaomba fedha za ukamilishaji wa mradi wa ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, Dar es salaam na Pemba ulioanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## SEHEMU YA TATU

### *3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI*

### *3.1 Maoni*

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarajio ya Wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(c) Upo umuhimu wa Wizara kuendelea kutoa elimu ya mara kwa mara kuhusu umuhimu na faida za Muungano.

(d) Serikali ifanye tathmini ya uwiano wa Watumishi wa umma kwenye taasisi za Muungano, ili kubaini kama mgawanyo wa Watumishi umezingatia pande zote mbili za Muungano.

(e) Upo umuhimu wa Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ili kutoa fursa sawa ya ugawaji wa fedha za mfuko wa jimbo kwa Wabunge wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

***3.2 Ushauri wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kutoa elimu ya kutosha kuhusu historia, faida na umuhimu wa Muungano wetu katika ngazi mbalimbali kwenye jamii;

(b) Serikali ihakikishe kuna uwiano wa Watumishi kwenye taasisi za Muungano kwa kuzingatia pande zote mbili za Muungano;

(c) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana kwa ukamilifu ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(d) Serikali ihakikishe kuna usawa kwenye ugawaji wa fedha za mfuko wa jimbo kwa Wabunge wa Tanzania bara na Tanzania Zanzibar.

**SEHEMU YA NNE**

## *4.0 HITIMISHO*

### 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama, Mb. - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb. - Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb. - Mjumbe
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Ndg. Mary Ngelela Maganga.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

24 Aprili, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyo, iwe kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako madhubuti, mahiri, makini na wenye uweLedi wa kutolea mfano kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa viwango vya juu kabisa ikiwa ni pamoja na kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi wa Mazingira, Usimamizi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo ni:

(i) Sehemu ya kwanza inatoa maelekezo ya jumla na kubainisha msingi wa muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya pili inachambua matokeo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo taarifa ya utekelezaji, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inaonyesha Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Matumizi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Sehemu ya Nne inaonyesha maoni ya Ushauri wa Kamati; na

(v) Sehemu ya Tano inahitimisha kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira aliyotoa mapema hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ni masharti ya Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ambapo Kamati inapewa jukumu la kuisimamia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Aidha, masharti ya Kanuni ya 118(4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, inaitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na Makadirio na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulifanywa tarehe 22 na 23 Machi, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi; sehemu hii inafafanua uchambuzi wa maeneo matatu ambao ni matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Miradi

ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, inazitaka Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilizingatia masharti hayo kwa kufanya ziara tarehe 15 Machi, 2023 na kutembelea kukagua Miradi Miwili ya Usimamizi wa Mazingira katika Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hiyo ni Mradi wa Vikundi vya Uzalishaji Mali ambapo ulitekelezwa kwa Bajeti ya shilingi bilioni 2.5. Hadi Februari, 2023 kiasi cha shilingi 1,143,800,275 kilitolewa, sawa na asilimia 45.5 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili hiyo; na Mradi wa Uchimbaji wa Visima virefu pamoja na upimaji wa ujazo wa maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo, biashara, binadamu na mifugo unaotekelezwa kwa gharama ya shilingi 216,546,000. Ufafanuzi wa kina kuhusu Miradi hii unapatikana ukurasa wa 5-9 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023; katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, lengo likiwa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa Bajeti unaoripotiwa na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzingatiaji wa Maoni ya Ushauri uliyotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitoa Ushauri katika maeneo matatu, napenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2022/2023; katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Fungu 31 iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 26,732,352,530. Kati ya fedha hizo shilingi 7,590,655,530 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 19,141,697,000 sawa na asilimia 72 ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ilipokea jumla ya shilingi 21,307,949,874.43, sawa na asilimia 80 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi 5,227,304,429.43, sawa asilimia 23.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 16,280,654,445 sawa na asilimia 76.4 ya kiasi cha fedha kilichotolewa ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na fedha zilizopokelewa. Uchambuzi huo unaonekana katika kielelezo namba moja hadi namba tatu ukurasa wa 12 na ule wa 13 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti katika vielelezo hivyo unaonyesha kuwa kwa ujumla upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya shughuli za kusimamia na kuhifadhi mazingira wa kuridhisha. Hadi Februari, 2023 fedha iliyopokelewa ni asilimia 80 ya Bajeti

yote iliyoidhinishwa na Bunge. Upatikanaji huo wa fedha katika kipindi hicho unakidhi matarajio ya Bunge kuhusu matumizi kwa ajili ya udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira hadi kufikia Februari, 2023 ni asilimia 66.2 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Upatikanaji huo wa fedha unatoa tafsiri kwamba uendeshaji wa shughuli na usimamizi, udhibiti na uhifadhi wa mazingira kwa kiasi unaendana na matarajio yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo unaolenga kuhimarisha udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira ulifikia asilimia 85 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na hivyo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka, 2023 ukurasa wa 285 ya kuendelea kukabiliana na athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Ni rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni, 2023 ili miradi iweze kukamilika kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2022/2023; bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ilikusudia kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu saba ya Idara ya Mazingira na *NEMC*. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi zote

zilizopangwa zimeripotiwa kutekelezwa. Hata hivyo uchambuzi unaonyesha yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudhibiti na kutunza mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 kinapaswa kuongezwa ili kuleta tija; na utekelezaji wa Kampeni za Upandaji na Utunzaji wa Miti hususani katika maeneo ambayo yameathirika sana na ukame hauzingatii aina ya miti inayoendana na eneo husika. Hali hii inasababisha matokeo ya kampeni kutokuwa na tija kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na *(NEMC)* kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Uchambuzi, Malengo, Mpango; matokeo ya uchambuzi yanaonyesha kuwa malengo pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 vinaendana na majukumu ya msingi ikiwemo kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa Miaka Mitano 2021/2022 mpaka 2025/2026; Malengo ya Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia *(Sustainable Development Goals)* ambapo ajenda ya mazingira ni ya 13 kati ya malengo 17 ya ajenda hiyo mpaka ifikapo mwaka 2030 na Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Jumla ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa Mwaka huo Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31, Idara ya Mazingira na *NEMC* inaombwa kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 25,298,661,900 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Uchambuzi wa Makadirio hayo unabainishwa kwenye kielelezo namba nne ukurasa wa 18 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati katika kilelezo hicho umebaini kuwa kwa ujumla Bajeti ya Ofisi ya

Makamu wa Rais, Mazingira inayoombwa kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti mazingira ni ndogo. Bajeti ya Ofisi wa Makamu wa Rais, Mazingira inayoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni tegemezi kwa asilimia 90. Fedha ya ndani inayotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni asilimia 10 tu. Takwimu hizi zinaashiria kwamba bado Serikali haijaweka msukumo unaostahili katika suala zima la mazingira ambalo ni ajenda kuu ya dunia na ndiyo mustakabali wa maisha ya viumbe hai kwenye uso wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Bajeti inayoisha, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2022/2023. Mchanganuo na ulinganisho uliofanywa unaonesha katika kielelezo Na. 05 ukurasa 20 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu katika kielelezo hicho inaonesha kwamba bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na *NEMC* kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inapungua kwa asilimia 5.4 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Kamati kuelezwa kwamba fedha zingine zimepelekwa kwenye Idara na Taasisi nyingine kwa suala la mazingira, Kamati bado ina wasiwasi kuwa hali ya kupungua kwa bajeti inaashiria kwamba msukumo wa utekelezaji wa shughuli na usimamizi wa uhifadhi wa mazingira umepungua ukilinganishwa na mpango wa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 unapungua kwa asilimia 13 ikilinganishwa na bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha za miradi ya maendeleo zinapungua kwa kiasi cha shilingi 2,485,652,000. Uchambuzi huu unabainisha kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaweza kuathirika kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ndani zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 105 ukilinganisha na kiasi kilichotengwa kwa mwaka 2022/2023. Kamati inapongeza juhudi za Serikali kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo Kamati inaona kiasi hicho cha fedha ni kidogo ukilinganisha na majukumu makubwa ya Ofisi na suala zima la utunzaji vifaa na usimamizi wa mazingira katika uhalisia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 14 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Kamati imeelezwa kuwa ongezeko hili linatokana na ajira mpya na kupandishwa vyeo kwa watumishi wa *NEMC*. Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na *NEMC* dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya ulinganisho wa bajeti, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na *NEMC* dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 ili kubaini ongezeko au upungufu wa bajeti ya Ofis ya Makamu wa Rais dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali. Uchambuzi wa Kamati unaonekana kwenye kielelezo Namba Sita na Namba Saba wa ukurasa wa 22 na 23 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati katika vielelzo hivyo umebaini kwamba bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Wakati bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imepungua kwa asilimia 5.4. Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na *NEMC* imepungua kwa asilimia 0.065 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia asilimia 0.057 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni asilimia 0.11 tu ya Bajeti Kuu ya Serikali ya maendeleo. Pungufu hiyo ni sawa na asilimia 0.02 ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha. Pungufu hiyo inaashiria kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira siyo kipaumbele cha Serikali katika mwaka huu wa fedha na kwa kiasi bajeti ya maendeleo ya Taifa mwaka wa fedha 2023/2024 imepunguza utegemezi kutoka nje kwa asilimia 0.04 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza utegemezi wa fedha wa kutoka nje, hata hivyo kiasi hicho ni kidogo, ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaendelea kuongeza fedha za ndani katika bajeti yake ili kuongeza kasi ya uhifadhi, udhibiti na usimamizi endelevu wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Maoni ya Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mapendekezo ya matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ninaomba kubainisha maoni ya Kamati yanayojenga msingi wa ushauri kwa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu na unyeti wa sekta ya mazingira katika maendeleo ya nchi, bado Serikali haijaweka msukumo wa kutosha wa kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta hii. Hali hii inadhihirishwa kwa Serikali kutenga bajeti kidogo kutokana na vyanzo vya ndani na tegemezi kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa fedha ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kunaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa

kutekelezwa na kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa. Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa kudhibiti mazingira, inaathiri ushiriki wao katika utekelezaji wa sera na sheria za mazingira. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Na. 191, Na. 20 ya mwaka 2004 kutoendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kunakwamisha ufikiaji wa malengo ya hifadhi ya mazingira nchini. Jukumu la kukabiliana na kutatua changamoto za mazingira ni mtambuka, hivyo inahitaji mfumo imara, ushirikiano na uratibu baina ya Wizara, Taasisi na wadau mbalimbali wa mazingira ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu kwa sasa mfumo uliopo ni dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuhimiza wananchi, Taasisi za Serikali na wadau mbalimbali kupanda miti, hakuna muongozo unaobainisha aina ya miti inayofaa kupandwa kulingana na mahitaji ya kiikolojia na faida za kiuchumi. Kamati inaipongeza *NEMC* kwa kazi nzuri ya kusimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira nchini. Hata hivyo, utekelezaji wa jukumu hilo unakwamishwa na changamoto za kimuundo na za kisheria zinazolikabili Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kutokana na uchambuzi wa Kamati naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa sera, sheria na bajeti.

(i) Serikali iongeze msukumo wa kutosha katika kuzuia, kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira kwa kuongeza kiwango cha bajeti kinachotokana na vyanzo vya ndani na nje. Ongezeko la bajeti litaiwezesha Serikali kutekeeleza mipango na mikakati iliyopo.

(ii) Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti ya mazingira, ikizingatiwa kuwa mazingira ni uhai. Hivyo ufinyu wa bajeti ya mazingira unaweza kukwamisha maendeleo katika sekta nyingine.

(iii) Serikali iharakishe kuleta Bungeni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Namba 191 ya mwaka 2004, kwa lengo la kuifanyia marekebisho ili iendane na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021na hali halisi ya mazingira ya sasa. Moja ya ahadi ya kutekeleza Ilani ya CCM ya uchambuzi ya 2020 ni kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kampeni ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na upandaji, utunzaji na ukuzaji wa miti 1,500,000 kila mwaka katika Halmashauri ili kuondokana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia utelezaji wa jambo hili na kupata takwimu za idadi ya miti inayopandwa, kutunzwa na kukuzwa hadi sasa. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa agizo lake la kuitaka kila kaya kupanda miti mitatu na kuendelea kuhamasisha wananchi kutekeleza agizo hilo. Kamati inashauri agizo hili la Makamu wa Rais litiliwe mkazo na lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kamati inatoa pongezi za dhati kwa benki ya *NMB* kwa kuunga mkono agizo la Makamu wa Rais la upandaji wa miti nchi nzima ambapo *NMB* watawezesha jumla ya miti 1,000,000 kupandwa nchi nzima. Kamati inawaomba wadau wengine wajitokeze katika zoezi hili na kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa ya kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa changamoto za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kuwa, suala la mazingira ni mtambuka, Serikali iweke mfumo imara na jumuishi utakaowezesha kusimamia na

kuratibu Wizara, Idara na Taasisi zake ambapo shughuli zake zinachangia uhifadhi wa mazingira. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona haja na umuhimu wa kuwa na Kamati ya Mawaziri wa kuratibu masuala mtambuka ndani ya Serikali ikiwemo hili suala la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na wadau wa mazingira Serikali ipanue wigo wa kuongeza kasi ya kutoa elimu ya mazingira kwa umma ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Ili kampeni za upandaji miti nchini iwe na tija na ufanisi unaotarajiwa Serikali iandae mwongozo unaobainisha aina za miti inayotakiwa kupandwa ambayo itakidhi mahitaji ya kiikolojia na faida za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho na utendaji wa *NEMC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utendaji wa Baraza la Taifa la Mazingira Nchini *(NEMC)*, Kamati inaishauri Serikali ianzishe mchakato wa kubadili muundo wa Baraza la Hifadhi ya Mazingira kuwa Mamlaka, mabadiliko hayo yalenge katika kutatua changamoto za kiutendaji, kibajeti, kiutumishi na kimuundo zinazoikabili Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Shukrani. Naomba kuchukua fursa hii tena kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuiliongoza Bunge letu kwa ueledi na umahiri mkubwa, tunakuombea afya njema na umri mrefu katika kutekeleza majukumu yako. Vilevile naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi wao katika kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge letu Tukufu. Kipekee nimshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nenda kwenye hoja mwisho, muda wako umekwisha.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru ninaomba majina yote ya Wajumbe yaingie kwenye *Hansard* iwe Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Baada ya kusema hayo, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadilio ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31, Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 jumla ya Shilingi 25,298,661,900 kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1. Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa Uongozi wako madhubuti, mahiri, makini na

wenye weledi wa kutolea mfano kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa viwango vya juu kabisa ikiwa ni pamoja na kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa mara ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, **Fungu 31** kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023** pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Idara hii kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024**.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano ambazo ni: -

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa Maelezo ya jumla, na kubainisha Msingi na Muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya **Pili** inachambua Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Taarifa za Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya **Tatu**, inaonesha Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Matumizi ya OMRM kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iv) Sehemu ya **Nne,** inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati na

(v) Sehemu ya **Tano**, inahitimisha kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira aliyoitoa mapema leo.

## 1.2. Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ni Masharti ya Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ambapo Kamati hii imepewa jukumu la kuisimamia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

Aidha, Masharti ya Kanuni ya 118 (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, yanaitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ulifanyika tarehe 22 na 23 Machi, 2023.

### 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ina Fungu Moja (**Fungu 31).**

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI
### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inafafanua Uchambuzi wa maeneo matatu yafuatayo, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa

Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, inayotaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Aidha, kabla ya ziara, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha na itakayokaguliwa na Kamati. Baada ya kupokea na kujadili taarifa Kamati ilifanya ziara kwa kutembelea na kukagua Miradi miwili ya Usimamizi wa Mazingira, katika Mkoa wa Tabora. Ufafanuzi wa Miradi iliyotembewa ni kama ifuatavyo:-

### a) Mradi wa Vikundi vya Uzalishaji Mali katika Wilaya ya Nzega.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni miongoni mwa Miradi ya Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame nchini (Reversing Land Degradation and Food Security in Semi Arid Areas – LDFS) ambao unatekelezwa katika Halmashauri za Micheweni (Kaskazini Pemba), Magu (Mwanza), Nzega (Tabora), Mkalama (Singida) na Kondoa (Dodoma). Mradi huu una thamani ya **Dola za Marekani Milioni 7.2** sawa na **Shilingi Bilioni 15.6** kutoka mfuko wa Mazingira Duniani. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, ni miongoni mwa wanufaika wa Mradi huu. Kamati ilipata fursa ya kuukagua Mradi uliyoko Nzega, Kata ya Sigili ikijumuisha Vijiji Vitano vya Sigili, Bulambuka, Bulende, Lyamalagwa na Iboja. Mradi huu kwa Halmashauri ya Nzega unatekelezwa kwa Bajeti ya **Shilingi Bilioni 2.5.** Hadi Februari,

2023 kiasi cha **Shilingi 1,143,008,275.00** kilipokelewa sawa na asilimia **45.7** ya Bajeti iliyotengwa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kunufaisha vikundi vya Ufugaji Nyuki, Ujenzi wa jengo la kukusanya mazao ya nyuki, kuongeza thamani ya mazao kupitia mashine ya kukoboa mpunga, Ujenzi wa jengo la ghala la kuhifadhia mpunga/ mchele na kusimika mashine ya kuchakatia mpunga, Ufugaji wa Kuku chotara na Mashamba darasa ya mazao ya Kilimo. Vikundi hivi vinajumuisha Wanufaika **672,** ambapo kati yao Wanaume ni **449** na Wanawake ni **223.** Vikundi hivi vimeundwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mikutano ya Vijiji.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zinazoambatana na Utekelezaji wa Mradi huu ni pamoja na:-

i) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina usiyo wa kuridhisha. Hadi Kamati ilipotembelea kiasi cha fedha kilichopokewa kilikuwa **asilimia 45.7** tu wakati kwa kipindi hicho ilipaswa kuwa **asilimia 66.6** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo;

ii) Wakandarasi kutolipwa malipo yao kwa wakati;

iii) Kutokuwepo kwa umeme wa uhakika kwenye Makao Makuu ya Halmashauri hali inayochangia malipo kutokufanyika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** katika Kijiji cha Sigili Kamati tukiwa na Mhe. Suleiman Jafo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira tulipata fursa ya kupanda miti ya kumbukumbu ili kuhifadhi mazingira.

**b) Mradi wa Uchimbaji wa Visima Virefu pamoja na Upimaji wa Ujazo wa Maji kwa ajili ya Matumizi ya Kilimo, Binadamu na Mifugo katika Wilaya ya Nzega.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una jumla ya Visima virefu Sita (6) katika Vijiji vya Bulambuka Visima Viwili (2) Bulende Visima Viwili (2), na Lyamalagwa Visima (2) kwa gharama ya **Shilingi 216,546,000.00.** Kazi ya Uchimbaji wa Visima hivi imekalimika katika Vijiji vyote na Mkandarasi amelipwa kiasi cha **Shilingi 194,891,400.00** sawa na **asilimia 90.** Mradi huu unatarajia kunufaisha Wakazi wapatao **2,922** kutoka kwenye **Kaya 487.** Aidha, Kamati ilikagua Kisima chenye Urefu wa Mita 120 na Uwezo wa kutoa Lita 24,800 kwa saa kilichopo katika Kijiji cha Bulambuka Kitongoji cha Mwakasubi/ Sigili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa Miradi hii, hata hivyo, Kamati inaona kuwa ipo haja ya Serikali wakati wa usanifu wa Miradi kuzingatia matumizi ya Wadau wote kwa maana ya matumizi ya kibinadamu (Wakulima na Wafugaji). Aidha, Wananchi washirikishwe kikamilifu ili kuleta tija iliyokusudiwa na kuwawezesha kuilinda kuitunza, kuisimamia na kuifanya kuwa endelevu.

**2.3 Maoni ya Jumla katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo yamebainisha mambo yafuatayo: -

a) Kasi ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya Mradi wa Vikundi vya Uzalishaji Mali hauridhishi kwani hadi mwezi Februari, 2023 kiasi cha fedha kilichopokelewa ni **asilimia 45.7** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi huu. Hali hii inaweza kuathiri Utekelezaji wa Mradi kwa muda uliyokusudiwa na kuongezeka kwa gharama zisizo za lazima. **Ni matarajio ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa kabla ya tarehe 30Juni, 2023 ili kukamilisha Mradi huu muhimu kwa Ustawi wa Wananchi;**

b) Bado kuna haja ya kuendelea kuelimisha Wananchi juu ya manufaa ya kufuga nyuki kwa kujihusisha na utundikaji wa Mizinga. **Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu manufaa ya kufuga nyuki kwa kujihusisha na utundikaji wa Mizinga hali ambayo si tu kwamba itapunguza au kuondoa kabisa ukataji wa miti bali pia itawawezesha Wananchi kufuga nyuki kibiashara.**

c) Ipo haja ya kuwawezesha Wanakikundi katika Kijiji cha Sigili kuchakata na kutafuta masoko ili waweze kunufaika na mradi kuliko kupeleka tena TFS kwa ajili ya masoko. **Serikali iwawezeshe Wanakikundi katika Kijiji cha Sigili kuchakata Asali na kutafuta masoko ili waweze kunufaika na mradi, TFS iwe ni Soko mbadala;**

d) Kumekuwepo na ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi. **Hivyo Kamati inashauri Wakandarasi wanapomaliza kazi yao walipwe mara moja kwa mujibu wa Mikataba ili kuepusha kuongezeka kwa gharama zisizo za lazima;**

e) Matumizi ya Maji katika Miradi hii kutowajumuisha kikamilifu Wafugaji. **Lengo la Miradi hii ni kuwakwamua Wananchi na changamoto ya Maji, hivyo ni rai ya Kamati kwamba Miradi hii iwanufaishe Wananchi wote Wakulima na Wafugaji kama ilivyokusudiwa;**

f) Kuchelewa kwa RUWASA kuanza Utekelezaji wa wazo la Mradi mkubwa wa kuweka miundombinu ya usambazaji wa maji ya Visima kutokana na Mradi kuhitaji fedha nyingi. **Kamati inashauri RUWASA kuanza na visima ambavyo havitagharimu fedha nyingi ili Wananchi waweze kuanza kupata huduma ya maji na mradi uweze kutoa matunda ndani ya muda uliowekwa (Project Period). Aidha, Maji haya yasambazwe kwenye Taasisi zote za Serikali ikiwemo Shule ambako**

**Wanafunzi wanapaswa kupewa miti ya kupanda na kuimwagilia;**

g) Kamati inashauri agizo la Makamu wa Rais la kila Kaya kupanda miti mitatu litiliwe mkazo;

h) Miradi hii imekuwa ikitengewa Fedha za ndani na Fedha za nje, Kamati inasikitika kuona kuwa kiasi cha Fedha za ndani kinachotengwa ni kidogo sana (Aslimia 4 tu), na hata hicho kidogo utolewaji wake ni wa kusuasua. **Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kuongeza kiwango cha Fedha za ndani na kuhakikisha kuwa kiasi kinachotengwa kinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili utekelezaji wa Miradi uwe kwa wakati na endelevu.**

**2.4 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Lengo ni kufanya ulinganisho kati ya Utekelezaji wa Bajeti unaoripotiwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo sehemu hii inaripoti mambo yafuatayo: -

a) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika bajeti ya 2022/2023;

b) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na OMRM.

### 2.4.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya OMRM, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitoa Ushauri katika maeneo matatu (3). Napenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia kwa kiasi kikubwa Ushauri wa Kamati. Mfano wa Ushauri uliozingatiwa unahusu **kumalizia mchakato wa kutafsiri Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kwa Lugha ya Kiswahili. Hatua hii itawezesha Wananchi kuielewa zaidi Sera hii na kuanza utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo. Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa kazi ya kutafsiri Sera ya Taifa ya Mazingira imekamilika na nakala kusambazwa kwa walengwa ikiwemo Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kote.**

Aidha, katika kusimamia utekelezaji wa Sera hii Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira wa miaka Kumi (2022-2032) ambapo pamoja na mambo mengine unatoa fursa ya elimu kwa Wadau, fursa ya kuandaa maandiko ya Miradi itakayochangia katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa kwenye Sera na fursa za upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali Watu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya Ushauri uliotolewa, ni rai ya Kamati kwamba Serikali iendelee kutekeleza kikamilifu na kwa haraka maeneo ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango cha chini. **Mfano wa Ushauri huo ni uharakishwaji wa mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191. Kwa**

**Maoni ya Kamati, uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati kikamilifu unawezesha Serikali kukidhi matarajio ya Wananchi**.

## 2.4 2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31** iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 26,732,352,530.00.** Kati ya fedha hizo Shilingi **7,590,655,530.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **19,141,697,000.00** sawa na **asilimia 72** ni za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha **Shilingi 936,225,000.00** fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, **Shilingi 4,362,627,730.00** Mishahara ya NEMC na **Shilingi 2,291,802,800.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kwa Idara ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari 2023, OMRM ilipokea jumla **ya Shilingi 21,307,949,874.43** sawa na **asilimia 80** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, kati ya Fedha hizo **Shilingi 5,027,304,429.43 sawa na asilimia 23.6** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **16,280,645,445.00** sawa na **asilimia 76.4** ya kiasi cha fedha kilichopokelewa ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge na fedha zilizopokelewa na matokeo ya Uchambuzi huo unaonekana katika **Kielelezo Na.1**

**KIELELEZO NA 1: Mchanganuo wa Bajeti iliyodhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2023 kwa ajili ya kuhifadhi na Kusimamia Mazingira**

| UFAFANUZI | KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA | % YA BAJETI ya OMRM | KIASI CHA FEDHA KILICHOPOKELEWA | % YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | **7,590,655,530.00** | 28 | **5,027,304,429.43** | **66.2** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **19,141,697,000.00** | 72 | 16,280,645,445.00 | **85** |
| **Jumla** | **26,732,352,530.00.** | 100 | 21,307,949,874.43 | **80** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**KIELELEZO NA 2: Mchanganuo wa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichoidhinishwa, kupokelewa na kutumika hadi Februari, 2023**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | MCHANGANUO | KIASI CHA FEDHA ZILIZOIDHINISHWA | KIASI CHA FEDHA ZILIZOPOKELEWA | %YA BAJETI ILIYOPOKELEWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | % YA FEDHA ZILIZOTUMIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MISHAHARA MAZINGIRA** | 936,225,000 | 513,325,999.84 | 54.8 | 356,692,000.00 | 9.5 |
| | **MISHAHARA NEMC** | 4,362,627,730.00 | 3,241,119,728.00 | 74.3 | 3,241,119,728.00 | 00 |
| | **OC** | 2,291,802,800.00 | 1,272,858,701.59 | 55.5 | 1,212,711,750.30 | 6 |
| **JUMLA** | | **7,590,655,530.00** | **5,027,304,429.43** | **66.2** | **4,810,523,478.30** | **5.7** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**KIELELEZO NA 3: Mchanganuo wa kiasi cha fedha za Matumizi ya Maendeleo kilichoidhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2023**

| MCHANGANUO | KIASI KILICHOI-DHINISHWA | % YA BAJETI YA MAENDELEO | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA YA BAJETI ILIYOTENGWA |
|---|---|---|---|---|
| Fedha za ndani | 782,000,000.00 | **4** | **662,089,448** | **85** |
| Fedha za nje | 18,359,697,000.00 | 96 | 15,618,555,997.00 | 85.1 |
| **JUMLA** | **19,141,697,000.00** | **100** | **16,280,645,445.00** | **85** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti katika **Kielelezo Na. 1 hadi 3** unaonesha kuwa:-

a) Kwa ujumla upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya shughuli za kusimamia na kudhibiti Mazingira ni wa kuridhisha. Hadi mwezi Februari, 2023 fedha iliyopokelewa ni **asilimia 80** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Upatikanaji huo wa fedha katika kipindi hicho unakidhi matarajio ya Bunge kuhusu matumizi kwa ajili ya udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

b) Fedha zilizopatikana kwa ajili Matumizi ya Kawaida ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira hadi kufikia mwezi Februari 2023, ni asilimia **66.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Upatikanaji huo wa fedha unatoa tafsiri kwamba, uendeshaji wa shughuli za usimamizi, udhibiti na uhifadhi wa mazingira kwa kiasi umeendana na matarajio yaliyokusudiwa;

c) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayolenga kuimarisha Udhibiti, Uhifadhi na

Usimamizi wa Mazingira ulifikia asilimia **85** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2023;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati na hivyo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 Uk. 285 ya kuendelea kukabiliana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Ni rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni ili Miradi iweze kukamilika kwa asilimia 100. Aidha, ni matarajio ya Kamati kuwa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha 2022/2023 utafaa kutumika katika upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ili miradi itakayokuwa imepangwa kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

### 2.5 Utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha **2022/2023** ilikusudia kufanikisha Utekelezaji wa Mipango na Majukumu 7 ya Idara ya Mazingira na NEMC.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi zote zilizopangwa zimeripotiwa kutekelezwa. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha yafuatayo: -

a) Kasi ya utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inapaswa kuongezwa ili kuleta tija na;

b) Utekelezaji wa Kampeni za Upandaji na Utunzaji wa Miti, hususani katika maeneo ambayo yameathirika sana na ukame, hauzingatii aina ya miti inayoendana na eneo husika. Hali hii, inasababisha matokeo ya Kampeni kutokuwa na tija iliyokudiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA NA NEMC KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo/Mpango

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Malengo pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024**, vinaendana na majukumu ya Msingi, ikiwemo kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Kwa mfano, jukumu la **Kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Sura 191 kwa kufanya kaguzi, na ufuatiliaji katika Migodi, Viwanda na Miradi mbalimbali inayotekelezwa nchini ili kulinda na kutunza mazingira** na jukumu la **Kutoa elimu kwa Umma na Wadau mbalimbali kuhusu masuala ya mazingira,** yanaendana na majukumu ya Msingi ya Idara ya Mazingira. Aidha, Majukumu hayo yanaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 kama ilivyofafanuliwa katika Aya ya 235 (g) (i), Ukurasa wa 285 wa Ilani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilijiridhisha kwa kuangalia Malengo ya Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia (*Sustainable Development Goals*) ambapo ajenda ya **Mazingira ni ya 13 kati ya Malengo 17 ya SDG's (2030)**. Katika lengo namba 13 linalosomeka kama ***Climate Action*** ambayo ndani yake ina malengo matano yafuatayo;

a) Kuimarisha ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na hatari zinazohusiana na hali ya hewa na majanga ya asili katika nchi zote;

b) Kujumuisha hatua za mabadiliko ya tabianchi katika Sera, Mikakati na Mipango ya Kitaifa;

c) Kuboresha Mipango na Mikakati ya utoaji elimu, uhamasishaji na kujenga uwezo wa kibinadamu na kitaasisi juu ya kuhimili na kukabiliana athari za na mabadiliko ya tabianchi.

d) Kuimarisha uwezo wa upangaji na usimamizi bora, unaohusiana na mabadiliko ya tabianchi katika nchi zilizoendelea sambamba na nchi za Visiwa kidogo kwa kuzingatia ushiriki wa Wanawake, Vijana, Jumuiya za Mitaa na Jumuiya zilizotengwa.

**Kamati inaipongeza Idara ya Mazingira kwa kuzingatia kikamilifu Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia *SDG's* (2030) pamoja na Ilani ya CCM katika Utekelezaji wa Majukumu yake. Hata hivyo, bado yapo maeneo machache yanayohitaji kufanyiwa kazi. Miongoni mwa maeneo hayo ni kuanzisha maeneo lindwa ya Mazingira (Environmental Protected Areas) ili kuokoa na kuhifadhi maeneo muhimu ya kimazingira.**

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya jumla ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31)**, Idara ya Mazingira na NEMC inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **25,298,661,900.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Uchanganuzi wa Makadirio hayo unabainishwa kwenye **Kielelezo Na.4.**

**KIELELEZO NA 4: Mchanganuo wa Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara na NEMC kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| MCHANGANUO | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA | | ASILIMIA YA BAJETI YOTE |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | Mishahara Idara ya Mazingira | **860,668,000.00** | 3.4 |
| | OC - Idara ya Mazingira | **2,517,500,900.00** | 10 |
| | Mishahara NEMC | **5,264,448,000.00** | 20.8 |
| **JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA** | | **8,642,616,900** | **34.2** |
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | Fedha za Ndani | **1,600,000,000.00** | 10 |
| | Fedha za Nje | **15,056,045,000.00** | 90 |
| **JUMLA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | **16,656,045,000.00** | **65.8** |
| **JUMLA BAJETI YOTE** | | **25,298,661,900.00** | **100** |

**Chanzo:** Randama Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

a) Kwa ujumla Bajeti ya OMRM inayoombwa kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti Mazingira ni ndogo;

b) Bajeti ya OMRM, inayoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni tegemezi kwa **asilimia 90,** Fedha ya ndani

iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 10** tu. Takwimu hizi zinaashiria kwamba bado Serikali haijaweka msukumo unaostahili katika suala zima la Mazingira ambalo ni agenda kuu ya dunia na ndio mstakabali wa maisha ya viumbe hai kwenye uso wa dunia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika Utekelezaji wa Bajeti inayoisha, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kupatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mchanganuo na ulinganisho uliofanyika unaonekana katika **Kielelezo Na. 5.**

**KIELELEZO NA 5: Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ikilinganishwa na maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| FEDHA | AINA YA MATUMIZI | FEDHA ILIYOIDHINISHWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | FEDHA INAYOOMBWA KWA MWAKA 2023/2024 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **KAWAIDA** | **Mishahara - Mazingira** | 936,225,000.00 | 860,668,000.00 | 75,557,000.00 | **(8)** |
| | **OC-Mazingira** | **2,291,802,800.00** | 2,517,500,900.00 | **225,698,100.00** | **10** |
| | **Mishahara -NEMC** | **4,362,627,730.00** | 5,264,448,000.00 | **901,820,270.00** | **21** |
| **Jumla Ndogo** | | 7,590,655,530.00 | 8,642,616,900.00 | 1,051,961,370.00 | **14** |
| **MAENDELEO** | **Ndani** | 782,000,000.00 | 1,600,000,000.0 | 818,000,000.00 | **105** |
| | **Nje** | 18,359,597,000.00 | 15,056,045,000.00 | 15,788,909,000.00 | **(3.3)** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla Ndogo** | | 19,141,697,000.00 | 16,656,045,000 | (2,485,652,000.00) | **(13)** |
| **JUMLA KUU** | | 26,732,352,530.00 | 25,298,661,900.00 | (1,433,690,630.00) | **(5.4)** |

**Chanzo**: Randama ya Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira na NEMC ya 2022/2023 na 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizi zinaonesha kuwa: -
a) Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na NEMC kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepungua kwa **asilimia 5.4** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Pamoja na Kamati kuelezwa kuwa fedha nyingine zimepelekwa kwenye Idara na Taasisi nyingine kwa suala la mazingira, **Kamati bado ina wasiwasi kuwa hali hii ya kupungua kwa bajeti inaashiria kwamba msukumo wa Utekelezaji wa shughuli za Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira umepungua ikilinganishwa na mpango wa Mwaka unaoisha;**

b) Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepungua kwa **asilimia 13** ikilinganishwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa kiasi cha **Shilingi 2,485,652,000.00. Uchambuzi huu unabainisha kuwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaweza kuathirika kwa kiasi fulani;**

c) Fedha za Ndani zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 105** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati inapongeza juhudi za Serikali kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, **Kamati inaona kiasi hicho cha fedha ni kidogo ikilinganishwa na majukumu makubwa ya Ofisi hii na suala zima la Utunzaji, Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika uhalisia wake;**
d) Bajeti ya Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 14** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha unaoisha. Kamati

ilielezwa kuwa ongezeko hilo limetokana na Ajira mpya na kupandishwa vyeo kwa Watumishi wa NEMC.

### 3.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na NEMC dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na NEMC dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 ili kubaini ongezeko/ pungufu la Bajeti ya OMRM dhidi ya Bajeti ya Taifa. Uchambuzi wa Kamati unaonekana kwenye Kielelezo **Na.6 na 7.**

**KIELELEZO NA 6&7: Ulinganisho wa Bajeti ya OMRM dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali**

| **KIELELEZO NA. 6 ULINGANISHO WA BAJETI YA OMR- MAZINGIRA DHIDI YA BAJETI KUU YA SERIKALI 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| **MCHANGANUO** | **BAJETI KUU YA SERIKALI** | **BAJETI OMR-MAZINGIRA** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000,000.00 | 2,291,802,800.00 | 0.051 |
| MISHAHARA | 9,740,800,000,000.00 | 936,225,000.00 | 0.010 |
| MAENDELEO NDANI | 12,122,100,000,000.00 | 782,000,000.00 | 0.006 |
| MAENDELEO NJE | 3,399,200,000,000.00 | 18,359,697,000 | 0.54 |
| **JUMLA MAENDELEO** | **15,006,002,000,000.00** | **19,141,697,000.00** | **0.13** |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | | - |
| **NEMC** | - | **4,362,627,730.00** | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **26,732,352,530.00** | **0.065** |

**Chanzo:** Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na Randama ya OMRM 2022/2023.

| KIELELEZO NA. 7 ULINGANISHO WA BAJETI YA OMRM DHIDI YA BAJETI BAJETI KUU YA SERIKALI 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **MCHANGANUO** | **BAJETI KUU YA SERIKALI** | **BAJETI MAZINGIRA** | **ASILIMIA** |
| OC | 6,396,900,000.00 | 2,517,500,900.00 | 0.045 |
| MISHAHARA | 10,882,126,000,000.00 | 860,668,000.00 | 0.008 |
| DENI LA SERIKALI | 12,771,533,000,000.0 | - | |
| NEMC | - | 5,264,448,000.00 | - |
| **JUMLA NDOGO** | **29,232,100,000,000.00** | **8,642,616,900.00** | **0.03** |
| MAENDELEO NDANI | 11,873,894,000,000 | 1,600,000,000.00 | 0.013 |
| MAENDELEO NJE | 3,282,081,000,000 | 15,056,045,000.00 | 0.5 |
| **JUMLA NDOGO MAENDELEO** | **15,155,975,000,000.00** | **16,656,045,000.00** | **0.11** |
| **JUMLA KUU** | **44,388,067,000,000.00** | **25,298,661,900.00** | **0.057** |

**Chanzo:** Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Randama ya OMRM 2023/20234

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

a) Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 8.1** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, wakati Bajeti ya OMRM imepungua kwa **asilimia 5.4;**

b) Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na NEMC imepungua kutoka **asilimia 0.065** kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 0.057** kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali;

c) Bajeti ya Maendeleo ya OMRM ni **asilimia 0.11** tu ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo. Pungufu hiyo ni sawa na **asilimia 0.02** ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha

unaoisha. Pungufu hiyo inaashiria kwamba OMRM siyo kipaumbele cha Serikali katika mwaka huu wa fedha na;

d) Kwa Kiasi Bajeti ya Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepunguza utegemezi kutoka nje kwa **asilimia 0.04** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/2023. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza utegemezi wa fedha kutoka nje. Hata hivyo kiasi hicho ni kidogo. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaendelea kuongeza fedha za ndani katika Bajeti yake ili kuongeza kasi ya udhibiti, Uhifadhi na Usimamizi endelevu wa Mazingira nchini.**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Fungu 31-Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Mapendekezo ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naomba kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga Msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

a) Kutokana na umuhimu na unyeti wa Sekta ya Mazingira katika maendeleo ya nchi, bado Serikali haijaweka msukumo wa kutosha wa kukabiliana na changamoto zinazoikabili Sekta hii. Hali hii inadhihirishwa na Serikali kutenga Bajeti ndogo kutokana na vyanzo vya ndani na tegemezi kwa kiasi kikubwa kutoka kwa Wahisani na Washirika wa Maendeleo;

b) Kupungua kwa fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kunaweza kuathiri utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa na kushindwa kufikia Malengo yaliyopangwa;

c) Uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu umuhimu wa Kuhifadhi, Mazingira unathiri ushiriki wao katika utekelezaji wa Sera na Sheria za Mazingira;

d) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 Na. 20 ya mwaka 2004 kutoendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kunakwamisha ufikiaji wa Malengo ya Hifadhi ya Mazingira nchini;

e) Jukumu la kukabiliana na kutatua changamoto za Mazingira ni mtambuka, hivyo linahitaji Mfumo imara wa ushirikiano na uratibu baina ya Wizara, Taasisi na Wadau mbalimbali wa Mazingira ili kufikia Malengo ya Maendeleo endelevu. Kwa sasa Mfumo uliopo ni dhaifu.

f) Pamoja na jitihada za Serikali za kuhimiza Wananchi, Taasisi za Serikali na Wadau mbalimbali kupanda miti hakuna Mwongozo unaobainisha aina ya miti inayofaa kupandwa kulingana na mahitaji ya Kiikolojia na faida za Kiuchumi;

g) Kamati inaipongeza NEMC kwa kazi nzuri ya kusimamia na kutoa Ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la Hifadhi ya Mazingira nchini. Hata hivyo, utekelezaji wa jukumu hilo unakwamishwa na changamoto za Kimuundo na Kisheria zinazolikabili Baraza.

### 4.2 Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Uchambuzi wa Kamati naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 4.2.1 Utekelezaji wa Sera, Sheria na Bajeti

a) Serikali iongeze msukumo wa kutosha katika kuzuia na kukabiliana na changamoto za uharibifu wa Mazingira kwa kuongeza kiwango cha Bajeti kutokana na vyanzo vya ndani na nje. Ongezeko la Bajeti litaiwezesha Serikali kutekeleza Mipango na Mikakati iliyopo;

b) Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Mazingira ikizingatiwa kuwa Mazingira ni Uhai. Hivyo ufinyu wa Bajeti ya Mazingira unaweza kukwamisha maendeleo katika Sekta zingine. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba kiasi cha Bajeti kinachoidhinishwa na Bunge kitolewe kikamilifu na kwa wakati ili kutokuathiri utekelezaji wa Mipango na Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka huu wa Fedha 2023/2024;

c) Serikali iharakishe kuleta Bungeni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ya mwaka 2004 kwa lengo la kuifanyia Marekebisho ili iendane na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na hali halisi ya Mazingira ya sasa;

d) Moja ya ahadi katika kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2020 ni Kuboresha utekelezaji wa Mikakati ya Kampeni za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza Mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na upandaji, utunzaji na ukuzaji miti milioni 1.5 kila mwaka katika Halmashauri ili kuondokana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia utekelezaji wa jambo hili na kupata takwimu za idadi ya miti iliyopandwa kutunzwa na kukuzwa hadi sasa.

Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa agizo lake la kuitaka Kila Kaya kupanda miti mitatu na kuendelea kuhamasisha Wananchi kutekeleza agizo hilo. **Kamati inashauri**

**agizo hilo la Makamu wa Rais litiliwe mkazo na lizingatiwe**. Sambamba na utekelezaji wa agizo hilo Kamati pia inaishauri Serikali kuanza utekelezaji wa pendekezo la Mhe Makamu wa Rais alilolitoa Mkoani Kagera mwaka 2022 kwenye kilele cha mbio za Mwengu wa Uhuru. Wakati wa sherehe hizo Mhe Makamu wa Rais alipendekeza kwamba Suala la Mazingira liwe miongoni mwa Agenda za Mbio za Mwenge za kila mwaka.

Aidha, Kamati inatoa Pongezi za dhati kwa Benki ya NMB kwa kuunga mkono agizo la Makamu wa Rais la upandaji wa miti nchi nzima ambapo NMB watawezesha jumla ya miti Milioni Moja kupandwa nchi nzima. Kamati inawaomba wadau wengine wajitokeze katika zoezi hili na kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa ya kijani.

**4.2.2 Utatuzi wa changamoto za Kimazingira na Mabadiliko ya tabianchi**

a) Kwa kuwa suala la Mazingira ni mtambuka Serikali iweke Mfumo imara na Jumuishi utakaoiwezesha kusimamia na kuratibu Wizara, Idara na Taasisi zake ambazo shughuli zake zinachangia uhifadhi wa Mazingira. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona haja na umuhimu wa kuwa na Kamati ya Mawaziri ya kuratibu masuala mtambuka ndani ya Serikali likiwemo hili suala la Mazingira. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais haraka iwezekanavyo;

b) Kwa kushirikiana na Wadau wa Mazingira Serikali ipanue wigo na kuongeza kasi ya kutoa Elimu ya Mazingira kwa Umma ili Wananchi waweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za Udhibiti, Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira;

c) Ili Kampeni ya upandaji miti nchini iwe na tija na ufanisi unaotarajiwa, Serikali iandae Mwongozo utakaobainisha aina ya miti itakayopandwa ambayo itakidhi mahitaji ya Kiikolojia na faida za Kiuchumi.

### 4.2.3 Maboresho ya Utendaji wa NEMC

Ili kuboresha Utendaji wa Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC), Kamati inaishauri Serikali ianzishe mchakato wa kubadili Muundo wa Baraza la Hifadhi ya Mazingira kuwa Mamlaka. Mabadiliko hayo yalenge katika kutatua changamoto za Kiutendaji, kibajeti, kiutumishi na kimuundo zinazolikabili Baraza kwa sasa. Aidha, mapendekezo haya yamezingatia uzoefu wa Taasisi za aina hii katika nchi nyingine.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii tena kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi na Umahiri mkubwa. Tunakuombea afya njema na Umri mrefu katika kutekeleza majukumu yako. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa weledi wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Anna Richard Lupembe Mb, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati, hususan wakati wa kutembelea, kukagua, kujadili na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na hatimaye kuandaa na

kukamilisha taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb _ **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb _ Mjumbe
4. Mhe. Prof. Shukran Elisha Manya, Mb _ "
5. Mhe. Bashiru Ally Kakurwa, Mb _ "
6. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb _ "
7. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb _ "
8. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb _ "
9. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb _ "
10. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb _ "
11. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb _ "
12. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb _ "
13. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb _ "
14. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb _ "
15. Mhe. Charles John Mwijage, Mb _ "
16. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb _ "
17. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb_ "
18. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb _ "
19. Mhe. Keneth Nollo, Mb _ "
20. Mhe. Joseph Kasheku Msukuma, Mb _ "
21. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb _ "

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira Mhe. Selemani Jafo, Mb. na Naibu Waziri wake Mhe. Khamis H. Khamis Mb, Katibu Mkuu Ndg. Mary Ngelela Maganga, Naibu Katibu Ndg. Edwin Gerald Nyamanga pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa vikao na uchambuzi wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi *ndc*, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndg. Michael Chikokoto *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi

Ndg.Gerald Magili na Msaidizi wa Kamati Bi. Modesta Kipiko kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kipekee ninawashukuru Makatibu wetu wa Kamati Ndg. Angelina Langisi Sanga na Ndg. Nyamwanja Chipanda Chilemeji kwa kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa hii inawasilishwa kwa wakati.

**5.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31) – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024** jumla Shilingi **25,298,661,900.00.00** kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono **hoja.**

Jackson Gedion Kiswaga, Mb,
**MWENYEKITI, KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA,**
24 Aprili, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye michango. Tunaanza na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, ajiandae Mheshimiwa Cosato David Chumi, ajiandae Mheshimiwa Esther Edwin Malleko. King hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza katika siku hii ya leo. Napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ambayo

inaendelea kufanywa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, pia kwa sababu mimi ni mwanamichezo napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Simba na Yanga kwa ushindi walioupata *weekend* hii katika michezo yao ya robo fainali na tunawaombea katika mechi zijazo waweze kushinda ili kusudi Taifa letu liweze kuingia katika hatua ya nusu fainali ambayo itakuwa rekodi kwa Taifa letu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba nijielekeze kwenye hoja. Mimi nina mambo kama matatu hivi. Kwanza, kumekuwa na jitihada kubwa sana za kuhamasisha upandaji wa miti, ni jambo jema na jambo zuri lakini lazima ifike wakati tujiulize je, kupanda huku kunaendana na utunzaji? Kweli tumeweka malengo ya kupanda nadhani miti 1,000,000 kwa kila Halmashauri, tunapanda vizuri sawa lakini je, miti mingapi inapona? Kwa hiyo pamoja na kupanda tujielekeze pia katika utunzaji wa miti hii ili tusije tu tukawa na takwimu za kwamba tumepanda miti kadhaa lakini miti ambayo inaendelea kuishi na kuwepo kwa nia ya kutunza mazingira inakuwa ni michache. Kwa hiyo, nguvu zielekezwe kwenye kupanda lakini pia na kwenye kutunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ninalopenda kuchangia ni kwa namna gani kama Taifa tumejipanga kunufaika na Mifuko ya Umoja wa Mataifa ambayo ina jukumu la kusaidia nchi maskini kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru na napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais katika mkutano wa mazingira kule *Scotland – Glasgow,* alikuwa jasiri na aliyaeleza mataifa makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa yana mchango mkubwa katika kuharibu mazingira na kuchangia madhara haya ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuahidi kuchangia ile mifuko takribani Dola Bilioni Mia Moja ambayo fedha hizi zitasaidia nchi maskini ambazo kimsingi hazichangii sana mabadiliko ya tabianchi, hazichangii sana kuharibika kwa mazingira, sasa hizi nchi kubwa zinao wajibu wa kuzi–*support* hizi nchi ndogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alikuwa jasiri na aliyaambia Mataifa makubwa kwamba pamoja na ahadi zenu ifike wakati muweze kuheshimu ahadi zenu na kutoa hizi fedha. Sasa kama Taifa tumejipangaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara na Serikali walikuja na huo mwongozo pamoja na kanuni za udhibiti na usimamizi wa biashara ya *carbon* au hiyo tunaiita hewa ya ukaa. Mifuko hii iko mingi na katika Mkutano wa mwaka jana maarufu kama *COP27* kumeanzishwa Mfuko unaitwa *Loss and Damage Fund*. Mfuko huu malengo yake ni kusaidia katika kutibu majanga mbalimbali ambayo nchi hizi maskini zinapata kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu na hoja yangu kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Serikali kwa ujumla, tumejipangaje katika kuhakikisha kwamba tunanufaika na fedha hizo na tunaweza kukabiliana na majanga yanapotokea. Kwa mfano, jambo la muhimu la kwanza sana inatakiwa lazima uwe na orodha ya majanga yanayotokea katika Taifa lako ili mfuko ule utakapoanza kutekelezwa basi walau unapoenda kuwasilisha yale maombi tayari unakuwa na ile orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, pamoja na Kanuni hizi, natumia nafasi hii kuwapongeza sana Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania walifadhili Halmashauri ya Mji wa Mafinga tukaenda kujifunza kule Wilaya ya Tanganyika kwa Mheshimiwa Kakoso. Wenzetu wamepiga hatua sana. Nimeona Serikali Mheshimiwa Jafo amesema kufikia 2024 Januari, hakutakuwa na matumizi ya mkaa kwa Taasisi za Umma na Binafsi ambazo zinahudumia watu kuanzia mia

moja. Je, kama Taifa tumejipangaje katika kutumia nishati mbadala?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mafinga tunavyo viwanda vya mkaa ambao unatokana na mabaki yanayotokana na uzalishaji wa mazao ya misitu. Sasa yale mabaki ni kwamba tungeweza kuyachoma kwa kuyachoma maana yake tungeendelea kuharibu mazingira, sasa viwanda kama hivi vilikuwa vitatu,viwili vimeshafungwa, kimoja kinaendelea lakini hata hiki kimoja mkaa kinauza nje ya nchi kwa sababu hapa nchini hawawezi kuuza kwa sababu bei inakuwa ni kubwa kutokana na mazingira yale ya uwekezaji siyo rafiki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia Mheshimiwa Waziri Mkuu alipiga marufuku matumizi ya kamba hizi za *nylon,* kwamba ili tuweze kufufua zao la mkonge, tuweze kutengeneza ajira lakini kwa ajili hiyo ya kulinda mazingira tupige marufuku uingizaji wa kamba za *plastic* lakini kamba bado pia zinaingia. Je, tunajipangeje katika haya yote, kwa mfano kuhakikisha kwamba hawa watu wanaozalisha nishati mbadala kama nilivyosema viwanda hivi vya Mafinga, tunaviwekea mazingira gani ili vizalishe ule mkaa ambao kama mtu hana uwezo wa kugharamia gesi basi aweze kuwa na ule mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, watu wa Mufindi, Iringa na Njombe tumepanda miti kwa wingi, niliposoma kanuni sijui kama nimeelewa vizuri na kwa kuwa inawezekana hata mimi Mwakilishi naweza nikawa sijaelewa vizuri, nilikuwa naiomba Wizara iwe na mpango mkakati maalum, waje watuletee elimu na kutuwezesha kufahamu je, hata hii miti ya kupanda nayo tunanufaika katika hii biashara ya hewa ya ukaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru kwa kunipa nafasi na Mungu atubariki wote na awabariki Simba na Yanga katika mechi zijazo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa tunampa nafasi Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, jiandae Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, jiandae Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja subiri. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko nilishamuita halafu utakuja wewe. Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii nyeti na muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nipeleke pongezi zangu za dhati kwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Najua jukumu la kutunza mazingira ni la nchi nzima, lakini ninasikitika sana, hata Wenyeviti wanapokuwa wanasoma taarifa zao za bajeti hapo, inaonekana bajeti ni finyu sana katika Wizara hii. Tujiulize, Wizara hii ndiyo imebeba Wizara nyingine zote. Bila kuwa na mazingira safi, bila kuwa na kutunza mazingira ya nchi hii, hivi vitu vingine vyote haviwezi kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona katika mlima wetu wa Kilimanjaro moto unatokea sana, ni uharibifu wa mazingira. Tunaona Serikali inatumia fedha nyingi katika kuzima moto huo, lakini siyo hivyo tu, hata watu wanakufa wakati wa

kuzima moto, na Serikali inapata hasara kubwa sana. Je, imejipanga vipi sasa kuweza kukabiliana na masuala yote hayo kama bajeti inakuwa ni finyu kiasi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kuangalia suala hili kwa umakini, kwa sababu, bila kutunza mazingira hatuwezi kufanya jambo lolote. Tukumbuke kwamba, hii dunia ni kama nyumba, na jinsi tunavyozidi kuiharibu, iko siku itatuangukia, nasi sote tutakuwa tumeangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu uharibifu wa mazingira umekuwa ni mkubwa sana. Ninasema tena kwa sababu ya moto unaowaka Mlima Kilimanjaro na uharibifu mkubwa wa mlima ule tunaona hata kiwango cha barafu kinazidi kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipangaje sasa katika kuona namna ya kutoa elimu kwa wale wananchi wetu wa kule chini ambao ndio wahusika wakubwa kabisa wanaohitaji kupewa elimu hii ili waweze kutunza mazingira? Wao ndio wanapaswa kuambiwa ni namna gani watatunza mazingira, ni njia gani mbadala wanazoweza kutumia ili wasiharibu mazingira kwa kukata miti ovyo, lakini elimu kule chini bado haijafika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naishauri Serikali, leo tunaweza kuuza hewa ya *carbon*. Ni kwa nini basi Serikali isijikite kwenda kutoa mafunzo na elimu kwa hawa watu wa chini kwenye Serikali za Mitaa ili waweze kujua umuhimu wa kutunza mazingira, na zaidi ni namna gani wanaweza kufaidika kwa kuuza hewa hiyo ya *carbon? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika andiko moja ambalo linasema, Wilaya ya Tanganyika kuna vijiji nane

vimepata takribani Shilingi milioni 380 kwa uuzaji wa hewa hii ya *carbon*. Kwa nini basi Serikali isione jambo hili ni la muhimu tukaweza kushirikiana na Halmashauri na wengine sasa wakapata hiyo elimu na namna gani wanaweza kupanda hiyo miti na zaidi ya hapo tukaweza kuvuna hiyo hewa na kuiuza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijikite kwenye suala la uzimamizi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira. Kama nchi, katika eneo hili tumefeli sana. Tanzania kwa mwaka mmoja inazalisha taka ngumu takribani tani milioni saba, lakini cha kusikitisha kiasi kinachoweza kukusanywa, yaani kuzolewa, ni asilimia 35 tu. Hebu tujiulize tunaishije kwenye mazingira kama haya ambayo taka kama hizo nyingine zote zimebaki, hazijapata ufumbuzi wa namna gani zinaweza kukusanywa na kuzolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kukicha majiji na miji yanakua, ongezeko la watu mjini linakua, viwanda na biashara na kazi nyingine za kuingizia wadamu kipato zinakua, lakini suala la kuzoa taka na kudhibiti taka bado limekuwa ni changamoto kubwa sana. Ninaishauri Serikali, kutokana na sababu hizi kubwa ambazo zinaonekana zinaenda kutuletea shida katika majiji yetu na Halmashauri zetu, Serikali ione ni namna gani basi itaongeza bajeti kwenye Wizara hii ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo, asilimia 30.7 ya utupaji taka nchini ni holela. Watu wanatupa taka kwa maeneo ambayo hayajatengwa. Unaweza mnaweza kuona, hata mnapopita kwenye mifereji au mito imekuwa ndiyo sehemu ya watu kutupa taka. Mvua inaponyesha, yale matakataka yanakuwa yanaziba mifereji ya maji na baadaye kunatokea mafuriko na baadaye tunapata kipindupindu. Hili ni jambo la kulifanyia kazi. Siyo hivyo tu, asilimia 38.4 ya maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kutupa taka, lakini miundombinu

yake haikidhi utupaji taka. Kwa hiyo, hili ni jambo la kulitazama kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya utupati taka, ni asilimia 27.8, lakini hayahudumiwi. Ni kwa nini yatengwe lakini yasihudumiwe? Ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Lakini leo tunasema asilimia 5.3 ya utupaji taka nchini ndiyo inahusisha utupati taka salama. Tunakwenda wapi kama asilimia hiyo yote ni sawa na asilimia 90 ya utupaji taka katika nchi yetu siyo salama? Kwa hiyo, tunawezaje kukwepa kupata kipindupindu na magonjwa mengine ya mlipuko? Hivyo naomba sana Wizara hii iweze kuongezewa bajeti ili iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Halmashauri nyingi hazioni umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya suala hili na ukusanyaji na utupaji wa taka. Mimi ninaishi hapa Mlimwa C, hapa hapa Dodoma, nitolee mfano hapa. Tunaweza kukaa na taka ndani zaidi ya wiki mbili bila kuja kuzolewa, lakini wanapokuja kuzoa, gari linalokuja kuzoa zile taka na lenyewe ni takataka. Hata wale wanaokuja kuzoa taka ukiwaangalia, hawana hata vifaa vya kuwakinga kwa zile taka wanazokuja kuzibeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tujiulize, tunakwenda wapi kama Taifa? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili, ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, jiandae Mheshimiwa Simai Hassan na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuamsha asubuhi hii ya leo tukaweza kuja kujadili bajeti hii muhimu kwa nchi na kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kupongeza Wizara zote mbili ambazo zinahusika na mambo mawili haya ya Muungano na Mazingira. Nikiendelea, kwanza napenda kuwapongeza wananchi wa Tanzania kwamba, keshokutwa tu tunatimiza miaka 59 ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Muungano ambao umeleta sura na nuru ya Taifa letu katika dunia nzima. Ni Muungano wa kupigiwa mfano, tunatakiwa sisi tuliourithi kutoka kwa waliouasisi kuundeleza na kuutunza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali na vikao mbalimbali vya kutatua changamoto mbalimbali za Muungano zinazojitokeza, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada hizo inazozichukua siku hadi siku. Pia napenda kukubaliana na maoni ya Kamati kwamba mgawanyo wa ajira na uwiano wa watumishi katika sekta za Muungano ufanyiwe kazi na uwe uwiano ule uliopangwa ili kuhakikisha pande zote mbili za Muungano zinanufaika na utumishi huo na ajira hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, najikita kwenye upande wa mazingira. Napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali inazochukua katika kuhakikisha nchi yetu inatunza mazingira, tunadhibiti mabadiliko ya tabianchi kwa

ujumla na shughuli mbalimbali za uhifadhi wa mazingira. Napenda nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, naipongeza Serikali kwa kuwekeza miradi ya mazingira mbalimbali kwa upande wa pande zote mbili za Muungano, na upande wa kwetu Zanzibar tumepata miradi ya kujenga tuta, ukuta, kuhifadhi maji chumvi yasiingie. Pia, tumepata mradi wa majiko ambayo yanatumia nishati mbadala ili kuepusha ukataji wa miti na kuni. Vile vile mradi ambao utasaidia wananchi wa Pwani wasipasue mawe ili kujengea kwa kupewa boti kama mbadala wa biashara zao na kujiingizia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto bado ziko, hasa kwa upande wa visiwa. Visiwa vyetu vinaliwa na maji ya bahari na kuna hatari ya kupoteza uhalisia wa visiwa hivi. Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo sasa ni Tanzania na ndani ya Tanzania kuna visiwa ambavyo vinahitajika duniani. Tudhibiti visiwa hivi visichukuliwe na bahari na baadaye vikapotea kabisa kwenye ramani ya dunia. Tanzania ni bara na visiwa vyake na hasa maeneo ya pwani. Maeneo kama ya Nungwi, Kizimkazi, Makunduchi, Mkoani, haya tayari maji yanapanda juu na yameshaathiri makazi ya wananchi na huduma mbalimbali za kijamii. Ni vyema sasa tukawekeza zaidi kuhifadhi visiwa hivi kwa sababu maji ya bahari yana nguvu kubwa yanapoingia kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea naomba nichangie kuhusu hapo hapo kwenye mazingira. Ukataji wa miti bado umekuwa mkubwa. Ukataji wa miti hauendani na uwekezaji wa miti. Tufanye tathmini ya kutosha, uwekezaji wetu wa miti unaendana na uhalisia wa miti iliyoota? Kwa sababu, tunawekeza fedha nyingi katika kupanda miti, lakini hatuna uhakika wa kutosha kwamba miti ile yote iliyopandwa

inakua na inastawi. Tukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam tu, mkaa unaotumika kwa mwezi ni tani ngapi? Kila tani kwa wastani ni miti mingapi? Miti mingapi kwa wastani ni hekta ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutazame hapo, tani zinazotumika kwa mwezi na miti inayokatwa kwa mwezi; kwa maana mti tunajua unatoa kiasi gani, kilo ngapi, halafu tuone sasa tani zilizokatwa miti ni hekta ngapi? Je, na upandaji wa miti unawiana na ukataji ule wa miti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, Tanzania tuna ardhi ya kutosha, tuna misitu, tuna eneo kubwa, lakini kuna fedha nyingi zimewekezwa kwenye mambo ya hewa ya ukaa. Kwenye hewa ya ukaa bado Tanzania hatujasaini, lakini kuna nchi ambao ni majirani zetu wa Afrika ikiwemo Kenya, Burundi, inatarajia kusaini; Gabon, Mozambique, Malawi, wameshasaini mkataba ambapo katika mkataba huo kuna ajira zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira zitakazopatikana kwa ajili ya uwekezaji kwenye hewa ya ukaa na fedha nyingi zitapatikana kwenye hewa ya ukaa. Kama ajira milioni 30 zinategemea kupatikana ifikapo mwaka 2030, lakini pia inatarajiwa kupata fedha kwa kupitia biashara karibu Shilingi trilioni 14, sisi tumekwama wapi? Au kuna masharti magumu ambayo hayaendani na mila na desturi zetu? Kama hakuna masharti ya namna hiyo, basi tunapaswa na sisi kujiunga na kusaini, ili tuweze kufaidika na hizi fedha na uwekezaji wa ajira mkubwa ambao unapatikana kwenye hewa hii ya ukaa ambayo tayari nchi jirani zetu wameshajiunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuishauri Serikali, ni kwenye utunzaji wa mazingira…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuwa mchangiaji. Awali ya yote, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Marais wetu; Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Taifa hili. Baada ya utangulizi huo, napenda nianze kwa kusema kwamba, vitu vyote duniani vina mipaka, lakini hakuna kitu kinachoweza kuunganisha dunia, mataifa, mabara na nchi kwa ujumla isipokuwa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za kimazingira hazitegemei wapi uharibifu wa mazingira umefanywa. Uharibifu wa mazingira unaofanywa na wanadamu ndio unaosababisha athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia iko *busy* katika kupambana zaidi na masuala haya ya mabadiliko ya taibanchi. Kwa kuzingatia hivyo, jambo hili linatupa picha wazi kwamba, *issue* ya mazingira ni *issue* ya *world, cross cutting issue,* siyo suala la Taifa moja, wala siyo suala la sekta moja katika nchi ambayo inastahiki kuchukua hatua. Ni lazima sisi kama nchi kila Wizara ichukue nafasi katika kukabiliana na masuala haya, kama tulivyo. Kwa sababu kila Wizara

inachukua jitihada kwa njia moja au njia nyingine bila kuhusika katika uharibifu wa mazingira. Kwa nini tushindwe kuchukua jitihada za msingi kwa kila Wizara katika Serikali hii kuweza kupambana na kuweza ku-*control* masuala ya uharibifu wa mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati dunia ipo katika kupambana na uharibifu wa hali ya hewa na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi sisi tukiwa kama Taifa, bado sioni haja na kujigamba kwamba tunachukua jitihada za kutosha katika kukabiliana na hali hii. Kwa sababu, sisi kama Taifa kupitia chombo hiki kitukufu, Bunge, leo hii tunajadili suala la mazingira na Muungano kwa kuchanganya vitu viwili kwa pamoja, wakati vitu hivi ukiviangalia, *concept* ta mazingira ndiyo inayobeba agenda ya dunia nzima sasa hivi. *Concept* ya Muungano maana yake ni masuala ya nchi mbili. Leo hii tunajadili kwa kutumia kutwa moja, sijui kama kweli tunachukua jitihada za kutosheleza kukabiliana na hizi *effects. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwenda kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, miradi yake haitakiwi kutekelezwa kwa kutumia bahati katika majimbo. Tunatakiwa tuangalie ule uhalisia, wapi *effects* zinaonekana waziwazi na kwa muda gani? Sisi kama Taifa hatuwezi kwenda kumshughulikia mgonjwa aliyekuja hospitali aliyejikata wembe wakati anakata kucha, kisa kaja mwanzo, tukamwacha mama mjamzito ambaye amefika hospitali muda huu akiwa anagaragara kutokana na uchungu wa kutaka kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana gani? Sisi Nungwi hali ni mbaya. Mkoa wa Kaskazini kiujumla athari za mabadiliko ya tabianchi siyo jambo la kufumbia macho. Bahari, upepo, visima kujaa maji ya chumvi vinaangamiza sana Jimbo la Nungwi, Kijini na hata maeneo ya jirani. Nakumbuka mwaka jana niliuliza swali dogo la nyongeza

kuhusiana na hatua mtakazoweza kuchukua kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, maeneo ya Nungwi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Muungano na Mazingira alijibu kwamba, katika bajeti ile ya 2021/2022 watatenga fungu la kwenda kujenga kuta pale, lakini cha kusikitisha, bajeti ilipita na hakuna hata moja lililofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alikuja Jimboni kwangu Nungwi, kaka yangu Mheshimiwa Jafo. Baada ya kuja tukaenda kukagua, lakini nasikitika mpaka leo hii bado sijaona jitihada zilizochukuliwa. Nimwambie kitu, ziara yake ilitupa matumaini sana, lakini ilikuwa aniambie tu ukweli kwamba alikuja zaidi kama ni *holiday.* Nikamwandalia *life jacket* angalau aende kuogelea na makasa na makobe kule, kama wanavyofanya watalii wengine. Kwa sababu, tulitegemea ziara ile itazaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku watu wanaohusika na suala la Muungano na mazingira wanakuja eneo la Nungwi, wanapima kwa kamba, wameshakuja kupima kwa *GPS,* kwa *tape,* kila aina ya vipimo wanakuja, lakini hakuna kimoja kinachofanyika. Sasa bora tuambizane kwamba eneo lile tulihifadhi kwa ajili ya utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi, ili wale wananchi tuwaondoe, tuwape ardhi sehemu nyingine kama Mwanza, Kagera, tuwatafutie sehemu ya kuishi ili pale tukatumie kwa rasilimali hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu, Mheshimiwa Selemani Jafo, na ninafikiria watu wa Muungano na Mazingira kwa upande wa Zanzibar wananisikia; chonde chonde, umesoma bajeti lakini bado halijakuwemo. Maeneo yale yanatuathiri vibaya sana, yanatudhalilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, upo, wewe ni msikivu sana. Shauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Zanzibar ni Visiwa ambavyo vinaathirika kwa asilimia kubwa

kutokana na staili ya mabadiliko ya tabia nchi kwa sababu tumezungukwa na bahari. Misaada inayokuja, uhisani unaokuja, ni vizuri tukaelekeza nguvu zetu kule kwa sababu athari zake zinaonekana waziwazi, hususan Nungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chonde chonde kaka yangu, nakuomba kupitia Serikali hizi Tukufu, Serikali sikivu. Twende tukatekeleze ujenzi wa ukuta kuzuia bahari isiendelee kutuathiri maeneo ya Nungwi na vitongoji vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu, Mheshimiwa Jafo, nakumbuka katika bajeti iliyopita vilevile kuna suala la mfuko wa jimbo. Kuna fedha za mfuko wa jimbo tulipitisha hapa kama sote majimbo ya Tanzania kwa kuongezewa. Lakini kinachosikitisha ni kwamba mpaka leo hii majimbo ya Tanzania Visiwani tunapiga zogo. Bado hatujaongezewa chochote. Fedha zile zipo kwa ajili ya kwenda kuipa *support* miradi ambayo haikupata fungu katika bajeti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Haikupata fungu…

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, taarifa Mheshimiwa Simai.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaelewa sana tatizo analolizungumza Mheshimiwa Simai la fedha za mfuko wa jimbo. Naomba tu nimpe taarifa na kumhakikishia kwamba Serikali imeshalifanyia kazi na muda si mrefu kadhia hiyo itakuwa imeshatatuliwa kupitia Wizara ya Fedha, na Waheshimiwa Wabunge wote wa Zanzibar watapatiwa fedha hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante; Mheshimiwa Simai, taarifa hiyo.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo, ahsante sana. Lakini fedha hizi tukumbuke kwamba zipo kwa ajili ya kuchochea maendelea ambayo ni miradi ya wananchi ambayo haikuwa kipaumbele katika miradi iliyotengewa fedha kwa ajili ya bajeti. Sasa niiombe Serikali tuharakishe mchakato huu wa mfuko wa jimbo na sisi Wazanzibari tupate hiyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ambayo iko mbele yetu ambayo inahusu Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niwapongeze viongozi wetu wawili; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo wanaendelea kushirikiana na kwa namna ambavyo wanaendelea kufanya kazi ya kuleta maendeleo kwa Serikali zote mbili; Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yao kwa utendaji wao mzuri wa kazi hizi na niwaambie tu kwamba tunaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba mambo haya ya Muungano yanaendelea kuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwaomba Watanzania wote, hususan vijana, kuendelea kuulinda, kuutetea na kuupigania Muungano wetu huu kwa faida ya nchi zetu zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba vikao vya Kamati ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Muungano vinaendelea na hoja mbalimbali – kama ambavyo Mheshimiwa Waziri leo amewasilisha – hoja mbalimbali tayari zimepatiwa ufumbuzi; niipongeze sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo bado tunazo kero mbalimbali ambazo zinaendelea kuleta changamoto kwa nchi zetu mbili. Alisema kwamba hoja ya mizigo inayotoka Zanzibar kuja Bara imeondolewa kodi zile ambazo zilikuwa ni kodi mara mbili, lakini bado hoja hii inaonekana kuwa ni changamoto, hasa kwa mizigo midogomidogo ambayo inatoka Zanzibar kuja Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliyoondoka ni hoja ya wafanyabiashara lakini haijaondoka hoja ya wananchi wanaosafiri kwenda Zanzibar na kurudi Bara wanaosafiri na mizigo yao midogo midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mwananchi amesafiri na kilo mbili za sukari anafika nazo Bara anaambiwa alipe kodi. Haiwezekani mwananchi amesafiri na *TV* moja, tena *used,* anakuja kutumia nyumbani, anafika Bara anaambiwa alipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni nchi moja, haiwezekani wananchi hawa anayetoka Morogoro kwenda Dar es Salaam halipi kodi anaondoka na mizigo yake, anaondoka na mambo yake kama hayo lakini hakuna sehemu yoyote ambayo anasimamishwa kulipa kodi. Lakini anayetoka Zanzibar kuja

Bara akifika Dar es Salaam anatakiwa alipe kodi kwa *TV* moja ambayo anakwenda kutumia nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili halijakaa vizuri. Niiombe sana Serikali ilifanyie kazi jambo hili. Bado kabisa halijakaa vizuri na inaleta kero kubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona magari ya nchi jirani mbalimbali yanayozunguka hapa Tanzania na hayana usumbufu wowote, hayaletewi usumbufu wowote, lakini kuna changamoto kubwa kwa usajili na utambuzi wa magari yanayotoka Zanzibar kuja Bara kuweza kutumika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ni moja, Tanzania ni moja. Ni kwa nini mpaka leo hakujawekwa sheria inayotambua, inayosajili magari yanayotoka Zanzibar kuja kutumika hapa Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, jambo hili limezungumzwa muda mrefu sana na linaendelea kuwa kero. Niiombe sana Serikali, nikuombe sana Waziri, utuambie ni lini utaleta sheria ya kuweza kuweka wazi masuala ya usajili wa vyombo vya usafiri…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba juzi tu nilinunua *TV* nilivyofika bandarini nikachajiwa *difference* laki mbili. Kwa hiyo, tatizo hili ni kubwa kweli kabisa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar, taarifa.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado changamoto hii. Kwa hiyo tuombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie, Sheria ya Usajili wa Vyombo vya Usafiri ni lini italetwa Bungeni kuweza kujadiliwa na kuweza kupitishwa rasmi na kuondoa mkanganyiko na usumbufu huu unaotokea kwa vyombo vya usafiri vinavyotoka Zanzibar kuja Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ajira, hasa kwa taasisi za Muungano. Upo uwiano ambao umebainishwa wa asilimia 21 kwa Zanzibar na asilimia 79 kwa Bara kwa zile taasisi zote za Muungano. Bado pia hapa kuna changamoto; hakuna utaratibu ambao uko wazi unaobainisha hizi asilimia 21 zinapatikanaje na asilimia 79 zinapatikanaje. Kwa hiyo, naomba sana Serikali hebu ifanyie kazi jambo hili, iweke utaratibu ulioko wazi, unaoonekana na ambao hauna mkanganyiko, kwamba tujue asilimia 21 zinapatikanaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri kwamba kuna haja na umuhimu mkubwa wa kufanya tathmini ya watumishi wa Umma wanaofanya kazi kwenye sekta za Muungano; bado. Likifanyiwa tathmini jambo hili naamnini itakuja kutuletea majibu hapa kwamba jambo hili hasa likoje. Ni kweli asilimia 21 inatekelezwa? Ni kweli ajira hizi ziko hivyo

ambavyo inazungumzwa? Lakini pia tutapata majibu mengi na tutaondosha manung'uniko mengi ambayo yapo sasa hivi yanayoendelea. Niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje na majibu haya kwa ufasaha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha jambo hilo pia kuna suala la ushiriki na ushirikishwaji kwa taasisi ambazo siyo za Muungano. Tunafahamu kwamba ushirikishwaji na ushirikiano wa taasisi za Muungano hakuna shida sana, lakini kwa taasisi zisizo za Muungano, na hasa kwa mikutano inayofanyika ya kimataifa ambapo Tanzania inakwenda kushiriki kule, Zanzibar bado baadhi ya taasisi hazijaweza kushirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba baadhi ya taasisi tayari, kwa mfano Ofisi ya CAG tayari mikutano mbalimbali Zanzibar inashirikishwa. Lakini kuna taasisi kwa mfano suala la Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, Zanzibar tuna mamlaka yetu na Bara tuna mamlaka nyingine. Kwa hiyo, niombe sana kwa mikutano ya kimataifa ambayo Tanzania inakwenda kushiriki kwa taasisi ambazo siyo za Muungano basi Zanzibar iweze kushirikishwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la mwisho ambalo ni suala la mazingira. Amezungumza hapa Mheshimiwa Simai, Mbunge wa Nungwi, kwamba jambo hili ni changamoto kubwa, hasa kwa visiwani. Mabadiliko ya tabianchi ni jambo kubwa sana kwa visiwa. Visiwa vinaendelea kuliwa na maji. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iweke msisitizo na mkazo mkubwa kwenye suala hili la mabadailiko ya tabianchi na kuongeza fungu hili la bajeti, hasa kwa maeneo ya visiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kusema hayo, niiunge mkono hoja hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango. Sasa namwita Mheshimiwa Nusrat, ajiandae Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na nitachangia upande wa Fungu 31, Idara ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira kwa umuhimu wake ni jambo ambalo mpaka sasa naona hatujalipa umuhimu wa kutosha kama ambavyo linastahili. Labda nitaje sekta ambazo zinaathirika kwa namna moja au nyingine na suala la mazingira, kwa namna zozote zile; sekta za maji, kilimo, afya, miundobinu na uchukuzi, nishati, madini, mifugo na uvuvi, maliasili na utalii, viwanda na biashara, teknolojia, elimu *and the list goes on.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hapa tulipo sisi kila Mbunge anawakilisha jimbo analotoka, kwa namna moja au nyingine hawezi kukwepa kuzungumza suala la mazingira na sasa hali ilivyo, mabadiliko ya tabianchi. Lakini inasikitisha kwamba upangaji wetu na mgawanyo wa fedha katika bajeti zetu za miaka ya fedha kwenye sekta ya upande wa maendeleo kwenye upande wa mazingira hatujatendea haki sekta na idara ya mazingira kama ambavyo inastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitaje kwa mfululizo miaka ya fedha mitatu mfululizo; fedha za miradi ya maendeleo zimetengwa kwa kutegemea sana fedha za nje katika kiwango kilichokithiri. Mwaka 2021/2022, Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 2.979, lakini asilimia 86.54 ya fedha hizi zilikuwa za nje, sawa na shilingi bilioni 2.570. Fedha za ndani zilikuwa milioni 400 tu ambayo ni sawa na asilimia 13.54, ndiyo hizo pesa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022/2023 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 18.642, lakini fedha za nje zilikuwa asilimia 98.5, sawa na shilingi bilioni 18.360. Fedha za ndani ambazo ni za kwetu zilikuwa asilimia 1.5, sawa na shilingi milioni 282 hivi; hiyo ndiyo pesa yetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha, Serikali imeomba shilingi bilioni 16.656, lakini tunategemea shilingi bilioni 15.056 fedha za nje, sawa na asilimia 90.4. Lakini fedha za ndani, za kwetu sisi sasa, ni shilingi bilioni 1.6 pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, atahari ya kutenga fedha kwa kutegemea fedha za jirani, fedha za wahisani, fedha za nje, ili upange mipango yako, ni sawasawa na sikukuu imefika unataka upike pilau lakini wewe una sufuria na mwiko, unategemea kila kitu pamoja na nyama na kuku na kila kitu kutoka kwa jirani. Jirani akiuguliwa, akifiwa, akiwa anapigana vita, wewe huwezi kula athari yake ni kubwa. Labda nikiongea hivi inawezekana ikawa lugha nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano. Mwaka 2017, Mfuko wa *Green Climate Fund (GCF)* ulitenga fedha kwa ajili ya Mradi wa *Climate Change* wa Mkoa wa Simiyu Dola milioni 187.7, lakini fedha hizo hazikuletwa zikaweza kuletwa mwaka 2020. Kutoka mwaka 2017 athari zimetokea, mradi umefanikiwa kupita kwenye vigezo vyote vya kupewa fedha lakini fedha imeletwa mwaka 2020. Kwa sababu anayetoa fedha ndio anayechagua wimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari zilizosababisha watu wa Mkoa wa Simiyu wapewe hizi fedha bado zinaendelea. Lakini kwa sababu tumeomba fedha kwa wahisani – na ni kitu kizuri, sisemi kwamba ninabeza kwamba haifai kupewa fedha za wahisani – lakini kuitegemea fedha za nje kwa kiasi hiki, zaidi ya asilimia 90, maana yake unashindwa kutekeleza miradi yako kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta nyingine zote nilizozitaja hapa zimetengewa fedha za ndani. Utekelezaji wake unategemea hizi fedha.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata hizo fedha ambazo mradi unatekelezwa kule Simiyu ziliombwa kupitia *Save the Children Fund,* Tawi la Canada. Kwa hiyo, hoja yake ni ya msingi sana kutenga fedha za kutosha hata hapa ndani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, taarifa hiyo.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napoikea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu chako ukikiuona ni cha muhimu utakipa *first priority* na utakitengea fedha. Bahati mbaya sana Serikali inapeleka fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kwenye sekta nyingine ambazo nilizitaja hapa ambazo zinaathirika kwa namna moja au nyingine na mazigira. Lakini fedha hizi utekelezaji wake pia unategemea *stability* ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunashindwa kutekeleza miradi ambayo Serikali imeitengea fedha nyingi kwa sababu ya athari za mabadiliko ya tabianchi na athari za kimazingira. Kwa hiyo, tunasababisha kupoteza wakati mwingine rasilimali za nchi kwa sababu hatuja-*prioritize* kutoka kwenye vyanzo vyetu vya uhakika ambavyo ni vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano. Mwaka huu ili tuone umuhimu wa kutenga fedha kutoka kwenye vyanzo vya ndani – mwaka huu wa fedha hizi shilingi bilioni 1.6 ambazo ndiyo chanzo cha ndani, asilimia 9.6 ya fedha za ndani kwenye mwaka huu wa fedha, hizi zinakwenda kujenga vitu vya msingi sana, wameongea watu wa kutoka upande wa pili wa Muungano, tunakwenda kujenga kingo ya Mikindani, Mtwara na Sipwese, Pemba kule, kwa hiyo unaona umuhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakuwa na *projects* za namna hii ambazo zinaangalia palipoathirika zaidi na kwenda kutafuta namna ya ku-*solve* pale kutoka kwenye vyanzo vyetu vya ndani, sisi ndiyo tutakuwa tumetoa fedha na wimbo tumechagua sisi maana yake tunakwenda kutibu athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo wananchi wanaziona moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumze jambo la pili kwenye *climate funding*. *Green Climate Fund* ndiyo mfuko mkubwa ambao Shirika la Umoja wa Mataifa la kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi *(UNFCCC)* wanautumia kwa ajili ya ku-*fund projects* za masuala ya *climate*. Lakini sisi nchi yetu, taasisi za Serikali hakuna hata taasisi moja ambayo iko *accredited,* haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ndiyo nchi ambayo ina miradi mitano tu kupitia *Green Climate Fund,* lakini Kenya wana miradi 16, Uganda wana miradi 10, Rwanda wana miradi tisa. Sisi tumeshindwa kuzisaidia taasisi zetu ambazo ziko chini ya Serikali kupata *accreditation* ili tupate hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CRDB* peke yake ndiyo imepata *accreditation* lakini mnakumbuka *CRDB* wanafanya

kwa njia ya mikopo, siyo *grants.* Sisi taasisi zetu zinatakiwa zipate fedha…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ni kengele ya pili. Mheshimiwa Nusrat mchango wako ni mzuri, isipokuwa sasa tujielekeze wahisani kwa nini hawaleti hizi pesa. Wahisani wanaweka ahadi kwa sababu wao ndio wanaochafua mazingira, sasa kuwe na mkakati wa kuzidai hizi pesa, siyo kusema tuziache hivi hivi tu. Kwa hili siyo wahisani, ni *obligation* na *commitment* ambayo nchi ambazo zinaharibu mazingira zime-*commit*. Afrika inachangia *percent* mbili tu ya uchafuzi.

Kwa hiyo, sasa wangekuwa wanajenga kwa nini hawatuleti, unazungumza na Waziri wa Mazingira anakupa *ticket* unakwenda unagombania hela zetu kule. Umeelewa?

Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, jiandae Mheshimiwa Profesa Shukrani.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Ofisi hii ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijalia kupata nafasi hii. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anazozifanya katika nchi yetu. Nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuisimamaia nchi yetu lakini pia kwa kuusimamia Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru watangulizi wa Muungano huu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja

na Marehemu Aman Abeid Karume, kwa kweli walikaa wakafikiri suala kubwa sana kuungana na kutufanya sisi kuwa ndugu. Wao waliunganisha udongo au walichanganya mchanga, lakini Muungano wetu kwa sasa sisi tumechanganya damu. Kwa kweli sisi sasa hivi ni ndugu hatuwezi kutengana na hatuwezi kugombana; mambo mengine madogo madogo yatakayotokea hayo ni mambo ya kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumpongeze mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuusimamia Muungano huu. Kuna watangulizi wake walipita, yeye ni Rais wa Sita lakini amefanya mambo makubwa sana, na shahidi ni Mheshimiwa Waziri ambaye amezungumza kuwa kero nyingi za Muungano zimetatuliwa. Hilo tulijua litafanyika kwa sababu Muungano huu sasa hivi umetufanya sisi kuwa ndugu, hatutakiwi tugombane, tuzozane wala tuoneane, lazima tuwe pamoja, na mama yetu hilo ndilo analolitaka. Mimi bado nitashikilia, kung'ang'ania kushikilia na kusema kuwa Mama Samia ni mcha Mungu, Mama Samia ni mkweli, bado nitaendelea kuzungumza suala hilo Mama Samia ni mkweli na ni mcha Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu watangulizi walitangulia walizungumza kuhusu kero za Muungano. Mimi nasema kero zipo na zitaendelea kuwepo madhali sisi ni binadamu; lakini nasema kwa kipindi cha Mama Samia mambo mengi yatatatulika; yametatuliwa lakini ataendelea kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu walizungumza kuhusu kero ya Bandarini. Bandarini pana matatizo makubwa sana; kuna wanawake wanaotoka Zanzibar wakati wa hizi Sikukuu wanakuja kununua vitu vyao vidogo vidogo Dar es Salaam, na tunasema nchi yetu ni moja, ni Tanzania, wakifika pale bandarini wanaadhibiwa sana na suala hili

tulishalizungumza sana. Sisi ni ndugu, Mheshimiwa Waziri tunamwomba afike bandarini kama wale watu wa bandarini hawana elimu wakapewe elimu. Sisi tunazungumza ni ndugu lazima tukubaliane, kuna mambo mengine hayana haja ya kujitokeza sisi kuja kulizungumza humu. Ni sisi wenyewe tujue hiki hakikubaliki, hili halikubaliki, lakini kumekuwa na unyanyasaji mkubwa bandarini wenzangu wamezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtu anakuja na *TV* yake moja, *TV* moja kweli ni ya kufanya biashara anakwenda kuzungumza na Watoto wake sasa hivi azam Alhamdulillah makero mengi mengi ma-*stress* yanaondoka kwa Azam tu, anakuja mtu *TV* ile ailipie kodi, tena anaambiwa ondoka, nimeshuhudia anaondoka. Ukienda kusema jamani mwachieni hayo matusi utakayoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutakuwa tunavuruga Muungano na tunamvurugia mama yetu. Yeye ana nia nzuri kuutetea Muungano huu na bado anautetea na anaulinda kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hiyo na sisi tuliopewa nafasi lazima tuzisimamie kwa kuzitetea nafasi zetu na kuwatetea wananchi wetu. Wanawake wengi wanaofanya biashara ndogo ndogo wanadhalilika, wanateseka bandarini, biashara zao zinapotea, inauma sana. Hawa ndio wapiga kura wetu; na mwanamke tunasema sasa hivi ndiye mtetezi wa nchi hii, lazima tupewe kipaumbele. Muungano wetu ndio kama ni kioo chetu, kwa hiyo lazima muungano huu tuulinde, tuutetee, na msimamizi sasa hivi ni Mama, hakutuacha nyuma. Sisi tunasema hatuna malalamiko makubwa ya kuzungumza kuhusu Muungano huu maana yake tunasema sasa tumechanganya damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,asilimia kubwa ya Wabunge wa Zanzibar wanaokuja miaka mitano lazima anaacha watoto huku. Huku wanaacha Watoto, ndiko kuchanganya damu huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,Kwa kweli Mheshimiwa mambo ya hizi kero, mambo madogo madogo yaondoke. Sisi kila siku tunazungumza tunapiga kelele tunazungumzia hayo kwa hayo yale kwa yale, hayapendezi. Muungano wetu nchi nyingi wanatuonea choyo au wanatuonea husuda, kwa kweli ni jambo la kusikitisha.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, taarifa

**TAARIFA**

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa dada yangu anaye changia hapa sasa hivi. Si kwamba wanaacha watoto tu, mimi mwenyewe hapa ni mtu wa Morogoro Mama yangu ni Mtu wa Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeyasikia maneno. Muungano huu hatukuchanganya udongo peke yake. Udongo bado utabakia kwenye kumbukumbu lakini sasa hivi tunasema Muungano huu tumechanganya damu. Tukizungumza hapa tukijifafanua asilimia kubwa tunasema sisi ni ndugu wa baba mmoja. Kuna mambo lazima tuyazungumze kiudugu, lazima tukubaliane isiwe kila siku tunapiga kelele Muungano Muungano. Muungano huu hakuna yeyote wa kuweza kuutengua kwa kusema huu haufai kwa sababu ukisema haufai mimi nikirudi Zanzibar huku na acha dada yangu, naacha bibi yangu, naacha shangazi yangu. Siwezi kwenda kule lazima huku nitarudi. Sisi sasa hivi tunakwenda *free* Zanzibar na Bara kwa sababu sisi ni ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utazunguka bara yote lazima utamkuta Mzanzibar yupo kazaa amejukuu kwa hiyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanahamisi, ahsante kwa mchango mzuri, ahsante. Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Rais Mazingira na Muungano. Mimi nitajikita katika sehemu ile ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika,ni kweli kwamba suala la mazingira ni mtambuka, na kama walivyotangulia wenzangu lina gusa Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Sekta binafsi; na kwa jinsi hiyo tungetamani hata kwa namna ambavyo suala la mazingira linashughulikiwa ndani ya Serikali liweze kuwa na mfumo ambao pia ni jumuishi; la sivyo likiachiwa Wizara moja kama Wizara moja tutaona kwamba athari zake zinaweza zisishughulikwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kuchangia hoja hii na mimi ningependa kuendelea kuweka msukumo zaidi, kwamba bajeti inayotengwa kutoka fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo bilioni 1.6 dhidi ya bilioni 15 za wahisani nadhani hatujitendei haki. Tunapaswa tukubali kwamba wakati mwingine changamoto zinazotokana na athari za mazingira ni changamoto ambazo ni zetu binafsi kuliko hata zile ambazo zinatoka kwa fedha za wahisani na kwa hiyo tuombe Serikali; kwa mwaka huu kama ilivyopendekezwa sawa; lakini kwa miaka ijayo tuendelee kuweka msukumo wa kuongeza bajeti ili itusaidie kuweza kushughulikia hoja za mazingira ndani ya nchi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nipende kuwapongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wamekuja na kampeni ya upandaji miti kote nchini. Lakini kampeni hii ingefanikiwa sana iwapo kungekuwa na mwongozo wa aina gani ya miti ipandwe kulingana na hali halisi ya maeneo husika. Kuna hatari ya kupanda miti katika vyanzo vya maji, na tunajua kuna miti ya mikaratusi, ukiipanda kwenye chanzo cha maji itanyonya maji yote na chanzo hicho kitakauka. Sasa tumeanzisha kampeni nchi nzima lakini mwongozo unachelewa. Tuwaombe Wizara waharakishe mwongozo kwa kuangalia ikolojia ya mahali husika ili wapande miti kulingana na mahitaji ya eneo husika, hilo litaweza kuwa na tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa nikiwaza kidogo, kwamba kama tungekuwa tunafanya maamuzi haya ya kujumuisha pamoja; muda mfupi uliopita Serikali imejenga majengo mengi sana ya taasisi za Serikali kwa maana ya shule na hospitali; laiti tungeliongeza fedha kidogo halafu tukaweka mifumo ya ukasanyaji maji katika taasisi hizi maana yake ni kwamba tungekuwa na maji ya kutosha kwa ajili hasa ya kumwagilia miti hii ambayo tunataka ipandwe nchi nzima. Kwa hiyo wakati mwingine tunapokuwa tunakuja na hoja ambazo ni jumuishi tuone kwamba tunaweza tukalisaidia. Leo kama kila shule iliyojengwa ingekuwa na mfumo wa ukusanyaji maji au kila hospitali iliyojengwa ingekuwa na mfumo wa ukusanyaji maji tungeona kwamba maji yangekuwepo yakutosha. Hata kumwagilia miti itakayopandwa na hata ukame utakapokuja bado miti inaweza ikakua vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda uliobaki naomba nichangie kuhusu uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya makazi; na haya yanasimamiwa vizuri tu kwa bajeti iliyopo, kwa hiyo tunachosisitiza hapa na kuomba ni usimamizi wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kelele na mitetemo katika makazi ya watu. Bado tunashuhudia katika nchi ambayo tuko katika uchumi wa kati, nchi ya wastaarabu baada ya saa nne usiku tunashuhudia kelele kutoka katika vilabu, kutoka katika nyumba za ibada. Sijui kuna shida gani katika hili, lakini sio sawa, kwamba katika nchi ya wastaarabu bado tuendelee kusikia mziki anao upenda *DJ* wa klabu husika wakati mimi siupendi mziki kwa wakati huo na ninahitaji kulala; na mara nyingi imetusumbua tunakwenda mahali kufanya kazi katika mji husika lakini unalazimika kusikiliza mziki uliochaguliwa na klabu hadi saa nane usiku, hili jambo halipendezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tena kwa mara nyingine, *NEMC* wanaweza, mahali kwingine walikwenda na wakapiga *stop* na haikuendelea tena; lakini mahali kwingine wanatoa faini tu na bado watu wanaendelea kupigia watu kelele usiku. Tunadhani kwamba sisi ni nchi ya wastaarabu ambayo inapofika saa nne usiku hatuhitaji kuendelea kupigiwa kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, na hili nalo linahitaji usimamizi wa kawaida tu. Mfumo wa ukusanyaji wa taka ngumu. Nilikuwa nataka nipendekeze kwa Wizara na taassisi husika. Kwamba, mbona sisi katika nchi yetu leo bado tunachanganya maganda ya ndizi na ya viazi pamoja na chupa ya coca cola na *heineken* iliyoisha halafu wote unakuwa ni uchafu mmoja upelekwe dampo, kwa nini? Yani tumeshindwa kama nchi kutoa elimu ya kwamba taka zinazotoka jikoni zitengwe mahali fulani, chupa zitengwe mahali fulani hata basi ziende zikatumike tena. Ninadhani tutatenda haki sana iwapo tutawaambia wananchi wetu waweze kutenganisha aina ya taka za nyumbani ili kwamba ziweze kutumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu viwanda. Viwanda vingi sana vimejengwa katika maeneo ya

makazi, na wakati mwingine viwanda hivyo vinatoa moshi mzito na kutiririsha maji machafu katika maeneo ya makazi. Kwa mfano ni wakazi wa Kibangu Makuburi. Viwanda vile vilivyoko pale *EPZA* vinaendelea kutoa moshi mzito pamoja na kutiririsha maji machafu. Hili hebu *NEMC* walisimamie vizuri. Kupiga faini peke yake hakutoshi, unapiga faini leo lakini tatizo bado lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, sijui kama ni mimi binafsi lakini nadhani kwamba Watanzania wote tunaona. Sasa hivi maeneo ya mjini, hasa katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani utagundua kuna vituo vya mafuta vinajengwa katika makazi ya watu kila baada ya mita 100, na wakati mwingine vituo hivi vya mafuta viko upande wa kushoto na kulia mwa barabara ya lami. Sasa unajaribu kujiuliza, kwa nini hali hii iko hivyo? Hivi hatuoni hatari ya kwamba vituo vya mafuta viko katika makazi ya watu na wakati mwingine havina hata uzio? Hivi ikitokea ajali ya moto tutasemaje? Kwamba ni kwa sababu hatuwezi kusimamia? Au ni kwa sababu tumeona hii hali ya kujenga holela ya vituo vya mafuta iendelee katika makazi ya watu? Sidhani kama hili ni jema kwa usalama wa Raia wa nchi yetu. Tunaomba sana Wizara husika iweze kulishughulikia kwa ufasaha. Utitiri wa vituo vya mafuta katika makazi ya watu katika jiji la Dar es Salaam si afya na wala si jambo la usalama kwa usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika,baada ya kusema hayo najua muda wangu unakwisha, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zahor, jiandae Naibu Waziri, jiandae Mtoa hoja.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba pia ikikupendeza au ikupendeze, endapo nitakukwaza kwa

muda wako basi univumilie kidogo ili tuweze kusaidia mchango kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja, na pia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ndiye nguzo anayehakikisha kwamba Muungano wetu huu unaendelea kubaki kuwa Muungano; lakini ni kiongozi anayeongoza kwa upenzi, kwa masilizano, kwa mashirikiano wala haongozi kwa bakora. Kwa hiyo mimi naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vile vile naomba nimpongeze na Rais wa Zanzibar kwa sababu watu wawili hawa ndio wanaotengeneza kitu kinachoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila ya hawa na bila ya kufuata misingi ya Katiba, Sheria na Kanuni zetu maana yake hakuna kitu kinachoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote, bila ya kuwasahu wenzetu waliopewa dhamana ya kusimamia Wizara inayohusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa leo niende kwenye namba lakini sitaingia kwenye namba, leo nitaingia kwenye *foundation* ya Muungano. Wenzetu hawa wamepewa chombo kikubwa sana, wamepewa chombo ambacho ndicho kinachoshikamanisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila Dira kukihenga henga chombo hiki sisi sote hapa hatuna sababu ya kuwepo. Kwa sababu tunakuwekwa hapa kwa kuwaenzi wazee wetu walipoamua, na wazee wetu waliamua kuunda kitu kinachoitwa Tanzania si kwa sababu ya Sheria, si kwa sababu ya Kanuni ila ni kwa sababu ya mapenzi waliyokuwa nayo kwa kitu kinaitwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba ninukuu kidogo na ikupendeze. Kwenye katiba yetu hii kwenye eneo la kwanza kabisa la utangulizi, halafu mengine yatafuata; naomba ninukuu kwa heshima. Anasema hivi, Misingi ya Katiba; Na kwa kuwa sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa haikuzungumzwa katiba wala sheria, naomba nirudie, imesema misingi ya uhuru, haki, udugu na amani. Wasomi wamekuja baadaye wakatutengenezea mambo yote haya lakini kubwa ni uhuru na imani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maana yake ni nini? Naomba niwaombe ndugu zetu hasa waliopewa dhamana ya kuunda au kusimamia Wizara inayohusu mambo ya Muungano, kwamba wako wazee wetu waliounganisha pamoja na mama yangu amesema pale kwamba tumeunganisha mchanga sasa tunaunganisha damu. Sasa naomba niseme hivi iko misingi ya kuunganisha zaidi imetajwa katika Katiba yetu, lakini kuna Vyombo viwili ambavyo vimetajwa katika Katiba hii ambavyo wasomi wetu wametuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 88 wa Katiba hii au kwenye Kifungu cha 102 kwenye Sura ya Nne inazungumza kitu kinachoitwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Maana yake Sura yote ya Nne inazungumza uwepo wa Zanzibar na Serikali yake. Vile vile, kwa maana hiyo hiyo kuna kitu kinaitwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kuna kitu kinaitwa Makamu wa Rais, kuna kitu Kinaitwa Waziri Mkuu, lakini kuna hiki kitu kinaitwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivi ndivyo vifaa vilivyoundwa kwa mujibu wa Katiba hii ili kuifanya Katiba yetu na nchi yetu iwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu ni hili, sababu ya kunukuu hii inaonekana au wengine wasomi wanaamini kwamba Katiba ndio Tanzania. Naomba tu niwambie Tanzania ni mapenzi ya damu. Tuliwahi kusema huko nyuma kwamba tumeungana kwa sababu ya mapenzi, ningewaomba wenzetu hasa wanaosimamia hili, waelewe kwamba wapo walioamua kwa makusudi ili kuifanya Tanzania ibaki kuwa Tanzania. Kwa hiyo ombi langu sana kwao, waendelee kuheshimu makubaliano tuliyokubaliana, wameyataja wenzetu wengi hapa. Kuna mambo ya ajira, kuna mambo ya mazingira, kuna mambo mengi tu. Naomba waendelee kuheshimu kwa sababu dhamana hii waliyopewa waelewe kwamba ina kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe wenzangu kwamba tumetoka mbali. Mara baada ya Muungano wa mwaka 1964 kulikuwa na kitu kinaitwa *mutiny,* sijui kama mliwahi kukumbuka vijana wenzangu, hii kwa Kiswahili ni uasi lakini kwa sababu kuna kitu kinaitwa Jamhuri, naomba niwakumbushe wenzangu kwamba uwepo wa Zanzibar ndio ulisababisha Muungano ukawepo kwa sababu jeshi lililoko upande wa Zanzibar lilikuja kuchukua nafasi huku ili kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuelewe kwamba, kwanza kila upande wa Muungano kwa maana ya Zanzibar na Bara wote ni maeneo yaliyo sawa kwa mujibu wa Katiba hii. Hata hivyo, kwa maana hiyo hiyo ningeomba kwamba hata Wabunge walioko humu nashukuru hata katiba imesema, Wabunge wote waliotoka kwenye majimbo, waliotoka kwenye maeneo mbalimbali wote ni Wabunge walio sawa, hakuna aliye bora wala hakuna aliye na daraja la pili. Kwa hiyo, ningeomba sana wenzetu wa Muungano waendelee kutekeleza dhima yao ya kuhakikisha kwamba Muungano unaendelea kudumu kwa sababu sasa si matashi

tena, sasa ni damu. Hatuna nafasi ya kurudi nyuma tunayo nafasi ya kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kuendelea. Kuna hoja wameizungumza wenzangu hapa, kwamba hoja ya jambo la mazingira. Amesema Profesa pale na amesema dada yangu pale kwamba tumeweka bajeti asilimia ndogo kwa ajili ya kupambana na mazingira. Wanasema kutenda kosa sio kosa, lakini kosa ni kurudia kosa. Ningeomba sana na hili namwomba Mheshimiwa Waziri alitafakari sana kwa sababu kuishi ni haki yetu kwa mujibu wa Katiba, lakini kutengeneza matatizo ambayo yatatufanya sote tuondoke ni kinyume cha Katiba, kwa sababu Katiba inatutaka tuishi, imetupa mamlaka ya haki ya kuishi. Kwa hiyo, ningeomba wenzetu wa Wizara kwamba bajeti inayokuja wahakikishe kwamba kwa asilimia kubwa lazima tutengeneze mazingira ya ku-*survive* sisi kama Tanzania. Tunapoendelea kutegemea wafadhili hata kama kwa sababu wamefanya *commitment*. *Commitment* ni jambo lingine, lakini *commitment* inatakiwa ianze na sisi kama watanzania. Kwa sababu hatuwezi kusubiri mwenzetu ajengewe ukuta kwa sababu athari inamuathiri Nungwi kule eti mpaka mfadhili aje, lazima tuanze sisi wenyewe, tusisubiri wafadhili waje eti ndio tuanze kujenga ukuta wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Tanga pale kunaliwa na Bahari, eti tumsubiri mfadhili aje atufanye kazi ya kutujengea ukuta kwa sababu sisi hatuna nafasi hiyo. Naomba sana kwamba tuzingatie bajeti yetu kwa maana lazima iwe na *priority* ya mambo yetu ya athari za mazingira kwa sababu ni wajibu wetu na ni haki yetu kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, pamoja na kwamba muda umeisha ningeomba sana kwamba suala la mazingira ni suala la kufa na kupona…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Endelea dakika moja.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Naomba sana kwa sababu ya muda ningeomba sana wenzetu wa Wizara inayohusu mambo ya Mazingira, mazingira ni suala la kufa na kupona sio la kumsubiri mfadhili eti atuonee huruma au aji-*commit* leo, atoe mwaka 2025, huo ni wajibu wetu sisi kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi ni tatizo na athari zake zinaongezeka kila mwaka. Nchi zilizoendelea, zimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ongezeko la hewa ukaa angani, ambayo imesababisha upandaji wa joto duniani. Kwa mujibu wa makubaliano kwenye mikutano ya kimataifa, nchi hizo zilitakiwa kusaidia nchi zinazoendelea na masikini kwa kutoa utaalamu, teknolojia na fedha za kukabili athari za mabadiliko ya tabia nchi. Je Tanzania tumenufaikaje na *Climate Change Green Funds?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina miti mingi na hasa maeneo yenye mvua nyingi kama mkoa wa Kagera, miti

inayosadia kunyonya hewa ya ukaa angani. Je, kama nchi na kama mkoa tumenufaikaje na *Carbon Credit*?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya mvua nyingi sizizotabirika, Mto Kanoni katika Manispaa ya Bukoba hufurika kila mwaka na kusababisha uharibifu wa mali, nyumba, mifugo na hata kusababisha vifo vya watu na mifugo. Serikali iliahidi tangu Januari, 2023 kuanza kuongeza kina na kujenga kuta wenye kingo za Mto Kanoni. Ni lini fedha hizo zitaletwa ili kuondoa adha ya mafuriko ya kila mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maeneo ya *Custom*, Kafuti, Nyamkazi zinafurika sababu kina cha Ziwa Victoria huongezeka. Wakazi wa maaeneo haya wamekuwa wahanga wa mafuriko, wanafilisika kwa sababu ya vitu vyao na nyumba zao kuharibika kila mwaka sababu ya mafuriko. Kwa nini kusijengwe kuta kando kando ya ziwa kuwanusuru hawa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mazingira katika Halmashauri zetu hazipewi kipaumbele ili wakabiliane na athari ya mabadiliko ya tabianchi, inabidi wapewe bajeti ya kutosha. Wanashindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Napendekeza bajeti za Idara za Mazingira kwenye Halmashauri zetu, pia na bajeti ya Wizara hii iongezwe, sababu wana majukumu makubwa na mahitaji yanaongezeka sababu ya mabadiliko ya tabia nchi. Inabidi kama nchi tulione hili tatizo la mabadiliko ya tabianchi, tulipe umuhimu unaotosha, tulipe bajeti inayoridhisha na wakati wa kufanya hivyo ni sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilolo kuna mwekezaji anaitwa *Udzungwa Corridor* ambaye anawekeza katika kupanda miti ya asili kwa

ajili ya uvunaji wa hewa ya ukaa. Shida iliyopo ni ukiukwaji wa taratibu za umiliki ardhi na uwazi katika uwekezaji huo. Naiomba Wizara ije na majibu je, inamfahamu mwekezaji huyu? Kuna haja ya Wizara kushirikiana na Halmashauri kuona ni jinsi gani mwekezaji huyu ataheshimu mikataba yake na wananchi na kuacha kununua maeneo ya wananchi wanayoyatumia kwa shughuli za kilimo. Mwekezaji huyu amenunua hadi eneo la ujenzi wa shule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; Kilolo ina misitu mingi ya asili kuna haja ya Wizara kutoa *support* kwa Halmashauri ili kuanza uwekezaji.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kuja na Mwongozo na kanuni za biashara ya *carbon*. Hamasa ya kupanda miti ni kubwa, napongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo na ufinyu wa bajeti yapo masuala ambayo kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia tunaweza kufanikisha mengi. Na hapa nina ushauri ufutao:-

Kwanza, tukumbuke kwamba tumechelewa sana kama Taifa kunufaika na mifuko ambayo ninahitaja mara kadhaa, kama *GCF, GEF, AP* na kadhalika; na hii tukiwa *honest* inatokana na ukweli kwamba ndani ya Serikali tuna tabia na hulka ya kujifungia, yapo mambo lazima tufanye *engagement,* tuwe na *partnership*, ikiwa Mheshimiwa Rais ameonesha njia katika kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia na sisi tunao wajibu wa kufuata nyayo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika *COP 27* baadhi ya asasi na *NGOs* zilifanya jitihada za kukutana na Mfuko wa *GCF,* na tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, *Climate Action Network* wanayo *concept note* ya *USD 380M*

*jointly with* ambayo fedha ikipatikana utekelezaji wa mradi utafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Mifugo na Mamlaka ya Hali ya Hewa. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa 22 na mradi utawafikia karibu 70% ya wakulima wadogo, wafugaji na jamii za wavuvi na fedha hii zaidi ya 65% itakwenda Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa nilizonazo *GCF* walithibitisha kupokea andiko wakashauri ili kukidhi vigezo, linapaswa andiko liwe kwenye *luggage* za kitaaluma kadri ya mwongozo vya *GCF.* Moja ya ushauri ni Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira wafanye mawasiliano na *GCF* kuomba *support* ya kupata Mshauri Mwelekezi na *GCF* wako tayari kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba suala hili lipo kwenu toka mwaka jana mwishoni na uzuri linafanywa kwa ushirikiano na Wizara ya Afya, hata hivyo hakuna kinachoendelea. Huu ndio msingi wa hoja yangu kwamba tunachelewa sana kufanya maamuzi, tupunguze kujifungia, ninawasilisha kwa maandishi kwa sababu kwa maadili nisingependa kuyazungumza kwa kuongea, lakini nitashukuru ikiwa ushauri huu Serikali itaufanyia kazi kwa kuwa wepesi katika kushirikiana na sekta binafsi na kuwa wepesi kimawasiliano, tupunguze urasimu.

Pili ni kuhusu biashara ya *carbon;* napongeza sana kuja kwa kanuni na mwongozo, hata hivyo bado tunahitaji kuwekeza katika utaaalam na ushawishi. Suala hili linahitaji utaalam wa hali ya juu sana hasa katika kupiga mahesabu husika.Ninaamini kuwa tukijipanga vema, tunaweza tukapunguza kukata miti, kwa sababu wananchi ikiwa watanufaika na biashara ya *carbon,* watapanda miti zaidi na iliyopo, wataitunza kwa umakini mkubwa sana. Kwa hiyo, narudia tena ushirikishwaji wa sekta binafsi na *NGOs* ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zuio la matumizi ya mkaa 2024 *vs* uwekezaji kwenye nishati mbadala; Mafinga tulikuwa na viwanda vitatu vya kuzalisha mkaa *(Briquettes charcoal)* ambao ni bora na rafiki kimazingira. Hata hivyo katika viwanda hivyo, viwili vimefungwa, kimebaki cha *Briquettes Energy Solution* ambacho hata hivyo kinauza mkaa nje mpaka Ujerumani na uhitaji ni mkubwa sana. Ushauri wangu, viwanda vya aina hii tuwe na mpango mkakati wa kuvijengea mazingira rafiki ya kiuwekezaji, lakini kwa kuwa pia zinashiriki kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwa sababu zinatumia mabaki ya mazao ya misitu, zinastahili kupata fedha kutoka mifuko husika, lakini pia kuna mkanganyiko kwamba fedha za *carbon* ni kwa ajili ya misitu ya asili, je, ukweli ni upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaalam *vs* ushawishi wa kisiasa hasa kikanda; ili kupata fedha hizi kunahitajika utaalam lakini ushawishi wa kisiasa, hasa kikanda, kwa mfano kupitia *EAC, SADC* na hata *AU,* kwa sababu kutengwa fedha ni jambo moja, lakini kuzipata ni jambo la kipekee. Mfano mzuri ni Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi kule Simiyu, nyote mnafahamu mzunguko uliotumika kuzipata fedha hizo, nashauri ushirikiano ndani ya Serikali na nje ya Serikali na ndio maana nasisitiza lazima ndani ya Serikali tuwe *open,* tuwe *sharp,* tukubali ushauri na tuwe wepesi kufanya *engagement,* hii itasaidia sana kupata fedha kutoka mifuko niliyoitaja lakini pia tukijipanga na suala zima la *Loss and Dama Fund* kwa sababu majanga ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake kuu na neema zake za kila namna. Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia pumzi hata tukapta fursa ya kujadili Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopeleka fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo kwa namna anavyoingoza Wizara hii akisaidiana na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kupongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa kuja na mpango wa kujenga kuta katika maeneo yetu ya mwambao na katika visiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe mpango huu uwe endelevu na uangalie maeneo mbalimbali ya pwani ya nchi yetu. Niiombe Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ifikirie kujenga ukuta ili kuzuia athari za kimazingira katika Mji Mkongwe wa Kilwa Kivinje ambao ulijengwa tangu wakati wa utawala wa kikoloni na sasa umebomoka. Kwa kufanya hivi tutaweza kuhifadhi ardhi ya mji huu na kufanya makazi ya watu, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, maeneo ya biashara na viwanda vilivyopo katika Mji wa Kilwa Kivinje, kuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nichukue fursa hii nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwenye upande huu wa kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, lakini zaidi katika suala zima la mazingira. Tumekuwa tukiona mara kwa mara amekuwa akienda katika Mikutano mbalimbali ya Kimataifa kuiwakilisha nchi yetu hasa kwenye suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliamua nisimame hapa nizungumze baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba mengine yalikuwa ni ushauri, lakini bahati nzuri mengine wanahitaji wapate ufafanuzi kuona kwamba kama Serikali ni jitihada gani ambazo tumezichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo hili ambalo limezungumzwa na Profesa Manya, suala la mitetemo na suala la changamoto za uchafuzi wa mazingira hasa kwenye masuala ya viwanda. Niseme tu kwamba sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, zipo jitihada mbalimbali ambazo tumezichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tumeshatoa maelekezo kwa upande wa makelele, tumekaa na nyumba za ibada, wenzetu ambao wengi wao wanakuwa wanapiga hayo makelele, lakini tumekaa na wamiliki wa baa, tumekaa na wamiliki wa maeneo na vitu vingine ambavyo kwa njia moja au nyingine wanasababisha hili suala zima la uwepo wa makelele yanayosababisha mpaka watu kushindwa kupata usingizi kama alivyosema katika nchi ya wastaarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza baada ya sisi kutoa maelekezo, Maafisa wetu wa *NEMC* tayari wapo *field* wanafuatilia na kusimamia yale maelekezo ambayo kama Wizara tumeyatoa. Kwa hiyo, niwaambie tu Wahemishimiwa Wabunge hili jambo sasa tunakwenda

kulikomesha kulifanyia kazi kama ambavyo wananchi wantaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda tayari tulishatoa maelekezo. Kwanza tulishawaelekeza wamiliki wote wa viwanda nchini wahakikishe kwamba wanatengeneza na kuweka mifumo rafiki ambayo itakuwa iko salama kwao na kwa wananchi, mifumo ambayo inatirisha maji. Kwa sababu ni kweli tulishuhudia baadhi ya viwanda wanatiririsha maji kwenye vyanzo vingine vya maji na maeneo mengine ya makazi ya wananchi, kitu ambacho kimekuwa kero kwa wananchi. Kwa hiyo, tumekwishatoa maelekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwahi pia kutoa maelekezo na tunaendelea kusimamia maelekezo yetu kuhusu suala zima la utoaji wa moshi na sumu nyingine katika viwanda hivi. Lengo na madhumuni ni wananchi wetu waweze kuishi katika maisha ya furaha zaidi kwa hiyo, niwambie tu Waheshimiwa Wabunge, suala la kero ya makelele, moshi, maji machafu na kero nyingine katika viwanda vyetu tumeshalifanyia kazi na utekelezaji umeanza na hivi tunavyozungumza vijana wetu wako *field* wanasimamia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuja hapa hoja ya visiwa. Ni kweli niseme kwamba hii ni changamoto na niwambie tu kwamba kwamba tayari Serikali kupitia Ofisi ya Makamau wa Rais, tumeshaanza kujenga kuta kwenye baadhi ya maeneo. Tumeanza kule Kwesekwese Pemba, tumeanza kule Mikindani, Mtwara na niwambie tu wale wote ambao wana changamoto hizi, tutakuja tufanye utafiti lakini pia tutahakikisha kuwa tunatenga fedha kwa ajili ya kujenga hizo kuta. Kwa sababu athari za haya maji kuingia kwenye vipando, kuingia kwenye maeneo ya makazi imekuwa ni changamoto. Jambo la Nungwi tumeliona na maeneo mengine tumeyaona tunaomba Waheshimiwa Wabunge na

wananchi wao waendelee kuwa na Subira, Serikali tunarafuta fedha kwa ajili ya kujenga hizo kuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuja hapa vile vile hoja ya kwamba tuongeze fedha zaidi katika fungu la Serikali *rather than* kukaa na kutegemea kutoka kwa wafadhili. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge tu kwamba, miradi hii ina sehemu nyingi, sio kwamba tunategemea eti kutoka kwa wafadhili tu. Kuna miradi ambayo inatekekelezwa na *NEMC* ambayo ni Serikali, kuna miradi ambayo inatekelewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo ni Serikali. Sasa hilo fungu ambalo linatoka nje sio kwamba tunakwenda tu, lakini ni kutokanana makubaliano ya Kimataifa ambayo tunakubaliana wakati tunapokwenda kukaa katika vikao vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi ni lazima fedha hizi wao wazitoe kwa sababu asilimia kubwa ya uchafuzi wa mazingira, ukiangalia na ndio maana wanakubali kutoa fedha hizi kwa sababu ni wao ndio wanatuchafulia mazingira ya anga na mazingira mengine. Kwa hiyo, niwambie tu Waheshimiwa kwamba wazo hili tunalichukua tunakwenda kulifanyia kazi, tutajitahidi tuongeze fedha kwenye hili fungu la Serikali ili tuimarishe miradi ile ambapo tutahisi fedha kutoka kwa wafadhili hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea tumepata pia hili jambo la kulipa kodi lile ambalo Waheshimiwa wanalalamika kwa upande wa Muungano. Nataka niwambie Waheshimiwa kwamba, kwanza nataka watu wafahamu kwamba Muungano huu ndio wengi wetu umetuleta hapa, sisi wengi wetu ni wanufaika wa Muungano huu. Wakati tunajibu maswali pale tulieleza kwamba kero hizi zilikuwa nyingi, lakini leo tumekwishafika kero 22, zimebakia kero nne, kero ambazo tayari timu zetu ziko katika vikao vya majadiliano ili kuhakikisha kwamba tunachanganua kero hizi. Sidhani kama Muungano huu unaweza ukadumu kwa zaidi ya miaka 50 halafu ukawa

una changamoto nyingi *rather than* mafanikio. Kwa hiyo, wakati tunahesabu changamoto za Muungano huu, basi tuhesabu zaidi mafanikio ya Muungano huu. Wapo waliosema kwamba wengine wana asili ya pande zote mbili kwa sababu ya umuhimu wa Muungano huu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Kwa hakika leo katika Bunge lako tumeshuhudia mjadala mzuri uliogusa upande wa Mazingira, lakini na upande wa Muungano. Pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa aliyoifanya na anaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe ambao wamenipa dhamana ya kuweza kuhudhuria katika Bunge hili, kwa hakika sina cha kuwalipa Mungu ndiye atakae walipa. Pili, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nilivyosema awali, Makamu wa Rais kama kiongozi wangu katika Ofisi lakini halikadhalika Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikishukuru sana kiti chako hiki ndicho kimetuendeshea mjadala mzuri sana katika sehemu

nzima ya Muungano na Mazingira. Nipende kuishukuru familia yangu kama nilivyosema awali kwa utulivu mkubwa wanaonipa ili niweze kufanya kazi yangu ya kutimiza majukumu haya ya kitaifa, Nawashukuru sana familia yangu kwa ujumla. Niwashukuru pia Mabalozi wa mazingira na wadau wote mbalimbali wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri zimekuja hoja mbalimbali na katika hili tumepata hoja kutoka katika Kamati zetu, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, halikadharika Kamati ya Maji na Mazingira. Naomba niwahakikishie Wanakamati kwamba yale yote ambayo yametolewa kama maoni ya kamati, ni jukumu la Ofisi yetu kuhakikisha kwamba tunaenda kuyatekeleza na hasa kuangalia masuala yale ya kuwakilisha upande wa Muungano na Upande wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hususani katika Kamati ya mazingira nilikokoteza ajenda ya upande wa Bajeti halikadhalika lakini *NEMC* kuwa mamlaka kuondokana na hadhi iliyo nayo sasa hivi. Naomba niwahakikishie katika suala zima la kuifanya *NEMC* kuwa Mamlaka, sasa hivi tunapitia Sheria yetu ya Mazingira, Sura Namba 191 na katika hili eneo hilo lipo na linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba eneo hili linafanyiwa kazi kwa kina, vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hoja yetu hii imechangiwa takribani 11…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yetu imechangiwa na wajumbe 11, ukiacha wawili ambao ni Wenyeviti wa Kamati, lakini tisa waliongea moja kwa moja

hapa Bungeni ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru maoni yote yaliyotolewa, kwa upande wangu nasema haya yote ni maoni *especially* katika upande wa mazingira. Kulikuwa na suala zima la bajeti. Ni kweli tumeliangalia tumeona hata katika Kamati, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati waliliona hili. Hata hivyo, tumesema kwamba tumeanza tulikotokea, ukiangalia bajeti yetu tulianza na bajeti ya ndani wastani wa milioni 400 na huko nyuma ilikuwa hakuna kabisa, leo hii tumefika *1.6 billion*. Katika hili tumshukuru sana Mheshimiwa Rais hasa katika kutafsiri maana ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwambie Waheshimiwa Wabunge, ukiachia hii bajeti inayopita katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo sisi kazi yetu kubwa ni suala zima la uratibu upande wa mazingira. Wizara mbalimbali za kisekta zimekwenda kutekeleza suala zima la ajenda ya mazingira na hii ndio maana nasema tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia katika bajeti ya mazingira, tumechimba malambo, ujenzi wa visima virefu katika maeneo mbalimbali, lakini maelekezo ya Mheshimiwa Rais katika Wizara za Kisekta ndio maana kupitia Wizara ya Kilimo kwa mfano, imetangaza kandarasi za ujenzi wa malambo takribani 10 yenye wastani wa Shilingi Bilioni 100. Yote hii ukiunganisha Wizara za Kisekta fedha ambazo Serikali imeelekeza katika Sekta ya Mazingira ni fedha nyingi zaidi. Hata hivyo, tumechukua *concern* ya Kamati na *concern* ya wajumbe. Ni kweli kazi yetu kubwa sasa katika Ofisi ya Makamu wa Rais, baadaye kuona ni jinsi gani tunapata bajeti kubwa ya kutosha ili kusaidia baadhi ya miradi mingine ya mazingira iweze kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara ya Mifugo halikadhalika, tumeona katika maeneo ya Simanjiro kule tumejenga mabwawa na malambo ya kunywesha mifugo. Pia Wizara ya Mifugo imetenga bajeti kubwa vile vile kwa upande wa mifugo, lengo letu ni nini? Ni kuhakikisha jinsi gani kazi zote kwa pamoja zinasaidia katika ujenzi wa shughuli za mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni suala zima la biashara ya hewa ya ukaa. Ni kweli naomba niwaambie ndugu zangu Wabunge, tulikotoka mwanzo ni kwamba hapa tulikuwa kabisa hatusomeki vizuri, ni halmashauri pekee ya Tanganyika ilikuwa inasomeka kwa mwaka inapata *collection* takribani kwa wastani wa Shilingi Bilioni tatu kwa Mwaka. Ni fedha nyingi zaidi, ndio maana Ofisi Makamu wa Rais iliamua kuandaa mwongozo na kanuni kama nilivyosoma katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna Kanuni ya Biashara ya Hewa ya Ukaa. Imani yetu kubwa katika kupitia biashara hii ya hewa ya ukaa na kanuni tulizozitengeneza, tutakwenda kufungua mlango mpana wa upataji wa fedha itakayosaidia miradi mbalimbali na hususani miradi ya kimazingira. Katika hili nipende kuipongeza Halmashauri niliyoisema ya Tanganyika, kwa kweli imeonesha mfano ndani ya nchi yetu. Naomba niwambie Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Idara ya Mazingira na Kituo chetu cha *Carbon Monitoring Centre* hivi sasa tunafanya *registration* ya watu wanaokuja kwa ajili ya biashara ya hewa hii ya ukaa na hili ndugu yangu Chumi aliuliza, je, hivi sisi tunaopanda miti tunahusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwambie biashara hii ya hewa ya ukaa itawahusu watu wa *TFS* ambao wana misitu inahifadhiwa, itahusu halmashauri yenye Misitu ya Halmashauri, itahusu vijiji vyenye Misitu ya Vijijii, itahusu watu

binafsi wenye misitu yao waliyoipanda wao wataingia katika biashara ya hewa ya ukaa. Kanuni ziko wazi katika eneo hili, niwaombe Watanzania hii ni fursa kubwa sana kwamba nchi yetu tunakwenda kufungua mlango mwingine mkubwa wa kujenga uchumi kupitia biashara ya hewa ya ukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lingine ambalo lilizungumziwa hapa ni suala zima la uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro. Ni kweli Mlima Kilimanjaro ni tunu yetu tuliyokuwa nayo, ni lazima tuilinde. Bahati nzuri mwaka 2022 nilishiriki wakati tulipopata ile changamoto ya moto na kweli hali ilikuwa ni mbaya. Ndio maana sisi kupitia ofisi yetu tuliamua tutengeneze utatu *TFS*, Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini wenye Mamlaka ya kuhifadhi huo Mlima ambao ni wenzetu wa *KINAPA* na jambo linaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu hiyo imeanza kuratibu vizuri na *concept paper* imeshaanza kuandikwa na naomba niwambie Watanzania, tunaenda kufanya tafiti kuangalia ni jinsi gani tunaweza kuilinda barafu ya Mlima Kilimanjaro, kwa sababu hii ndio tunu yetu ambayo inatuletea utalii mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine ni upande wa Muungano. Nishukuru sana hoja mbalimbali zimeletwa katika Muungano, naomba niwahakikishie kama alivyosema Naibu wangu hapa ni kwamba tumefanya kazi kubwa na katika hili tumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mchakato wa kushughulikia hoja za Muungano ulianza toka mwaka 2006, mwaka 2010 hoja mbili za Muungano zilipatiwa ufumbuzi na mwaka 2020 hoja tano. Kwa hiyo, kati ya hoja 25, katika hiyo miaka yote zilitatuliwa hoja saba tu za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan ndani ya miaka miwili ni hoja takribani hizi tunazosema 18 tumeongeza zile hoja zingine sasa hivi, hii yote ni kazi kubwa

imefanyika ndugu zangu. Katika hili mnyonge mnyongeni, lakini Mama Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Ali Mwinyi wamefanya kazi kubwa kutatua hizi hoja za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu bado kuna makandokando mengine na hasa usafirishaji wa mizigo. Hili tulikubaliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na hasa mambo haya mengine ni mambo ya uratibu tu na kiutendaji na hili Wizara ya Fedha wamesema wanalichukua kwenda kulifanyia kazi. Imani yangu, hizi kero tunazoziona sasa hivi kwa kadri tulivyokubaliana jambo hili tutapata ufumbuzi na tutaondoa kabisa kero hizi ndogo ndogo ambazo tunasema ni *petty issue* katika mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ajira haya tutayafanyia kazi, tunashukuru ushauri wenu tunaenda kuratibu vizuri kuangalia katika taasisi zetu za Muungano, lengo letu ni kuufanya Muungano wetu kuwa rafiki zaidi, naomba niwaambie Muungano wa Tanzania ni *unique,* leo hii tuko humu ndani huwezi ukamtofautisha Wakojani wala huwezi ukamfananisha wa Bagamoyo wala wa Kakonko wote tuko pamoja hapa, hakuna nchi ambayo inanufaika na matunda mazuri kama haya ya Muungano tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu letu kubwa ni kuuenzi Muungano wetu na hasa ndugu zangu nawaambia kazi kubwa wanayofanya Viongozi wa nchi yetu, tuwaenzi kwa hii tunu waliyotupatia tuendelee kuulinda Muungano wetu. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameelekeza mwaka huu sherehe ya Muungano mwaka huu isherekewe tofauti kila Mkoa watu washerehekee Muungano wafungue miradi, wapande miti na mambo mengine yote, jambo hili maana yake tunaleta urafiki, humu leo Bungeni watu wameoana Bara na Visiwani, hongera sana kwa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya ndugu zangu naomba nishukuru sana, hoja zote tumezichukua kwa ajili ya kuzifanyia kazi naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI-KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 - Makamu wa Rais**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*................................Sh.14,731,640,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa kuna mshahara wa Waziri na kuna majina, tunaanza na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Moja kati ya taka ambazo zinachafua mazingira na zinaathari kubwa kwa binadamu na mimea na wanyama ni taka ambazo zinatokana na *plastic,* kwa sababu kwenye ardhi hazimeng'enyeki na hivyo haziji-de*compose,* pia wanyama au zikiingia kwenye bahari zinatengeneza

*microplastics* ambazo ni *harmful* kwa samaki hata kwa binadamu ambao tunakuja kula hao Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua na nisipopata *commitment* ya kutosha kutoka kwa Waziri nitashika Shilingi. Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 30 ameeleza thabiti kwamba kaulimbiu ya mwaka huu ni *bit plastic pollution,* Tanzania tuna Sheria ya Kuzuia Matumizi ya Mifuko ya *plastic* na zile *plastic bottle*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kupata *commitment* kwanza ni *enforcement* ya hiyo sheria, lakini kuja na sheria ya kuzuia sasa matumizi ya *single use plastics*. Zile *plastics* ambazo zikishatumika haziwezi kutumika tena kama vile *disposable things,* kama hivi vikombe vya *plastics* tunavyotumia sana kwenye masherehe. Nchi za wenzetu mfano Rwanda wameshaondoa kabisa hizo *single used plastics* wenyewe wanatumia *paper bags* ambazo ni *disposable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua *commitment* ya Serikali ya kuleta sheria ya ku-*ban single used plastics* kama ilivyofanya kwenye mifuko ya *plastics.* Ni lini sasa Serikali italeta sheria kuzuia matumizi ya hizi *plastics (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa na nimshukuru sana Dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko kwanza kwa kuonyesha kwamba suala la *plastics* ni changamoto kubwa na ndiyo maana katika hili unaona tumejipambanua dhahiri kwanza. Siyo hivyo tu, tukumbuke hivi karibuni nilitoa maelekezo mpaka kwa *NEMC* kusema hata watu wao wa Kanda wakishindwa

kutimiza wajibu wao maana yake itaonekana kwamba hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Kauli hii ni mwangwi wa kwamba hatuhitaji suala zima la *plastic,* ushauri wako wa suala zima la zile *single used plastic*, maana yake tunataka zile *plastic* ziwe *recyclable,* ndiyo maana ukiangalia tumeelekeza suala zima watu wanaotengeneza hizi bidhaa sasa ziweze kuwa zinaweza kurejeshwa kabisa, ambazo hazirejesheki kwa mujibu wa kanuni tuliyokuwa nayo ya mwaka 2019 haziruhusiwi kuingia masokoni, kwa hiyo Mheshimiwa Dada yangu Matiko nadhani tuko pamoja kabisa na naomba nikuhakikishie mimi katika hili sina masihara kabisa na ndiyo maana tumetoa maelekezo mazito zaidi kwa ajili ya kuhakikisha jambo hili linakaa vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa bado upo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Waziri hakunielewa vizuri kabla sijaelekea kwenye kushika Shilingi. Nilichokuwa naomba kwa Tanzania ya sasa hivi hata ukienda kwenye *supermarket* yoyote ile utakuta zile *disposable equipment* ni za *plastic* ambazo haziwi *decomposed.* Kwenye nchi za wenzetu mfano Rwanda na Kenya wanafuatia wanatengeneza *disposable stuff* ambazo ni za makaratasi siyo za *plastic,* sasa nikasema kama ulivyo *burn plastic uses* hapa Tanzania, ije sheria ya kutozalisha wala kusambaza hizo *disposable stuff* ambazo ni *single use plastics* Tanzania bado zipo, hata tukiondoka na wewe hapa tukaenda kwenye *supermarket* pale tutazikuta nyingi sana zinatumika, hata nikiwa na sherehe nitazitumia hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mbunge anataka *commitment* ya kama wanavyofanya nchi zingine. *Commitment* tu basi.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa Mheshimiwa Matiko na hili halina shida, sawa Serikali tumekuwa *committed* katika hilo na tutaenda kulirudia vizuri kanuni zetu kama kuna *gap* vizuri tutarejea kanuni zetu, lengo kubwa kwenda kubana kila kitu ambacho kinaleta madhara katika nchi yetu *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na kwamba tunategemea fedha za nje zaidi katika miradi ya maendelao, lakini hata hizo za nje tunashindwa kuzi-*access* kama ambavyo tunastahili kwa sababu tunashindwa ku-*comply* na mahitaji ya wanaotu-*fund* kuna *procedure* ambazo ni lazima ku-*comply*. Kwa mfano, tunatakiwa tupeleke *proposals* lakini pia tunatakiwa tuna *clear institutions* kwa ajili ya kupata hizo fedha, hususani kwenye Mfuko wa *Green Climate Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *commitment* ya Serikali kwa sababu haya mambo ni mambo ya ndani ya kwenye mfumo ya kwenye Serikali ambao wanaweza kuya-*manage* wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *commitment* ya Serikali kwenye kuhakikisha kwamba hatujikongoji inapokuja *procedures* za kufuata ili tukachukue zile fedha, kwa sababu tunaonekana ni kwamba hatu-*comply on time* ndiyo maana hatupati fedha *on time*. Kama sasa hivi, kabla ya bajeti kuja tulitegemea kwamba wawe wameshamaliza wameshapeleka *proposals* za miradi ili iende sambamba na bajeti zetu tayari tuwe na vitu ambavyo tayari viko kwenye *process* ili tupate hizo fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Dada yangu Mheshimiwa Nusrat Hanje kwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikuwa hatufanyi vizuri katika eneo hilo na mwaka jana tulikuwa na kikao *block* yote ya *SADC* kwa ajili ya kuzungumza hizi fedha ni jinsi gani tutazi-*access* kwa sababu inaonekana *capacity* ilikuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa jambo ambalo hata wenzetu *World Bank* tulikuwa na kikao mwaka jana ya jinsi gani tutatengeneza *capacity* ya kuweza ku-*qualify* katika hii Mifuko. Hili naona tunaenda vizuri sasa hivi. Tunashukuru sana taasisi yetu ya *CRDB* ambayo sasa hivi imekuwa *accredited,* hata hivyo tunataka TAMISEMI, Wizara ya Fedha na baadhi ya Taasisi nyingine kuweza kuwa na sifa hizo kwa ajili ya kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie takribani mwezi mmoja na nusu hivi tulikuwa na kikao na wadau wote wa mazingira kwa ajili ya kuhakikisha jinsi gani tunapata fedha kwa pamoja na naomba niwahakikishie Mheshimiwa Nusrat ulichosema ni kweli na hivi sasa tumefanya kazi kubwa ya kuboresha hilo jambo baada ya kuona kwamba kulikuwa na *gap* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Kifungu hicho kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*...............................Sh. 5,449,047,600
Kifungu 1002 – *Finance & Accounts Unit*..............Sh. 606, 909,100
Kifungu 1003 - *Policy & Planning Division*...........Sh. 1, 331,047,600
Kifungu 1004- *Government Communication Unit*.................................................Sh. 523, 368,700
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*............................Sh. 553,561,500
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*...Sh. 708,349,500
Kifungu 1007- *Information & Communication Technology Unit*.....................................................Sh. 465,736,300
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*...........................Sh. 722,004,200
Kifungu 2001- *Union Secretariat*...........................Sh. 1,709,757,600
Kifungu 5001- *Environment*..................................Sh. 8,642,616,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration & Human Resources Management*...............................Sh. 2,002,000,000
Kifungu 5001- *Environment*.................................Sh.16,656,045,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zote. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri sana, vilevile Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wewe na Naibu Waziri

mmefanya kwenye Wizara yenu mkisaidiwa na Katibu Mkuu na watu wa *NEMC*. Ninampongeza vilevile Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* Dkt. Mwafwenga kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini tuwaombe *NEMC* suala la makelele kwenye maeneo ya makazi ya watu imezidi. Watu wanakereka watu wanaugua, wazee wengi wanateseka sana na kelele ya miziki ambayo wala haina *control* yoyote. Kwa hiyo tunaiomba *NEM*C mlifuatilie na mtoe adhabu kali kwa watu wanaokiuka taratibu za uchafuzi wa mazingira hasa kwenye kelele.

Ninawapongeza sasa rasmi bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira imepitishwa rasmi, hongereni nendeni sasa mkafanye kazi. Pia tunampongeza Mama Jafo pale juu kwa kumtunza vizuri Mheshimiwa Waziri na saa nyingine utasamehe ziara zake ni nyingi Zanzibar – Pwani.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge wanakaribishwa kupata elimu inayotolewa na *RITA* kuhusu Uandishi wa Wosia na upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kuanzia Tarehe 24 Aprili – 05 Mei, 2023 nyuma ya Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi *(Makofi)*

*(Saa 7.14 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*